Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Tisa - Tarehe 23 Juni, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 80

### Matokeo ya Tume ya Kuchunguza sababu za ajali mbaya ya Treni

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

(a) Je, Tume iliyoundwa kuchunguza chanzo/sababu za ajali kubwa ya treni imebaini nini katika uchunguzi wake?

(b) Kwa kuwa walioathirika na ajali hiyo walilipwa mpaka mwisho wa mwezi wa nne; na kwa kuwa baadhi ya waathirika wanaoishi vijiji vya mbali ni vigumu taarifa ya ukomo wa muda wa malipo kuwafikia; je, Mbunge wao anaweza kuwawakilisha wananchi wa aina hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kahumbi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, tarehe 24 Juni, 2002 katika eneo la Msagali karibu na Dodoma, ilitokea ajali ya gari moshi la abiria lililokuwa linatoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza na Kigoma. Gari hilo lilikuwa na mabehewa 22 na abiria zaidi ya 1,200. Uchunguzi uliofanywa na Tume ya Jaji Msoffe, umeainisha kuwa chanzo cha ajali hiyo hakikutokana na uhalifu wowote, bali makosa ya kiufundi na uzembe wa dreva. Kichwa cha treni hiyo Na. 3901 kisingeweza kuhujumiwa kwani hakuna aliyetegemea kuwa kingefungwa kwenye gari la abiria siku hiyo baada ya kile ilichotoka nacho Dar es Salaam kuharibika na kubadilishwa Morogoro. Taarifa hiyo inabainisha kuwa wingi wa vifo na majeruhi umetokana na mwendo wa kasi sana wakati gari moshi linarudi nyuma, kujaza abiria kupita kiasi hasa mabehewa ya daraja la tatu, ukosefu wa huduma ya kwanza na uduni wa zana za uokoaji kama vifaa vya kukatia mabehewa.

(b) Mheshimiwa Spika, zoezi la kuwatambua wahanga wa ajali hii lilianza rasmi tangu Julai, 2002, ambapo Serikali iliamua kutoa pole ya Sh. 500,000/= kwa wale waliopoteza ndugu zao na Sh. 100,000/= kwa wale walioumia na kulazwa hospitalini. Serikali ilitoa mwongozo wa kutekeleza zoezi hili mwezi Septemba, 2002. Kati ya tarehe 5 - 18 Septemba, ilikuwa kutoa matangazo kwa umma kupitia Vyombo vya Habari na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Ni katika kipindi hicho hadi tarehe 30 Septemba, 2002 ambapo wananchi walitakiwa kuwasilisha majina ya wahanga, pamoja na maelezo katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya zao. Kati ya tarehe 1 - 15 Oktoba, 2002 Wakuu wa Wilaya walitakiwa kuwasilisha majina ya wahanga kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yao, ambao nao walitakiwa kuyawasilisha Idara ya Uratibu wa Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu kati ya tarehe 16 - 31 Oktoba, 2002. Kutokana na Serikali kuwajali wananchi wake hasa walio vijijini, zoezi hili badala ya kuishia mwezi Desemba, 2002 liliongezewa muda hadi 30 Aprili, 2003. Ni matarajio ya Serikali kwamba, waliokuwa wamechelewa awali walipata muda wa kukamilisha madai yao.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao walichelewa kuwasilisha hadi tarehe hiyo ya mwisho, Serikali haiwezi kuongeza muda tena kwani muda huo wa miezi minane iliyotolewa ingetosha. Aidha, Mbunge hawezi kuwawakilisha wahanga wa Jimbo lake kwani fedha zote zimetumwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa wanaohusika na malipo yanafanywa kwenye Ofisi za Makatibu Tawala wa Wilaya wanakotoka wahanga.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili limefungwa rasmi tarehe 30 Aprili, 2003 na jumla ya majina 826 yalikuwa yamehakikiwa. Kati yao waliokufa ni 282 na waliojeruhiwa ni 544 na jumla ya fedha zilizolipwa ni Sh.195,400,000 na mtu mmoja akapatiwa mguu wa bandia wenye gharama ya Sh.440,000.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yanayoonyesha Serikali kuwajali watu wake, lakini hapa nina ushahidi wa watu watatu waliokufa katika ajali hiyo, ambao hawakulipwa na hatua zote alizozisema zimepitiwa. Pia nina watu watatu ambao waliumia katika ajali hiyo na wamepeleka malalamiko yao kwa Katibu Tawala wa Mkoa lakini hawajalipwa.

Sasa je, kosa hili ni lao au ni la Watendaji ambao wanasema wao wamewasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, sasa hawawezi kufikiriwa hawa watu kulipwa fidia yao na majina yao ninayo?

Pili, kwa kuwa hata wahanga wa meli vilevile wapo ambao hawajalipwa, ninalo jina la mtu ambaye hajalipwa, je, naye inakuwaje kwa sababu anachoambiwa ni kwamba lazima alete mafaili yake yote yanayoonyesha kote alikopitia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa pamoja ningeweza kusema kwamba, pamoja na kufunga zoezi hili, lakini namruhusu Mheshimiwa Mbunge, anipatie hivyo vielelezo ili tuweze kuvichambua na kuviangalia, kama viko katika kumbukumbu zetu tutawatendea haki hao wahusika. Kwa bahati njema viongozi niliowataja wote Makatibu Tawala na Wakuu wa Mikoa, wako hapa leo katika bajeti yetu, tutashirikiana katika kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amesema sababu kubwa ya ajali ile ni uzembe wa dreva. Je, Serikali imechukua hatua gani za tahadhari kwamba uzembe wa namna hiyo usirudiwe pamoja na hatua za kinidhamu dhidi ya dreva aliyefanya makosa hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua kutokana na uzembe uliosababishwa na dreva anayeitwa Ndugu Godfrey Kiwelesa. Baada ya ripoti ile kubainisha kwamba kulikuwa na uzembe, Serikali kupitia Shirika lake la *TRC* lilimfukuza kazi. Lakini pia wako wafanyakazi waliohusika na kubainika akiwemo *Station Master* wa Morogoro, naye aliadhibiwa kwa kushushwa ngazi katika nafasi yake ya kazi. Lakini hatua mbalimbali za kinidhamu zilichukuliwa katika njia nzima ya reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma.

Na. 81

**Televisheni ya Taifa (TVT)**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa ni vigumu kwa Televisheni ya Taifa (TVT) kuonekana nchi nzima katika miaka ya hivi karibuni; na kwa kuwa baadhi ya Televisheni binafsi zina uwezo na ari kubwa kuliko Serikali na kuzifanya Televisheni zao zionekane nchi nzima katika kipindi kifupi na kwa gharama nafuu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba sheria inayotaka Televisheni binafsi kurusha matangazo yao katika asilimia 25 ya Mikoa yote nchini imepitwa na wakati?

(b) Je, ni lini sheria hiyo itarekebishwa ili kuondoa dhana kwamba endapo Televisheni binafsi zitaonekana nchi nzima itakuwa ni kuiaibisha Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la kuwaruhusu wenye Redio na *TV* binafsi kusambaza matangazo yao nchi nzima linategemea sana sera ya nchi kwa kuainisha vigezo mbalimbali muhimu, likiwemo suala la usalama. Kwa msingi huo, Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana nami kuwa suala lililopo siyo sheria hiyo kupitwa bali kuwepo kwa Sera ya Habari na Utangazaji inayozingatia maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Uingereza ni *BBC* pekee ndiyo inayoruhusiwa kusambaza matangazo yote nchini kote kwa kutumia vituo vya kurushia matangazo. Vituo vya binafsi vinaruhusiwa kujenga mitambo ya kurushia matangazo katika maeneo fulani tu. Kadhalika Marekani wanao utaratibu unaoruhusu vituo binafsi kuwa na usikivu na uonekanaji usiozidi asilimia 35 kwa kutumia mitambo ya kurushia matangazo, lakini siyo kwa njia ya *satellite*. Lakini *Voice of America* inaruhusiwa kutangaza nchi nzima. Nchi zenye vipingamizi na zisizo na vipingamizi, zote hutegemea sana sera za nchi zao na hasa zinazozingatia maslahi husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha Sera Mpya ya Habari na Utangazaji, ambapo suala la vituo vya redio na *TV* binafsi, kuruhusiwa ama kutoruhusiwa kutangaza zaidi ya asilimia 25 ya nchi nzima, limezingatiwa ipasavyo.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Bakari Mbonde na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilipoweka Sera ya Utangazaji inayoruhusu Televisheni binafsi kuonekana kwa asilimia 25 ya nchi nzima, hakukuwa na dhana kwamba, endapo Televisheni za binafsi zitaonekana nchi

nzima itakuwa ni kuiaibisha Serikali. Namshauri Mheshimiwa Mbunge, awe na subira kwa kuwa jambo hili litakuwa limepata ufumbuzi pindi Sera ya Habari na Utangazaji itakapokamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri hivi karibuni.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mbwembwe za Ofisi ya Waziri Mkuu na vilevile Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, kundwa *Task Force* ili TVT ionekane Dodoma, lakini kumbe ilikuwa danganya toto. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Tanzania ni nchi pekee duniani ambapo Televisheni ya Taifa haionekani Makao Makuu ya Nchi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hiyo ni kashfa na aibu kwa Taifa? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Watanzania walio wengi wanapenda mchezo wa mpira wa miguu na huangalia mashindano ya ligi maarufu duniani kupitia Televisheni binafsi kwa sababu TVT haina ubavu. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, nyakati hizo Watanzania wengi wanaangalia Televisheni binafsi kwenye mashindano ya mpira wa miguu, haoni kwamba nyakati hizo wanaoangalia TVT ni makada wa siku nyingi kama vile akina Mzee John Samwel Malecela, Mzee Pius Msekwa na wengine? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tungependa Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali iwe na mbwembwe kushinda Televisheni zote nyingine duniani na hiyo ni fahari ya Tanzania na ni fahari yetu sote. Lakini la msingi ni kwamba, tumeanza hatua kwa hatua kujenga misingi mizuri ya Televisheni kwa nchi nzima. Tumeanza na Dar es Salaam na pia Mkoa wa Pwani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bakari Mbonde, angeshukuru sana kwamba, watu wa Mkoa wa Pwani pia wanaona Televisheni ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taratibu zetu ni kwamba, tutajitahidi katika kipindi hiki kati ya leo na Desemba, Televisheni ya Taifa ionekane katika Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Lindi na kabla ya mwezi Desemba, 2004 Televisheni ya Taifa ionekane nchi nzima. Kwa hiyo, hizo ni mbwembwe za Serikali na pia ni utekelezaji mzuri wa Sera ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Bakari Mbonde, amesema kwamba, angependa kuona mchezo wa mpira wa miguu unaonekana katika Televisheni ya Taifa. Lakini pia ningependa niwapongeze sana wenye Televisheni binafsi, kwa sababu Televisheni ya Taifa haiko tayari, wamechukua nafasi hiyo ya kuonyesha michezo mbalimbali duniani. Kwa hiyo, Televisheni ya Taifa itakapokamilika itafanya yote hayo ambayo nafikiri Watanzania wangependa wayaone. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hizi ni zama za uwazi na ukweli na kwa kuwa teknolojia ya *satellite* imesambaa dunia nzima kiasi kwamba huwezi tena kuzuia mtu asione habari yoyote duniani. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, kwanza tukubali kwamba, sera ya asilimia 25 imepitwa na wakati? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Nyalandu kabisa kwamba, kuendelea kuwa na utaratibu wa kuzuia Televisheni za binafsi au Redio binafsi kuwa katika Mikoa maalum tu, umepitwa na wakati. Kwa sababu *satellite* inaweza kuonyesha nchi nzima na nje ya Tanzania. Kwa sababu hiyo ndiyo maana nimesema tusubiri wakati bado tunaiangalia sera yetu na Serikali itatoa uamuzi ambao utaweza kusaidia kupunguza kero hiyo kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Na. 82

**Uwiano wa Shule za Sekondari Kati ya Mkoa na Mkoa**

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE** aliuliza:-

Kwa kuwa uwiano wa Shule za Sekondari kwa Mkoa wa Kilimanjaro ni 1:10,000 na Kigoma ni 1:70,000:-

(a) Je, Serikali imeweka mipango ipi ya makusudi ya kuondoa tofauti hiyo kubwa katika utoaji wa elimu kwa watu wake?

(b) Je, isingekuwa busara sasa kwa Serikali kutumia sehemu kubwa ya fedha za msamaha wa madeni kujenga shule za sekondari katika Mikoa ambayo iko nyuma kielimu ukiwepo Mkoa wa Kigoma na hasa kwa kusaidia nguvu za wananchi wanapokuwa wamekwama katika kukamilisha miradi ya ujenzi wa sekondari?

(c) Pamoja na nia nzuri ya kusisitiza viwango vya miundombinu mbalimbali katika shule za sekondari zilizojengwa na wananchi, je, Serikali inaweza kulegeza baadhi ya masharti katika Mikoa iliyo nyuma sana kielimu ili nayo iweze kuwa na sekondari za kutosha?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Ruzuba Magayane, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kigezo kimojawapo kinachotumika hivi sasa kutoa kibali cha ujenzi wa Sekondari katika Mkoa au Wilaya ni idadi ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la saba na kukosa nafasi ya Sekondari, sio idadi ya watu katika eneo hilo. Kwa kipimo hicho, Wilaya inayohitaji shule nyingi zaidi za sekondari ni Kinondoni na Mkoa wenye shule chache zaidi za sekondari kulingana na wanafunzi wanaofaulu darasa la saba ni Mkoa wa Shinyanga, ukifuatiwa na Mkoa wa Dar es Salaam. Wilaya inayoongoza kwa kuwa na shule nyingi za sekondari za wananchi ni Arumeru. Serikali inaendelea kuwahimiza wananchi kujenga Shule za Sekondari ili watoto wote wanaofaulu darasa la saba waweze kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari. Aidha, Serikali inashauri upanuzi wa shule za wananchi zilizopo kutoka mikondo miwili mpaka kufikia mikondo minne, ufanywe upanuzi wa shule mpaka kufikia mikondo minne kabla ya kujenga shule nyingine.

(b) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kutoa Elimu ya Sekondari kwa usawa kwa Mikoa na Wilaya zote. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari ambao unakamilishwa mwaka huu wa 2003, utaainisha kiufundi mikakati ya kufikia lengo hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, tunapenda tuwe na Shule za Sekondari nzuri ambazo mandhari yake yatawavutia walimu na wanafunzi waipende shule yao na wanafunzi wayapende masomo wanayofundishwa. Kwa kuwa tunalenga kuwa na elimu bora, tujitahidi kuboresha mazingira ya kutoa elimu hiyo. Lengo la kuweka masharti na kusisitiza viwango vya miundombinu katika shule za Sekondari ni kuwa na shule bora zinazotoa elimu iliyo bora, itakayokuwa na manufaa kwa mnufaikaji na Taifa kwa ujumla. Serikali inapoona nia na juhudi za wananchi katika kujenga shule yao, hutoa ushauri muafaka kulingana na hatua ya ujenzi iliyofikiwa, bila kulegeza masharti muhimu ya utoaji wa elimu bora. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imefanya vizuri sana katika kuboresha Elimu ya Msingi kupitia MMEM. Je, juhudi hizo zitaendana na upanuzi wa shule za sekondari na vyuo vya ufundi katika maeneo husika ili watoto walioandikishwa darasa la kwanza wasirudi kuwa ambao hawajui kusoma na kuandika baada ya kumaliza darasa la saba?

Pili, kwa kuwa tofauti za kupatikana kwa elimu katika Wilaya mbalimbali kunaendana pia na kupatikana kwa ajira kwa vijana. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kuwa na tofauti katika Wilaya na Wilaya kwa wanaoenda shule huleta pia tofauti katika ajira na hivyo wengine hawapati ajira?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, uzoefu tulioupata katika MMEM tutajitahidi sana kuutumia katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari. Kwa mfano, moja ambalo tumejifunza ni kwamba, wananchi wakisaidiwa ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya kununulia vifaa ambavyo vinanunuliwa kutoka viwandani, matokeo tumeona wanajenga shule nzuri zaidi na kwa *speed* nzuri zaidi. Kwa hiyo, tunalenga pia katika Mpango wa Sekondari, tuuchukue huo uzoefu wa kutoa ruzuku ya maendeleo. *(Makofi)*

La pili, napenda pia nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tofauti ya elimu matokeo yake inaleta tofauti za kushiriki katika ajira zinazopatikana. Kwa sababu kila zinapotangazwa ajira zinatoa sifa za elimu, kwa hiyo, Mkoa ulio nyuma kielimu kwa kweli hautashiriki katika vijana wake kupata ajira. Pia kwa utaratibu huu wa kupanua Elimu ya Sekondari, kwa mtindo wa kufuta utashi kwa wanaohitaji, matokeo ni kwamba, walio na uwezo kiuchumi labda wana mazao ya biashara au wameendelea zaidi, ndiyo wanaofanikiwa kujenga Sekondari. Kwa hiyo, mambo yote haya tunataka tuyatazame kwa pamoja katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, ili Serikali itoe changamoto iliyo kubwa zaidi ili kurekebisha tofauti zinazojitokeza katika jamii kwa utaratibu wa sasa. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais, katika ziara yake ya mwaka 1997, katika Wilaya za Ngorongoro, Monduli, Simanjiro na Kiteto, aliahidi kwa wananchi wote kujenga sekondari moja kwa kila Wilaya, kutokana na hali halisi ya elimu katika Wilaya hizo. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa imebakia miaka miwili tu basi mambo haya yaishe? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Rais aliahidi kama alivyosema Mheshimiwa Losurutia, napenda kumshukuru kwa kunipa taarifa hiyo. Mimi naomba sana sana tushirikiane naye, leo hii tuongee nizijue vizuri hizo ahadi na tuone namna ambavyo tunaweza kutekeleza ahadi hizo kabla ya mwisho wa kipindi hiki. Ni wajibu wetu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Rais, ameahidi mahali, tufuatilie na mimi kama Waziri, nitahakikisha kwamba, ahadi hiyo inatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. JOHN SAMWEL MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kuhusu suala la kuzisaidia shule za sekondari, ningependa kumpa ombi, je, Serikali inaweza kuwafikiria wafugaji kuwapa upendeleo maalum wa kuwajengea hosteli ili watoto wao waweze kusoma kwa sababu haya makabila ya wafugaji wengi wao huhamahama kufuata maji na malisho?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Elimu kwa wote, ni kweli kabisa tunawajibika kuwa na mikakati maalum kwa makundi maalum ambayo kwa utaratibu wa kawaida hayafikiki. Katika makundi hayo, kundi mojawapo ni la wafugaji, ambao bado wanahamahama na mkakati ulio sahihi hapa kwa kweli ni kuwa na shule za bweni na ndiyo maana tuna shule za msingi tano, tano, za bweni katika Wilaya ambazo zinajulikana kuwa za wafugaji hivi sasa. Lakini nakubaliana naye kwamba, mkakati huu inabidi tuuangalie pia katika shule za sekondari na hata zile za kutwa zilizojengwa na wananchi, Serikali tushirikiane nao. *(Makofi)*

Na. 83

**Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inaandaa mpango wa kuboresha Elimu ya Sekondari kama ilivyofanya kwa Shule za Msingi. Je, Serikali itakubali kuanza mpango huo kwa kuanzia na zile Halmashauri ambazo zina Sekondari chache kama ilivyo kwa Halmashauri ya Mtwara ambayo ina Sekondari mbili tu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mtwara Vijijini inazo shule mbili za sekondari na moja ni Sekondari ya Seminari ya Kitaya. Wilaya ya Mtwara Vijijini ni moja kati ya Wilaya 15 nchini, ambazo zina shule za sekondari zisizozidi tatu. Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kuwa kuanzia mwaka 1986 jukumu la kujenga shule za sekondari za kutwa ni la wananchi wenyewe wakishirikiana na Halmashauri zao. Pamoja na hilo, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, iliyopitishwa na Bunge hili, inaelekeza kutoa elimu kwa uwiano kwa maeneo na makundi mbalimbali.

Mpango wa kuboresha elimu ya sekondari unaokamilishwa utahusu pamoja na mambo mengine, upanuzi wa elimu hiyo kwa uwiano stahili kulingana na mahitaji na malengo ya Kitaifa. Kwa maana hiyo, katika mpango wa upanuzi, Wilaya zilizoko nyuma katika kutoa elimu hiyo, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Mtwara Vijijini, zitapewa kipaumbele. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini, waendelee na jitihada za ujenzi wa shule za sekondari kama wanavyofanya Waheshimiwa Wabunge wengine na mpango nilioueleza utakapoanza utawaongezea nguvu.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni ni rafiki yangu sana na aliniahidi kwamba, atanisaidia kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nanguruwe na aliahidi mbele za watu. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufanya utafiti katika Shule ya Sekondari ya Kitaya ili kuzungumza na wananchi wa Kitaya na Uongozi wa Shule ya Kitawa ili kumaliza mgogoro wa udini uliopo kwenye shule ile au mgogoro wa vyama ulioingia kwenye shule ile ili shule ifanye kazi yake kama ilivyokusudiwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu ahadi niliyoitoa, napenda nimhakikishie ahadi ile bado iko pale pale, haikuweza kutekelezeka mwaka wa fedha tunaoumaliza, ni matumaini yangu katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, tunategemea kuipa kipaumbele.

Kuhusu swali la pili, ni mara ya kwanza ndiyo nasikia kwamba pale katika Sekondari ya Seminari ya Kitaya kuna mambo ya udini na vyama vya siasa. Lakini napenda nichukue nafasi hii kufafanua kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu iliyopitishwa na Bunge hili, yeyote anayepewa usajili wa kuanzisha Shule ya Sekondari haruhusiwi kutoa nafasi za elimu ile kwa ubaguzi wa kufuata dini au vyama vya siasa, wala kufuata ukabila na unyumbani nyumbani.

Isipokuwa kama lengo la shule ile ni kufundisha watu ambao wamelengwa kuwa watumishi wa madhehebu mbalimbali, hapo wanaweza wakachukua wanafunzi wa dini yao kwa maana ya kuandaa Wachungaji, Mapadri na Masheikh wa kufanya kazi katika madhehebu yao.

Lakini kwa Sekondari za Kawaida hawatakiwi waendeshe ubaguzi wa namna hiyo. Lakini napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini kwamba, wengi wao hata katika zile shule ambazo wamelenga kufundisha watu wao kwa maana ya dini zao, huweka nafasi za wengine kuweza kuchanganyika nao na wanachangia katika kupanua elimu. *(Makofi)*

Na. 84

**Umeme Kijiji cha Soya Wilaya ya Kondoa**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliwekwa kwenye OrderPaper kwa makosa lilikwisha jibiwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge)*

Na. 85

**Kupeleka Umeme - Sekondari ya Reginamundi**

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya Mwaka 2001/2002 ilitenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye Sekondari ya Reginamundi iliyoko Mahenge pamoja na eneo la Nawenge - Vigoi - Mahenge:-

(a) Je, kazi ya kuweka nguzo na kupeleka umeme shuleni hapo imefikia wapi?

(b) Je, upanuzi wa umeme kwenda Nawenge na Vitongoji vyake vya Vigoi Juu umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, Mbunge wa Mahenge, kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa kupeleka umeme Shule ya Sekondari ya Reginamundi, umbali wa kilomita 11 kutoka Mahenge Mjini ulikadiriwa kugharimu shilingi 175 milioni mnamo mwaka 1999. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa fedha, kazi ya kutekeleza Mradi huu haikuanza.

Mnamo mwaka 2000, *TANESCO* ilitenga kiasi cha shilingi 6,551,709.00 ili kuanza kazi hii, fedha hii ilijenga laini yenye urefu wa kilomita moja tu ya msongo wa kilovoti 33 kuelekea maeneo ya Shule ya Reginamundi. *TANESCO* ilitenga kiasi hicho cha fedha ikiwa ni sehemu ya gharama ya kutekeleza Mradi huo kufuatana na ahadi ya Uongozi wa Juu wa Kanisa la *Roman Catholic* unaomiliki shule hiyo kuwa ungechangia gharama za kazi hiyo pindi itakapoanza. Uongozi wa Kanisa kwa bahati mbaya haukutimiza ahadi yake ya kutoa mchango huo na hivyo kazi ilisimama.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika Bajeti ya mwaka 2001/2002, *TANESCO* ilitenga tena kiasi cha shilingi 40,554,530.00 ili kuendeleza kazi hiyo. Vifaa kadhaa vilikwishapelekwa Mahenge kwa ajili ya kazi hiyo. Hata hivyo, kabla ya kuvusha, vifaa hivyo havikuweza kufika kutokana na tatizo lililojitokeza la kuzama kwa kivuko.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatazamiwa kuendelea mwaka huu wa 2003 baada ya upelekaji wa nguzo na vifaa vingine na inakadiriwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2003 iwapo hakutajitokeza tatizo lingine lolote.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Nawenge, Shirika lilitenga jumla ya shilingi 22,657,577.97 mnamo mwaka 2001, kwa ajili ya kuvuta laini ya km 2 ya kilovoti 33, kuweka *transfoma* ya *50KVA* na kujenga laini ndogo za kusambazia umeme kwa wateja yenye urefu wa kilomita 0.6 kwenda Nawenge. Kazi hiyo ilikamilika mwaka 2002 na ningependa kuchukua nafasi hii kuwaomba wananchi wa Nawenge wajitokeze zaidi kulipia *Service line* ili juhudi iliyofanyika ya kupeleka umeme huko iwe ya manufaa zaidi kwao na kwa Taifa kwa ujumla. Aidha, upanuzi wa laini ya usambazaji katika maeneo ya Nawenge na Vitongoji vyake, utategemea upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, ni kwamba sasa hivi pantoni inafanya kazi hakuna tena sababu ya kuzungumzia suala hilo. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kusisitizia usimamizi ili kuhakikisha kwamba *TANESCO* wanamaliza kazi hii ya kwanza?

Mheshimiwa Spika, la pili, je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kufuatana pamoja na mimi kwenda kuona kazi inayofanyika Reginamundi kule Mahenge eneo la Nawenge?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia kwa juhudi kubwa suala zima la kupeleka umeme katika hii Shule ya Reginamundi. Amekuwa akishirikiana nasi kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimthibitishie Mheshimiwa Kasapira kwamba, kama nilivyosema katika kujibu swali la msingi ni kwamba, *TANESCO* mwaka huu imepanga kuendelea na kazi na tunafahamu kwamba, kivuko sasa hivi kinafanya kazi na tunaamini kwamba, kutokana na mipango iliyopo na kama nilivyosema awali, kama hakutajitokeza jambo lingine lolote la dharura, basi kazi hiyo ya ujenzi wa laini hii utaendelea hatua kwa hatua hadi tuikamilishe.

Kuhusu mwaliko wake, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Kasapira kwamba, nimefurahi kupokea mwaliko huo na mimi nitakuwa tayari kwenda kwenye eneo hilo, kushirikiana naye na viongozi wengine wa eneo hilo katika kuhakikisha kwamba, tunakagua kazi ambayo imefanyika. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa maelezo ya tatizo lililotokea kupeleka umeme Mahenge Reginamundi. Huu ni Mradi ambao ulipangiwa kutekelezwa kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, mwaka 2001/2002, miradi ambayo katika hotuba hiyo iko katika ukurasa wa 27 hadi 22. Kwa vile ametoa sababu kwa Mradi huu uliochelewa, kwa Miradi hii mingine yote iliyoorodheshwa kwenye hotuba hiyo ukurasa wa 17 hadi 23 ataweza kutudokezea sababu ikiwa ni pamoja na Miradi yangu ya Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimeelezea matatizo ya Mradi wa Reginamundi kutokana na ukosefu wa fedha. Sababu hii ya ukosefu wa fedha inajitokeza mara kwa mara pia kwa miradi mingine. Tunaweza tukapanga vizuri, lakini kutokana na mapato hafifu ya Taifa katika mwaka husika, fedha ambazo tumezitegemea pengine zinaweza zisipatikane na hivyo kupelekea baadhi ya miradi ikashindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametaja maeneo mahsusi na kutaja ukurasa mahsusi katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ambayo sinayo sasa hivi hapa, nadhani si rahisi kuweza kupitia kijiji hadi kijiji na kumjibu moja kwa moja hapa. Lakini napenda nimfahamishe kwa ujumla wake kwamba, kwa kuwa swali aliloluliza linahusu takwimu za maeneo husika, basi baada ya Bunge hili nitakuwa tayari kushirikiana naye na kumfahamisha kipengele hadi kipengele, kipi kilipata fedha na kipi hakikupata.

Mheshimiwa Spika, nadhani huo ni utaratibu mahsusi kwamba, swali linalohusu takwimu inabidi liletwe katika utaratibu ambao linaweza kujibika kwa ufasaha.

Na. 86

**Kiwanja cha Michezo cha Kisasa**

**MHE. MOHMED ABDULLY ALLY (k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imeahidi kujenga Kiwanja cha Michezo cha Kisasa kabla ya mwaka 2005 na kupelekea kuundwa Kamati ya kushughulikia suala hilo na kwa kuwa mwaka 2003 unaingia:-

(a) Je, Kamati imefanya utafiti ili kubaini gharama za ujenzi wa kiwanja hicho?

(b) Je, uwanja huo utahimili kuchezewa michezo ya aina ngapi?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hivi sasa bado ni mapema mno kujua gharama za ujenzi wa uwanja huo. Ni mapema mno kujua gharama za ujenzi kwa sababu wanaoomba kuwa wajenzi bado hawajapatikana. Kwa mujibu wa zabuni, si busara kutangaza kiasi cha pesa zitakazotumika katika ujenzi, kwa kuwa gharama ni mojawapo ya kigezo cha kushindanisha wazabuni walioomba. Aidha, zabuni iliandaliwa kwa ajili ya kumtafuta msimamizi na mshauri wa ujenzi. Baada ya kuzingatia taratibu zote za zabuni kama sheria ya manunuzi ya vifaa na bidhaa inavyotaka, msimamizi aliyepatikana ni *BKS Group (pty) Ltd. of South Africa*, ambaye atashirikiana na *Co-Architecture* wa Tanzania. Msimamizi na mshauri aliyeteuliwa alitiliana sahihi na Serikali tarehe 7 Aprili, 2003 na tayari amekwishaanza kazi. Hivi sasa taratibu zinaendelea ili kumpata Mjenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuwa na Uwanja wa Kisasa utakaoweza kukidhi mahitaji ya michezo mingi ikiwemo soka, riadha, kuogelea, mpira wa wavu na mpira wa kikapu. Michezo mingine ni mpira wa mikono, tenisi, kriketi, netiboli na mpira wa magongo.

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa hali ya ujenzi wa viwanja vya michezo ni wa aina yake, hali ya kutumia majani imepitwa na wakati. Je, katika ujenzi huu katani itatumika katika uwanja huo? *(Makofi)*

La pili, hivi sasa kuna vyumba maalum ambavyo waamuzi huwa wanafichwa na hawaonekani na zile timu. Je, katika ujenzi huo mambo hayo yatazingatiwa au itakuwa hali ile ile ya marefa kuwapa chochote? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, majani yatatumika katika sehemu inayostahili majani. Kwa Kiswahili kizuri ni nyasi. Katani itatumika pale ambapo patatumiwa kwa riadha. Kwa uwanja unaojengwa sasa ni uwanja wa kisasa, katani itatumika katika maeneo ya riadha, pale wanapochezea soka zitatumika zile nyasi maalum kama viwanja vya wenzetu mnavyoviona. Ukiangalia kwenye televisheni utaona kama vile wametandika *carpet*, ndio uwanja unaokusudiwa kujengwa Dar es Salaam hivi sasa.

Vyumba maalum vya uamuzi, hayo pia vile vile yamezingatiwa pamoja na usalama wa viongozi watakaokuwa wanakwenda na kuangalia na kupunguza kero ya watazamaji. Kitakuwa ni kiwanja ambacho mtu unakwenda kwa saa unayotaka wewe mwenyewe, sio kwamba kama kuna mechi kubwa kwa mfano, kama Timu ya Yanga inacheza, watu tunakwenda pale saa 7.00 mchana, kiwanja hiki sasa kitaruhusu watu kwenda saa 9.30 mchezo unaanza saa 10.00. Kwa hiyo, yote haya yamezingatiwa. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na mikakati mizuri ya Serikali ya kujenga uwanja wa kisasa wa michezo. Vile vile mikoa ina mikakati ya muda mrefu ya kujenga viwanja vya michezo ukiwemo Mkoa wa Singida. Kwa kuwa juhudi za wananchi wa mikoa mingine zimeshindwa kumaliza kujenga uwanja wa michezo ikiwemo Mkoa wa Singida Uwanja wa Namfua. Je, Serikali ina mikakati gani ya kusaidia mikoa ambayo imejitahidi ya kuwa na nia ya kumaliza uwanja wa michezo ili kuwatia moyo wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni swali jipya lakini kama Waziri unaweza kulijibu endelea.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama wote tunavyofahamu, hali ya uchumi wa nchi haikuwa nzuri. Hivi sasa ndiyo maana mmeona kwamba, vipaumbele vya michezo vimeanza kujitokeza. Hapo hali ya uchumi itakavyozidi kuimarika, ni dhahiri Wizara itaanza kupeleka misaada katika mikoa ili kuimarisha michezo. Lakini kwa hivi sasa tunaendelea kutegemea juhudi za kujituma katika mikoa ili kuboresha mazingira na maeneo ambayo watu wanacheza michezo.

Ombi kubwa ambalo nataka kulitoa kwenye Serikali za Mikoa ni kwamba, uvamizi wa viwanja ambavyo vimetengwa kwa ajili ya michezo ungekomeshwa ili watu waendelee kupata mahali pa kuchezea.

Na. 87

**Sera ya Wazee**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa wastaafu wengi hapa nchini ni wazee na wengi wao wanaishi maisha duni sana na hata hawajui namna ya kuendesha maisha yao hata yale ya kujikimu:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuikamilisha Sera ya Wazee, ili iwe wazi kwa kila mmoja?

(b) Je, taratibu za awali za kusaidia wazee wapate tiba bila kusumbuliwa zimefikia wapi au nayo inasubiri Sera ya Wazee ili itoe mwongozo?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha rasimu ya Sera ya Wazee baada ya kuwashirikisha wadau wote. Sera hiyo imekwishajadiliwa katika ngazi mbalimbali na tayari imepitishwa katika Baraza la Mawaziri mwezi Septemba, 2002. Tunaamini kuwa sera hii ipo wazi kwa kuwa toka maandalizi yake wadau wote walishiriki. Mikakati ya utekelezaji imeandaliwa na kabla ya Julai, 2003, itasambazwa kwa wadau ili kupata maoni yao.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa matibabu ya bure kwa wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea umeanza kutekelezwa. Hata hivyo, utaratibu huu una mapungufu kwa kuwa wazee wengi walio vijijini hawajanufaika kwa sababu inakuwa vigumu kutambua wazee waliofikisha umri wa miaka 60 na pia upatikanaji wa uhakika wa dawa zinazotakiwa wakati wa matibabu. Kwa hiyo, tunatarajia sera ya kuchangia gharama za afya itakapofanyiwa mapitio itarekebisha mapungufu yanayojitokeza hivi sasa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa suala la usumbufu kwa wazee kupata matibabu katika hospitali limekuwa ni kero yao kubwa kwa muda mrefu na kwa kuwa kupata vitambulisho vya umri hasa kwa wazee wa vijijini inakuwa ni vigumu kwa sababu wengine hata wakati walipozaliwa hawajui ni tarehe ngapi. Je, kwa nini Serikali isifute kabisa suala zima la kuchangia gharama za matibabu kama wanavyofanya kwa watoto ambao wako chini ya umri wa miaka mitano?

Pili, kwa kuwa wazee wana matatizo ya magonjwa ambayo ni tofauti na vijana. Kwa nini katika hospitali zetu, zahanati na vituo vya afya, wasiwe na kitengo maalum ambapo Madaktari au Wauguzi wawe ni watu wenye umri mkubwa, si vijana au watoto, ambapo wazee watakuwa huru kuwazungumzia matatizo yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, wazee wanakaa katika maeneo yanayojulikana. Sheria ya kutoa nafuu kwa wazee ili wapate matibabu bure inasema wazi kwamba, kila mzee atapata kitambulisho pale alipo cha kumjulisha kwamba yeye ni mzee na anastahili kupata matibabu bure. Kwa hiyo, kitambulisho hicho ndicho kitakachofanya aende kwenye zahanati iliyo karibu naye au kituo cha afya kilicho karibu naye na vile vile baada ya hapo atakwenda hospitali kama atapelekwa kule na kupata rufani. Kwa hiyo, kwa kweli hatuwezi tukasema kwamba wazee ndiyo sera inavyosema wazee watatibiwa bure. Lakini utaratibu unataka mzee apate kitambulisho kutoka pale anapokaa. Hilo la kwanza.

La pili, ningependa kusema kwamba kwanza tunastaafu tukiwa na miaka 60. Sasa hao wazee wa kwenda mpaka kwenye zahanati atakayekuwa na umri wa zaidi ya miaka 60 haitawezekana kwa mujibu wa sheria, kwa sababu wakati huo atakuwa yeye ameshakufa. Kwa hiyo, kutaendelea kuwa na vijana katika vituo vyetu vya afya na Madaktari na mimi ninafikiri wanafanya kazi nzuri kuwahudumia wagonjwa bila kujali uzee wala nini, wanafanya kazi vizuri sana. Pia nataka nikiri kwamba, kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanawasibu wazee zaidi kuliko vijana. Lakini wale wanaohudumia wote wana utaalam wa kutibu bila kujali kama yule ni mzee ama kijana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa lile swali lake la pili la wazee kuona haya kutibiwa na vijana, mimi ningependa kutoa rai kwamba, sisi Wabunge tujaribu kusaidia kuwaelimisha wazee. Ni kweli mila zetu wakati mwingine zinatuelekeza katika kuona kwamba, tunakwenda kwa marika au tunakwenda kwa jinsia. Mimi nitawapeni mfano ambao umeniathiri mimi mwenyewe, mara ya kwanza nilipofika Sekondari Kidato cha Pili, nikaandikiwa kuchoma sindano. Nilipokwenda chumba cha sindano nikamkuta mchoma sindano ni mwanamke, ndiyo mara ya kwanza kupambana na mwanamke anichome sindano. Nikasema haiwezekani nikatoka, baadaye nikarudi kwenye saa 8.00 nikamkuta bado yupo mwanamke huyo huyo ikabidi basi nivue nguo nichomwe sindano. Lakini baadaye niliona kwamba ni kitu cha kawaida. Kwa hiyo, tukiendelea kuwaelimisha wazee hawa wataona kwamba ni kitu cha kawaida kutibiwa na Madaktari vijana.

Na. 88

**Vyombo vya Kuhifadhia Maji**

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI** aliuliza:-

Kwa kuwa watu wengi waishio kwenye maeneo yenye upungufu wa maji wanajitahidi kununua vyombo vya kuhifadhia maji kwa ajili ya matumizi yao mbalimbali kama kunywa, kuogea, kupikia, kufulia na kadhalika:-

(a) Je, vyombo kama mapipa, *Sim Tank/Poly Tanks* vina usalama kiasi gani kwa kazi na matumizi yaliyotajwa hapo juu?

(b) Je, hakuna vyombo vinavyoweza kutengenezwa hapa nchini vya kukidhi haja iliyotajwa bila kutiliwa mashaka na watumiaji?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mbunge Viti Maalum, lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kusambaza na kuhifadhi maji, aina mbalimbali za mabomba na matanki hutumika. Katika usambazaji wa maji, mabomba aina ya chuma na *plastic* hutumika kama vile *Ductile Iron, Cast Iron, Galvanized Steel, PVC, Polyethylene* na kadhalika. Aidha, matanki yanayotumika kwa kuhifadhia maji ni ya *plastic,* chuma, *ferro cement* na kadhalika. Kwa kawaida mabomba na vifaa vya kuhifadhia maji huchunguzwa ubora na usalama wake ili kulinda afya za watumiaji. Vifaa vya *plastic* vinavyotumika katika kusambaza na kuhifadhi maji vipo katika kiwango cha *Food Grade* hivyo ni salama.

Aidha, mapipa ambayo yametengenezwa maalum kwa ajili ya kuhifadhia maji, hutakiwa kuwa na usalama kwa ajili ya afya ya watumiaji. Napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*, huhakiki ubora wa vifaa hivyo kwa madhumuni ya kuzilinda afya za watumiaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia nafasi hii, napenda kuwatahadharisha wananchi kutotumia mapipa ambayo hayakutengenezwa kwa lengo la kuhifadhi maji kwa matumizi ya majumbani. Mapipa haya ni yale ambayo matumizi yake ya awali ilikuwa ni kuhifadhia madawa ya kilimo *(Agrochemicals)*, dawa za kuulia wadudu *(Pesticides)* na kadhalika, mapipa yanayouzwa barabarani bila kukidhi viwango kinachotakiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hapa nchini kuna viwanda vya kutengeneza vifaa vya kuhifadhia maji, ambavyo vinakidhi haja bila kutiliwa mashaka na watumiaji. Viwanda hivyo ni pamoja na vile vya *Simba Plastic, Polytank, Sumaria Group, Chemi-Cotex* na kadhalika. Aidha, matanki yanaweza kujengwa katika ujazo mbalimbali kwa kutumia saruji, mchanga na kokoto. Endapo tanki linalohitajika ni la ujazo mkubwa kuanzia lita 10,000 na zaidi, nondo hutumika ili liweze kuwa imara.

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa umaskini wa Tanzania ndio unaosababisha kufanya yale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji ameyatahadharisha. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi za vifaa hivi vinavyotoka viwandani ili wananchi waweze kumudu kuvinunua? *(Makofi)*

Pili ni kwamba, je, viwanda hivi vikifanya kazi nzuri na kufikia kiwango cha Kimataifa kinachotakiwa, vimetangaza vipi nchi yetu nje ya nchi na kujipatia fedha za kigeni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, hatujapokea malalamiko Wizara ya Fedha kama kodi ni tatizo linalosababisha watumiaji wa matanki haya kuhitaji kupunguziwa kodi ili waweze kuyamudu. Kama hilo ni tatizo, basi naomba liletwe ili Serikali iweze kuona kama kodi ni kubwa.

Lakini kwa sababu Serikali inahitaji fedha na inahitaji kutoza kodi ili iweze kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, kwa hiyo kodi itaendelea kutozwa katika viwango vya sasa mpaka itakapodhihirika kwamba, mahitaji ni makubwa na watu wanaohitaji kuyatumia hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, pili, matanki yanayozalishwa Tanzania yanasafirishwa nje na yanaingiza fedha za kigeni.

Na. 89

**Kero ya Maji Korogwe**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa kero ya maji katika Mji wa Korogwe imekuwa ni tatizo sugu na Serikali inalifahamu tatizo hilo kwani imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali za kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo na ahadi yake ya mwisho ilikuwa ni ya mwaka 2002/2003 kwamba kati ya miradi miwili yaani ule wa kutoa maji toka Mlima Mashindei au ule wa kutoa maji kutoka kwenye chanzo cha *HTM - Tabora* toka Mto Ruvu, lakini hadi leo hakuna chochote kilichofanyika cha kuupatia Mji huo maji ya uhakika:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizoifanya Serikali ishindwe kutimiza ahadi yake ya muda mrefu iliyoweka kwenye Bajeti iliyopita?

(b) Je, sasa Serikali ina mikakati gani inayotekelezeka ya kuupatia Mji wa Korogwe maji ya uhakika, hasa ikizingatiwa kuwa mji huo umepata hadhi ya mji na maendeleo kukua siku hadi siku?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mji wa Korogwe unapata huduma ya maji kutoka vyanzo vya maji ambavyo ni maji ya mtiririko vya Mbesa, kisima kirefu cha Kilole na kisima kirefu cha *Old Korogwe*. Vyanzo vya Mbesa na Kilole, ni vya zamani sana na kwa ujumla havikidhi mahitaji ya maji kwa Mji wa Korogwe ambao unakua siku hadi siku.

Katika juhudi za kuwapatia wananchi wa Korogwe maji safi na salama, tanki moja la kuhifadhia maji la lita 20,000 limejengwa Kitonga na lingine la lita 30,000 limejengwa *Old Korogwe*. Kisima kingine cha Mtonga kimechimbwa ili kuongeza wingi wa maji katika Mji wa Korogwe. Serikali inatambua kwamba, matumizi ya vyanzo vya *HTM - Tabora* na Mlima Mashindei yatapunguza kwa kiasi kikubwa, kero ya maji kwa wakazi wa Mji wa Korogwe. Kutokana na gharama kubwa za kuendeleza vyanzo hivyo, Serikali imeshindwa kutekeleza jambo hili mapema kama inavyotarajiwa. Hata hivyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha zitakazosaidia kuendeleza vyanzo hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Mbunge kulileta tatizo hili Wizarani, Serikali imechukua hatua za muda mfupi zifuatazo katika kutatua tatizo la maji Mjini Korogwe:-

- Mwezi Oktoba, 2001 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, ilifunga mtambo mpya katika kisima cha Kilole na kwa sasa unafanya kazi vizuri;

- Mwezi Februari, 2002 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, ilichimba kisima kingine kipya *Old Korogwe* na kufunga mtambo mpya na wenyewe unafanya kazi vizuri.

- Mwezi Machi, 2003 Wizara yangu pia kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, ilichimba kisima kingine kipya eneo la Mtonga; na

- Mwezi Mei, 2003 Wizara yangu imetoa fedha kiasi cha Sh.41.5 milioni kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya maji na mabomba ya mtandao. Kisima hiki kinakadiriwa kutoa meta za ujazo 410 kwa siku na kitahudumia Mtaa wa Mtonga, Shule ya Sekondari ya Semkiwa na kuongeza kiasi cha maji katika mtandao wa zamani.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri mpya ya Mji wa Korogwe, pamoja na Mheshimiwa Bendera, itaendelea kutafuta fedha na mbinu za kuwapatia maji Wananchi wa Mji wa Korogwe.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba vyanzo vya maji vilivyopo sasa vya *Old Korogwe* na Kisima cha Kilole havikidhi haja na huwa vinaharibika mara kwa mara na mara nyingi vinaharibika zaidi ya miezi mitatu na kuleta kero Mjini na kwa kuwa Serikali imesema vyanzo vya maji vya *HTM - Tabora* vina uhakika kabisa wa kuleta maji kwa sababu ni kilometa 8 tu kutoka *HTM - Tabora* kwenda Mjini Korogwe na maji yanakwenda kwa *gravity*.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa hivi ni busara Serikali ikatumia haya maji ya *gravity* ambayo ni rahisi kuliko kuchimba visima na kuleta matatizo hasa ya mitambo ili Korogwe iweze kupata maji ya uhakika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA -MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Bendera, kwa juhudi zake kubwa anazofanya katika kuwatafutia maji Wananchi wa Korogwe na Jimbo lake kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, chanzo cha *HTM - Tabora* kutoka Mto Ruvu ndicho kingekuwa na gharama nafuu za uendeshaji kama kingekuwa kimekamilika. Lakini kama nilivyosema, Serikali imechukua hatua za muda mfupi ambazo nimezitaja na imejitahidi sana kwa kushirikiana na Halmashauri, pamoja na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, Wizara pamoja na Serikali itaendelea kushirikana na Halmashauri, pamoja na Mheshimiwa Mbunge, ili kukamilisha Mradi huu ambao tayari upo kwenye mipango ya Wizara na Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha sijapata maombi ya Mwenyekiti wa Kamati yeyote ya kutaka Kamati yake ikutane. Kwa hiyo, sina taarifa ya Vikao vya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kusema kwamba, kwa hoja iliyoko kwenye *Order Paper* ya leo, nimeshapata Waheshimiwa Wabunge 48, ambao wameomba kuchangia, nafikiri kwa muda uliotengwa wanatosha. Nafikiri orodha hii itakuwa kwenye ubao wa matangazo kama kawaida, lakini wale ambao watajikuta hawapo kwenye orodha, nashauri wachangie kwa maandishi

Vile vile, napenda kukumbusha kwamba, kwa Kanuni mpya za Bunge, Bunge linaingia katika Kamati ya Bunge Zima kupitisha vifungu, siyo kama mwaka 2002. Sasa, ni lazima tutenge muda wa Kamati ya Bunge Zima ya kupitia kifungu kimoja kimoja.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2003 *(The Finance Bill, 2003).***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Ofisi ya Waziri Mkuu

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2002/2003 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2003/2004. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, wamepata fursa ya kusikia maelezo kuhusu Hali ya Uchumi Nchini na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004. Napenda niwapongeze kwa dhati Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao zilizotoa maelezo hayo kwa ufasaha. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri katika hotuba hizo na hatimaye kukubali kupitisha Bajeti ya Serikali. Serikali itazingatia ushauri wao katika utekelezaji wa Bajeti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu, kwa uchambuzi wa Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Serikali wa mwaka 2003/2004 na ushauri wake kwa Serikali. Aidha, ninawashukuru wadau wote, ambao wametoa michango yao ya mawazo katika hatua mbalimbali za utayarishaji wa Bajeti na Mpango huo. Nazishukuru Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu, kwa kupitia makadirio ya matumizi ya kila Wizara, Ofisi na Idara za Serikali zinazojitegemea na kushauri ipasavyo. Napenda niishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kupitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge. Tumepokea ushauri wao na tutauzingatia wakati wa kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, chaguzi ndogo katika Majimbo ya Uchaguzi yaliyokuwa wazi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zilifanyika tarehe 18 Mei, 2003. Jumla ya Vyama saba vilishiriki katika chaguzi hizo. Vyama hivyo ni CCM, *CUF*, CHADEMA, *TLP, NCCR - Mageuzi, TADEA* na *UMD*. Chaguzi hizo ziliendeshwa kwa amani, uhuru na haki. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuruu kwa dhati Wananchi wote walioshiriki katika chaguzi hizo kwa kutuonyesha kwa mara nyingine jinsi Watanzania tulivyokomaa kisiasa na wenye kuthamini amani na utulivu. Nawashukuru Viongozi wn Watendaji wa Tume zetu mbili za Uchaguzi, yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kwa kazi yao nzuri.

Navishukuru Vyama vyote vya Siasa vilivyoshiriki katika chaguzi hizo kwa kuonyesha ukomavu mkubwa wa kisiasa na kwa kuendesha kampeni kwa uadilifu mkubwa. Kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa ambao ni Wabunge wanaowakilisha Majimbo manne ya Tanzania Bara waliotokana na Chama cha Mapinduzi na Wabunge wanaowakilisha Majimbo kumi na tano ya Tanzania Zanzibar wanaotokana na Chama cha *CUF*. Ninapenda kuwakaribisha nyote katika Bunge letu Tukufu. Aidha, nawapongeza wote waliochaguliwa kujaza nafasi zilizokuwa wazi za Udiwani, Uenyekiti wa Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji, Uenyekiti wa Vitongoji na zile za Ujumbe katika Serikali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya chaguzi hizo ndogo yameijengea nchi yetu heshima kubwa ndani na nje ya nchi yetu. Wapo baadhi ya watu waliotabiri kuwa vurugu zingelitokea na wapo waliokuwa wanaeneza *propaganda* za uongo zilizokuwa na lengo la kuwatisha wananchi na kuwatia woga wa kutoshiriki kwenye chaguzi hizo. Hata hivyo, kitendo cha wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika chaguzi hizo, kimedhihirisha kuwa wanaelewa mustakabali wa nchi yetu upo mikononi mwetu. Kazi kubwa tuliyonayo Viongozi wa Kisiasa hivi sasa ni kuendelea kuwaelimisha wananchi watambue umuhimu wa uchaguzi kama nguzo kuu ya demokrasia na wawe tayari kushirki kikamilifu katika kuwachagua Viongozi wanaowataka kwa hiari yao wenyewe. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa uimarishaji wa demokrasia nchini, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanzisha Daftari la Wapiga Kura. Maandalizi yameanza kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ili kuangalia namna rahisi ya kuanzisha Daftari hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuendeleza na kuimarisha Muungano, Serikali zetu mbili zimeendelea kuimarisha mazingira ya mashirikiano na kuondoa kero mbalimbali. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuratibu uboreshaji wa mashirikiano baina ya Wizara na Asasi za Serikali zote mbili katika mambo ya Muungano na kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu za matukio na maamuzi mbalimbali. Tumefikia pia makubaliano kuhusu gawio litokanalo na faida ya Benki Kuu ya Tanzania na misaada kutoka kwa wahisani kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Tume ya pamoja ya Fedha ya Muungano, imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 134 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mambo yasiyo ya Muungano, Serikali zote mbili zimejiwekea utaratibu wa kuwa na mikutano ya mashirikiano ambapo maamuzi mbalimbali kuhusu sera, sheria, kubadilishana wataalam, utafiti na upanuzi wa maeneo ya mashirikiano yameshughulikiwa. Aidha, ufumbuzi wa matatizo mbalimbali umefanyika kwa maelewano makubwa. Serikali zetu mbili zitaendelea kuondoa vikwazo katika masuala ya Muungano na kudumisha mashirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2002/2003, Bunge lako Tukufu lilifanya mabadiliko ya Kanuni za Bunge ambapo Kamati za Bunge ziliundwa upya. Muundo na majukumu ya

Kamati hizo unawawezesha Waheshimiwa Wabunge, kuchambua masuala mbalimbali na kusimamia shughuli za utendaji wa Serikali katika Wizara walizopangiwa kwa umakini zaidi. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu, kwa kuchaguliwa kushika madaraka ya Uongozi wa Kamati hizo ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Bunge lako Tukufu lilipitisha Miswada ya Sheria 21, liliridhia Maazimio ya Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa 19 na maswali ya msingi 609 ya Waheshimiwa Wabunge yalijibiwa na Serikali. Maagizo na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati za Bunge yamefanyiwa kazi na baadhi ya maeneo, yakiwemo ya utekelezaji wa ahadi za Serikali, yanaendelea kushughulikiwa. Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni ya mwaka 2002/2003, itatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili wa Bunge. Katika mwaka 2003/2004, ujenzi wa ukumbi mpya wa kisasa kwa ajili ya mikutano ya Bunge, Mjini Dodoma na ujenzi wa Ofisi ya Bunge, Zanzibar utaanza. Aidha, uimarishaji na ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yao utaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi sasa idadi ya Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu nchini imefikia kumi na sita baada ya Chama cha *Progressive Party of Tanzania (PPT - Maendeleo)*, kupata usajili wa kudumu tarehe 4 Machi, 2003. Aidha, kipo Chama kimoja tu cha Amani Demokrasia Tanzania (CHADETA), kilichopata usajili wa muda tarehe 18 Februari, 2003. Kutokana na mazingira ya kisiasa tuliyonayo hivi sasa na uzoefu tulioupata tangu turejeshe Mfumo wa Siasa za Vyama Vingi, upo umuhimu wa kuipitia Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992, ili iweze kukidhi mahitaji ya wakati tulionao. Kwa msingi huo, Serikali inaandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo na yatawasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, hali ya usalama katika maeneo ya Maziwa Makuu haikuwa ya kuridhisha. Hata hivyo, yapo matumaini ya amani katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kutokana na kuanza kutekelezwa kwa makubaliano baina ya makundi yanayohusika kwenye migogoro hiyo. Hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya Tanzania na nchi jirani kwa ujumla ni shwari isipokuwa mpaka kati ya Tanzania na Burundi, pamoja na ule wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kama nilivyoeleza. Katika mipaka hiyo bado lipo tatizo la waasi na wakimbizi wanaoingia nchini bila utaratibu na wakati mwingine huingia na silaha. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2003, nchi yetu ilikuwa na wakimbizi wasiopungua 700,000 wanaoishi makambini. Juhudi za kuwarejesha wakimbizi kwao zinaendelea kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi na nchi wanakotoka. Hadi mwezi Aprili, 2003, wakimbizi wa Rwanda wasiopungua 28,000 na wengine wapatao 42,000 wa Burundi walirejeshwa kwao. Hata hivyo, baada ya makabidhiano ya Serikali mpya ya Burundi, matumaini yameanza kuonekana kwani wakimbizi wengi wameanza kuondoka wenyewe bila kutegemea Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi. Serikali kwa kushirikiana na Mataifa mengine itaendeleza juhudi za kutafuta suluhu ya matatizo ya kisiasa ya nchi jirani. Juhudi hizo zitasaidia kupunguza mzigo kwa Watanzania na kuleta maendeleo ambayo kwa muda mrefu yamerudishwa nyuma kutokana na athari za wakimbizi na usalama usioridhisha katika maeneo ya mipakani na hata ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunakabiliana na ongezeko la uhalifu katika baadhi ya maeneo nchini. Hali hiyo inachangiwa na ongezeko la wakimbizi, urahisi wa upatikanaji wa silaha kutoka nchi jirani zenye migogoro na ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Serikali iliendesha operesheni mbalimbali za kudhibiti ongezeko la ujambazi, silaha na kilimo cha bangi katika baadhi ya Mikoa nchini. Operesheni zote zilifanyika kwa kushirikisha Vyombo mbalimbali vya Ulinzi na Usalama, pamoja na raia wema na zimesaidia kupunguza matukio ya uhalifu katika maeneo husika. Ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kukabiliana na matukio ya uhalifu, Serikali iliongeza Bajeti ya Jeshi hilo, ilitoa mafunzo kwa Askari na elimu kwa umma. Aidha, hatua zimechukuliwa kuimrisha ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na Serikali za Mitaa ili kubadilishana taarifa na mikakati ya kukabiliana na uhalifu. Ninapenda kuwahakikishia wananchi kuwa, Serikali itaendelea kupambana na wahalifu bila huruma yoyote. Tunachoomba ni ushirikiano wa wananchi wote ili mafanikio yawe makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, matukio ya matumizi ya dawa za kulevya yanaongezeka nchini. Katika mwaka 2002 kulikuwa na matukio 5,441 ya kukamatwa kwa watu waliojihusiaha na dawa za kulevya ikilinganishwa na matukio 4,751 yaliyotokea mwaka 2001. Hili ni ongezeko la asilimia 14.5 ambalo linadhihirisha kuwa tatizo la dawa za kulevya bado ni kubwa nchini. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya imeimarishwa kwa kupewa majengo ya ofisi na vitendea kazi. Kwa kusaidiana na Jeshi la Polisi, Tume imeweza kuwakamata wafanyabiashara wa dawa za kulevya na kupambana na ulimaji na usambazaji wa mimea haramu hasa ya bangi. Aidha, Tume imetoa elimu kuhusu athari za dawa za kulevya kwa jamii. Katika mwaka 2003/2004, kazi hizo zitaendelezwa ili ushiriki wa wananchi kwenye vita hivyo uweze kuwa mkubwa zaidi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itawasaidia waathirika wa dawa hizo ili wakishatibiwa na kujirekebisha wawe raia wema.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa vitendo vya uhalifu nchini kutapunguza idadi ya mahabusu na wafungwa magerezani na hivyo kuondoa kero ya msongamano kwenye magereza. Takwimu zinaonyesha kwamba, idadi ya wafungwa na mahabusu kwa sasa inazidi uwezo wa magereza yaliyopo. Kwa mfano, hadi tarehe 31 Mei, 2003, kulikuwa na wahalifu 44,667 katika magereza yote nchini ambapo uwezo uliopo ni wa kuhifadhi wahalifu 22,699 tu. Kati ya wahalifu hao, 25,221 ni wafungwa na 19,446 ni mahabusu. Tatizo la mahabusu wengi magerezani ni kubwa na wakati mwingine limesababisha maafa kama yaliyotokea tarehe 18 Novemba, 2002 huko Mbarali, ambapo mahabusu 17 walipoteza maisha kwa ajili ya kusongamana. Kuwepo kwa mahabusu wengi pia ni gharama kubwa kwa Serikali kwa sababu ni watu wanaokula na kutibiwa bila ya kufanya kazi. Serikali inachukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo. Baadhi ya hatua hizo ni marekebisho ya Sheria za Bodi za *Parole* ya mwaka 1994, ambayo imepanua wigo ili wafungwa wengi zaidi wanufaike na utaratibu wa misamaha ya *Parole*. Aidha, baada ya kuanzishwa kwa Sheria ya Kuhudumia Jamii ya mwaka 2002, taratibu za kuanza kutumika kwa Sheria hiyo zimeanza ambapo wahalifu wenye makosa madogo madogo watapatiwa vifungo vya nje.

Mheshimiwa Spika, kurejeshwa upya kwa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, kumetupa fursa nyingine ya kuwaandaa vijana kuwa raia wema, wenye uzalendo wa kusimamia umoja, utaifa, usalama na ulinzi wa Taifa. Vijana na awamu ya kwanza waliotumikia JKT wanatarajiwa kukamilisha mkabata wa miaka miwili mwezi Oktoba, 2003. Hivi sasa tayari wapo vijana walioandikishwa kutumikia awamu ya pili na wanatarajiwa kuhitimu mafunzo yao mwezi Februari, 2005. Makambi ya JKT yanayotumika yameongezeka toka mawili hadi manne, ambayo ni Mafinga, Makutupora, Oljoro na Ruvu na vijana waliopo katika makambi hayo ni zaidi ya 5,000. Vijana hao, zaidi ya kupata mafunzo ya awali ya ulinzi na usalama, wamekuwa wakipewa mafunzo katika stadi mbalimbali zikiwemo za kilimo, ufugaji na ufundi wa aina mbalimbali, kwa lengo la kuwafanya wawe na uwezo wa kujitegemea zaidi baadaye. Tunatarajia kuwa vijana hawa watakapomaliza mafunzo yao, watakuwa chachu kwa vijana wenzao katika kushiriki shughuli mbalimbali za uzalishaji mali Vijijini na Mijini na ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuimarisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama, jukumu la ulinzi na usalama wa nchi yetu ni la kila Mtanzania na kila Mzalendo. Kuwepo kwa Jeshi la Mgambo kunatokana na msisitizo uliowekwa na Waasisi wa Taifa letu, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere na Marehemu Abeid Amani Karume. Kwa kutambua umuhimu wa Jeshi hilo, Serikali inatayarisha Sera ya Ulinzi ambayo itajumuisha shughuli za mgambo. Sera hiyo itasaidia kuimarisha nguvu ya ulinzi na kuweka sawa usimamizi wa mgambo kiutawala wakati wa amani na wakati usio wa amani. Natoa wito kwa Watanzania wote, kuthamini na kushiriki kikamilifu katika mafunzo na ulinzi wa mgambo ili sote tuwe walinzi imara wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.6 mwaka 2001. Ongezeko hilo ni matokeo ya Utekelezaji wa Sera nzuri za Kiuchumi na mikakati mbalimbali ambayo imekuwa na malengo ya kuongeza uzalishaji mali na uboreshaji wa huduma za kiuchumi. Aidha, Serikali imeboresha huduma za jamii, imeongeza mapato na kudhibiti matumizi yake, imevutia wawekezaji, imeendeleza ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya nchi. Sambamba na mafanikio yaliyopatikana katika ukuaji wa uchumi, kasi ya mfumko wa bei imeendelea kushuka kutoka asilimia 4.5 mwezi Juni, 2002 hadi kufikia asilimia 4.3 mwezi Mei, 2003. Mwenendo huo unatokana na hali nzuri ya upatikanaji na ugavi wa chakula, pamoja na Sera za makusudi za kudhibiti mwenendo wa mapato na

matumizi ya Serikali na ujazi wa fedha nchini. Tunahitaji kujenga uchumi wenye misingi imara na endelevu utakaokabiliana na changamoto za maendeleo na kwenda sambamba na mabadiliko ya masoko na teknolojia katika ulimwengu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika yanaonyesha kuwa idadi kubwa ya wananchi maskini wanaishi Vijijini. Kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 6.2 bado hakitaweza kufanya uchumi wetu utengemae. Changamoto iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa, ukuaji wa uchumi ni endelevu na wa viwango vikubwa vya kati ya asilimia 8 hadi 10. Viwango hivyo ndivyo vitakavyoboresha na kuendeleza huduma za jamii na kiuchumi na hatimaye kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa hususan kwa wananchi wanaoishi Vijijini. Hivyo, sote tuongeze matumizi bora ya raslimali zilizopo na jitihada za pekee zielekezwe kuongeza tija katika kilimo na uzalishaji viwandani. Serikali itaendelea kubuni sera na mipango yenye lengo la kuondoa umaskini na juhudi zitaelekezwa katika kujenga na kuendeleza shughuli ndogo ndogo za uzalishaji na biashara zinazojumuisha usindikaji wa bidhaa asilia, viwanda vidogo na utoaji wa huduma mbalimbali. Katika kufanikisha azma hiyo, juhudi zitaelekezwa katika utoaji wa mikopo midogo, kujenga na kuendeleza ujasirimali kwa mtu mmoja mmoja au vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali na utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhimiza Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali na biashara ili kukuza uchumi wetu. Mfumo wa uendeshaji wa Kituo cha Uwekezaji cha Taifa umerekebishwa kukidhi haja hiyo na kuwa Kituo cha kisasa cha Uwezeshaji wa Uwekezaji Raslimali na Biashara. Tangu kituo hicho kianzishwe mwaka 1990 hadi Mei, 2003, kimepitisha miradi 2,288 yenye thamani ya Shilingi 8.2 trilioni. Kati ya miradi hiyo, miradi 1,017 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani, ambayo ni sawa na asilimia 44.5, miradi 538 sawa na asilimia 23.5 inamilikiwa na wawekezaji wa nje na miradi 733 sawa na asilimia 32 inamilikiwa kwa ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Miradi hiyo imetoa nafasi za ajira kwa watu wapatao 463,703.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza ushiriki wa Sekta Binafsi, Serikali imeendelea kuratibu na kuwezesha shughuli zote za uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara. Baraza hilo ni kiungo muhimu katika kukuza mashirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kuhusu masuala ya Sera na Sheria za Uwekezaji yatakayojenga uchumi imara na kuleta maendeleo endelevu. Katika jitihada za kuvutia wawekezaji, Serikali itaendelea kutekeleza programu maalum ya kuweka mazingira bora ya uendeshaji biashara nchini, itakayohuisha na kubainisha Sheria za Uwekezaji zilizopitwa na wakati ili kuondoa kasoro zilizopo. Aidha, Serikali inatayarisha mkakati wa kuendeleza Sekta Binafsi ambao ndiyo utakuwa dira ya uwekezaji na biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya ubinafsishaji na urekebishaji wa Mashirika yetu ya Umma ni kuongeza ufanisi na uzalishaji, kupata teknolojia mpya na mitaji toka nje na kupanua masoko ya bidhaa zetu. Lengo la Serikali ni kuiachia sekta binafsi iendeshe uchumi ili Serikali ielekeze nguvu zake katika shughuli za huduma ya jamii, miundombinu, utawala na ulinzi na usalama. Tangu zoezi la ubinafsishaji lianze, jumla ya Mashirika 266, sawa na asilimia 85 ya Mashirika yote yanayotakiwa kubinafsishwa, yamebinafsishwa. Kati ya hayo, Mashirika 134 sawa na asilimia 50.4 yamenunuliwa na Watanzania kwa asilimia 100, Mashirika 116 sawa na asilimia 43.6 yamebinafsishwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali, wawekezaji wa ndani na wa nje na Mashirika 16 sawa na asilimia 6.0 yemepata wawekezaji wa nje kwa asilimia 100. Mengi ya Mashirika hayo yanafanya kazi kwa ufanisi katika uzalishaji bidhaa na utoaji huduma.

Kwa ujumla kumekuwa na ongezeko la uzalishaji mali, tija, ajira na mapato ya kodi kwa Serikali. Serikali itaongeza kasi ya ubinafsishaji na urekebishaji wa Mashirika ya Umma yaliyosalia, ili zoezi hilo likamilike mapema na tupate mchango wake katika maendeleo ya uchumi wetu. Aidha, Serikali itaanzisha vyombo vinne vya udhibiti ambavyo vitafuatilia utendaji wa makampuni na mashirika yanayotoa huduma muhimu kwa wananchi. Vyombo hivyo ni Mamlaka za Kudhibiti Nishati na Maji, Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Mawasiliano na Utangazaji na Usafiri wa Anga. Mamlaka hizo zina jukumu la kulinda maslahi ya watoaji na watumiaji wa huduma hizo kwa kuhakikisha kuwa makampuni na mashirika yanatoa huduma bora na kwa bei halali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Serikali iliongeza Bajeti ya Sekta ya Kilimo kwa asilimia 32, ili kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kukuza kilimo cha kujikimu na kukifanya cha biashara, kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chackula katika ngazi zote na kuinua hali ya chakula katika ngazi zote na kuinua hali ya maisha ya wananchi, hususan waishio vijijini. Ili kuongeza uzalishaji, mafunzo kuhusu mbinu shirikishi jamii yaliendeshwa kwa wataalam wa ugani wa Wilaya, Kata na Vijiji na hatimaye kwa wakulima. Maandalizi ya awamu ya kwanza ya Mpango Kamambe wa Kitaifa wa Umwagiliaji Maji Mashambani yalikamilishwa. Aidha, Serikali imeanza kukarabati skimu kumi na mbili za umwagiliaji maji mashambani zenye jumla ya hekta 3,515 katika Wilaya mbalimbali. Vile vile, Serikali imeanzisha vyama vya umwagiliaji maji mashambani katika skimu sita za Bagamoyo na Ruvu (Pwani), Lumuma (Kilosa), Balili (Bunda), Buswahili (Musoma) na Uchuma (Tarime).

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza kilimo cha wanyamakazi, vituo 20 katika Mikoa mbalimbali vilikarabatiwa na mafunzo kwa maafisa ugani 520 na wakulima 6,331 yalitolewa. Ili kuhakikisha pembejeo zinapatikana, Mfuko wa Pembejeo uliingia Mkataba na Benki ya *Exim* na Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro, ili ziweze kutoa mikopo kwa waagizaji, mawakala na wasambazaji. Hadi Aprili, 2003, mikopo ya shilingi 1.8 bilioni ilikuwa imetolewa. Serikali pia ilidhibiti visumbufu vya mazao na kupambana na milipuko ya visumbufu hivyo katika mikoa 19 mara tu ilipojitokeza.

Mheshimiwa Spika, motisha kubwa kwa wakulima na wafugaji ni kuhakikishiwa soko la mazao yao. Pamoja na nchi yetu kuwa moja ya nchi izlizopewa fursa ya kuuza bidhaa zake katika Soko la Marekani, bila kutozwa ushuru wala kuwekewa viwango, bado Watanzania wengi wanadhani soko hilo ni la nguo pekee. Kuna bidhaa zaidi ya 1,800 chini ya mpango huo wa soko hilo, ambazo zinajumuisha mazao ya kilimo na bidhaa nyingine. Tunaweza kufaidika chini ya mpango huo kwa kuuza mboga, matunda na vifaa vya sanaa. Soko lingine kubwa ni lile la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, ambalo sasa ni Eneo Huru la Biashara. Soko hilo lina wakazi zaidi ya 200 milioni na ni jukumu la Chama cha Wakulima na Wafugaji, Shirikisho la Wenye Viwanda na Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo kwa pamoja kujiandaa kutumia fursa inayotolewa na Mkataba wa Jumuiya hiyo kikamilifu kwa kutafuta masoko ya bidhaa zao katika nchi wanachama. Katika eneo la Afrika Mashariki, jitihada zinaendelea za kukamilisha itifaki ya mkataba wa kuanzisha Umoja wa Ushuru wa Forodha baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Changamoto kwa wananchi wote kwa jumla ni kujiandaa kutafuta soko la bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vyetu, bidhaa za kilimo, ufugaji na uvuvi katika nchi jirani za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, bei za mazao yetu ya kilimo kwenye Soko la Dunia bado ziko chini. Sababu mojawapo ni kwamba, ubora wa mazao yetu haujafikia viwango vinavyokubalika Kimataifa. Viongozi na watalaam wanalo jukumu la kuwaelimisha na kuwahimiza wakulima kuzingatia taratibu za kilimo bora na utunzaji wa mazao ili kuongeza ubora na thamani ya mazao yetu. Wanunuzi nao ni lazima wazingatie ubora wa mazao wanayoyanunua na wawalipe wakulima bei nzuri kwa mazao yenye ubora wa juu ili kuwatia moyo wa kuzalisha na kupanga mazao kwenye madaraja ya ubora. Serikali itaendelea kuhimiza na kuwahamasisha wakulima kuanzisha na kupanua kilimo cha mazao yasiyokuwa ya asili, ambayo yana bei nzuri ndani na nje ya nchi yetu. Mazao hayo ni pamoja na viungo mbalimbali kama vile, *vanilla,* mbogamboga, mlonge, karanga mti, michikichi na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Ushirika, Serikali imechukua hatua za kutoa mafunzo ya elimu shirikishi kupitia Chuo cha Ushirika Moshi kwa watalaam mbalimbali wa ushirika nchini. Vile vile wataalam hao wamepatiwa nyenzo na mafunzo ya uhasibu na ukaguzi ili waweze kuwasaidia wanaushirika kusimamia shughuli za ushirika kikamilifu. Aidha, hatua zimechukuliwa kuwahamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika hususan Ushirika wa Akiba na Mikopo ambao ndiyo uliopo karibu zaidi nao. Ili kuwawezesha wanaushirika na wadau mbalimbali kuelewa mwelekeo wa ushirika nchini, Serikali imeanza kusambaza Sera ya Ushirika katika maeneo mbalimbali nchini. Pamoja na hatua hizo, Serikali pia imekamilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ushirika ili yaweze kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu katika mwaka 2003/2004. Aidha, hatua zinaendelea kuchukuliwa katika kuunda ushirika imara kwa kuwahamasisha wananchi ili waweze kuunda na kuanzisha Vyama vya Ushirika vyenye kumilikiwa na wanachama wenyewe. Vile vile elimu ya ushirika itaendelea kutolewa kwa wanaushirika.

Mheshimiwa Spika, mifugo ni sekta muhimu ya uzalishaji na ina uwezo mkubwa wa kuchangia Pato la Taifa. Ili sekta hiyo iwe endelevu, Halmashauri za Wilaya zinapaswa kuhusisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma mbalimbali kama vile usambazaji wa dawa na matibabu. Aidha, tuhimize usafirishaji wa mifugo kwa usafiri wa reli, magari na vyombo vya majini. Vile vile hatuna budi kutoa taarifa za magonjwa ya mifugo mara yanapogundulika. Majosho yaliyopo yatumiwe kikamilifu na kujenga mapya pale ambapo hayapo. Wafugaji wahimizwe kukaa kwa utaratibu wa kudumu na kuhakikisha kuwa idadi ya mifugo yao inaendana na uwezo wa malisho uliopo. Ni vyema mifugo izalishwe kibiashara na kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda imeendelea kukua na katika mwaka 2002 imechangia Pato la Taifa kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 8.3 mwaka 2001. Mafanikio hayo yanatokana na kuanzishwa kwa miradi mipya ya viwanda, mazingira mazuri ya uwekezaji na upatikanaji wa huduma muhimu kama umeme na maji. Kuimarika kwa sekta ya viwanda kutachangia katika ongezeko la ajira, upatikanaji wa bidhaa muhimu, mauzo nje ya nchi, mapato ya Serikali kuongezeka na ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa jumla. Vile vile sekta ya viwanda vya kati na vidogo imeonesha dalili za ukuaji mzuri hasa katika eneo la usindikaji linalofanywa zaidi na wanawake. Napenda kuwapongeza washiriki wote, hususan wanawake, kwa mafanikio hayo. Aidha, nalipongeza Shirika la Kuhudumia Viwanda la Umoja wa Mataifa kwa misaada yake mbalimbali kwa sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uanzishaji na Uendelezaji Viwanda Mahsusi kwa ajili ya mauzo nje ya nchi ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2002. Serikali inaendelea kuainisha maeneo yanayofaa kwa ajili ya matumizi ya *EPZ* na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda chini ya mfumo wa *EPZ*. Kiwanda cha Nguo cha *NIDA Textiles Ltd*. kimepata usajili chini ya Sheria ya *EPZ* kwa ajili ya Soko la Marekani chini ya mpango wa *AGOA*. Aidha, Kiwanda cha Urafiki kitapewa hadhi hiyo mara taratibu zitakapokamilika. Serikali pia imeandaa kanuni za *EPZ* na zitaanza kutumika kwa mujibu wa sheria. Ili kuwezesha utaratibu huo wa kuanzisha maeneo ya uzalishaji kuwepo mikoani, Serikali imeagiza Mikoa ya Tanga, Mtwara, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Kagera na Kigoma, kuyafanyia tathmini maeneo yanayofaa ili yatengwe maalum kwa ajili ya matumizi ya *EPZ*. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itakamilisha hatua za kisheria za kumilikisha Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)*, maeneo ambayo yatatengewa miundombinu na viwanda kwa ajili ya *EPZ. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ya sekta ya biashara kama yalivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, ni kuongeza mapato yatokanayo na biashara ili kuinua kiwango cha ukuaji wa uchumi. Kwa maana hiyo ni lazima tuwahimize na kuwahamasisha wananchi kupenda na kuthamini bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu na kutumia soko la ndani kama msingi wa kuelekea soko la nje. Tuendeleze kampeni ya “Nunua Bidhaa za Tanzania Ujenge Tanzania”. Aidha, Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972, itapitiwa upya na mapendekezo kuwasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu. Mapendekezo hayo yana lengo la kuondoa kero kwa wafanyabiashara na mianya ya rushwa na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii imeendelea kukua licha ya athari za wimbi la ugaidi linaloikabili dunia. Mapato yatokanayo na utalii yamekuwa yakiongezeka na idadi ya watalii pia kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2002/2003, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya, iliandaa mpango kamambe wa utalii, wenye malengo ya kutambua soko la utalii la ndani na nje, kubaini maeneo mapya ya utalii na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika biashara ya utalii. Ili kukuza utalii, Serikali imeanza utaratibu wa kuanzisha mbuga mpya za Kitulo Wilayani Makete na Saadani Wilayani Bagamoyo. *(Makofi)*

Changamoto kubwa inayotukabili ni kubaini vivutio zaidi vya utalii na kutambua maeneo mengine mapya. Katika mwaka 2003/2004, Serikali kwa kushirikiana na mikoa itaendelea kubaini maeneo ya utalii wa mazingira katika Bonde la Mto Rufiji na maeneo ya kusini mwa nchi. Aidha, itaendeleza utafiti, uhifadhi, utangazaji na uuzaji wa raslimali za mambo ya kale. Uongozi wa Mikoa na Wilaya uchukue jukumu la kuanzisha majengo ya makumbusho katika ngazi za vijiji, Wilaya na hata Mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misitu ni mhimili wa maisha ya viumbe vyote na inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Licha ya kupata mazao mbalimbali yatokanayo na misitu, tunaitegemea

sana kwa ajili ya maji na mvua. Hata hivyo, pamoja na umihumu huo, kasi ya uharibifu wa raslimali za misitu na mazingira imeendelea kuwa kubwa. Inakadiriwa kuwa Tanzania inapoteza wastani wa hekta 91,200 za misitu kila mwaka. Kwa kuwa uwezo wa Serikali pekee kusimamia maeneo ya misitu yote ni mdogo, nawasihi wananchi wanaoishi kuzunguka misitu washiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa kuna matumizi bora na endelevu ya raslimali hiyo. Mifano ya mafanikio yaliyoonekana chini ya utaratibu huo ni Mradi wa Hifadhi Ardhi Shinyanga (HASHI) na ule wa Jumuiya ya *SULEDO* Wilayani Kiteto. Miradi hiyo ilitunukiwa tuzo ya *Equator Initiative* na Jumuiya ya Kimataifa kwa kutambua juhudi za wananchi wa maeneo hayo katika kuhifadhi misitu na mazingira yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa ulifikia asilimia 2.7 mwaka 2002 ikilinganishwa na asilimia 2.5 mwaka 2001. Wakati huo huo ukuaji wa sekta hiyo ulifikia asilimia 15 mwaka 2002 ikilinganishwa na asilimia 13.5 mwaka 2001. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu na vito vya thamani. Kwa mfano, uzalishaji wa dhahabu umeongezeka kutoka kilo 30,088 mwaka 2001 hadi kilo 34,065 mwaka 2002. Aidha, katika kipindi hicho thamani ya dhahabu iliyouzwa nchi za nje iliongezeka kwa asilimia 50.8. Hii inatokana na kujengwa kwa mgodi mkubwa wa nne wa dhahabu nchini wa Afrika Mashariki, Wilayani Tarime. Mgodi huo umejengwa kwa Dola za Marekani 90 milioni na una uwezo wa kuzalisha tani 6.2 za dhahabu kwa mwaka. Hata hivyo, madini yanayozalishwa nchini yamekuwa yakiuzwa nje ya nchi bila ya kusanifiwa. Hali hiyo inakosesha nchi mapato na nafasi za ajira kwa wananchi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji kuanzisha vituo vya kuongeza thamani ya madini nchini, lengo likiwa hatimaye kupiga marufuku uuzaji wa madini hayo bila kusanifiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ni muhimu katika mkakati wetu wa kuondoa umaskini. Tunapokuwa na barabara nzuri, wananchi wanaweza kusafirisha mazao ya kilimo na ufugaji kwa urahisi kutoka sehemu ya uzalishaji kwenda kwenye masoko. Barabara pia zinatuwezesha kusafirisha bidhaa kutoka viwandani kwenda kwa wananchi vijijini na zinawezesha upanuzi wa haraka wa sekta zinazokua kama vile madini, utalii na biashara nyingine muhimu katika kanda yetu ya Afrika. Pamoja na umuhimu huo, Tanzania ina barabara zenye urefu wa kilometa 85,000 na kati ya hizo ni chache zenye lami hasa katika ngazi za Wilaya. Kwa ujumla asilimia 65 ya barabara zetu haziko katika hali nzuri. Hiyo ina maana kwamba, bado tuna jukumu kubwa la kujenga, kukarabati na kutunza barabara zetu. Jukumu hilo ni letu na hatuwezi kuwategemea wafadhili pekee na ndiyo maana kuanzia mwaka 2002/2003, tulianzisha Mradi Maalum wa Ujenzi wa Barabara Kuu kwa kutumia fedha zetu wenyewe. Jitihada hizo za Serikali zitasaidia kuongeza mtandao wa barabara za lami nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi wa barabara kuu na zile za mikoa. Mtandao wa barabara za mikoa umeboreshwa kwa kutumia wakala wa barabara. Matengenezo hayo yamewezesha barabara za mikoa kwa sehemu kubwa kupitika majira yote ya mwaka na hivyo huduma muhimu kuwafikia wananchi wanaoishi vijijini. Aidha, Bodi ya Mfuko wa Barabara imeendelea kutembelea asasi za barabara na kuhakikisha kwamba, fedha zinatumika kwa kazi zilizokusudiwa na thamani ya kazi inalingana na fedha zilizotumika. Katika jitihada za kuongeza mapato kwa ajili ya matengenezo ya barabara, Serikali inafanyia kazi mapendekezo ya marekebisho ya viwango na upanuzi wa wigo wa vyanzo vya mapato ya mfuko. Katika mwaka 2003/2003, Bodi itaendelea kuimarisha mfuko na kuwashirikisha wadau mbalimbali kutoa taarifa kuhusu sehemu zinazohitaji matengenezo ya dharura. Aidha, Serikali itatekeleza miradi mbalimbali ya upembuzi yakinifu, usanifu, ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja. Barabara Kuu nchini hasa barabara za Dar es Salaam, Kibiti, Lindi Mingoyo, Dar es Salaam, Dodoma, Singida Mwanza, zitaendelea kupewa kipaumbele kwa kutumia fedha zetu na kwa kushirikiana na wafadhili. Sambamba na hili barabara zingine nazo zitaendelea kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika tuna kazi kubwa ya ujenzi na utunzaji wa barabara za vijijini ambazo ziko katika hali mbaya. Barabara zetu za vijijini zikiwa nzuri zitarahisisha mazao mengi ya wakulima kupelekwa mijini au nje ya nchi na wao kupata fedha na ari ya kulima, kufuga na kuvua zaidi. Hivyo, ni kujumu letu sote kujenga na kutunza vizuri barabara hizo. Matatizo ya kukarabati barabara mara kwa mara yatapungua kama teknolojia sahihi na viwango vya utaalam vitafuatwa katika hatua zote za usanifu na ujenzi wa barabara zetu. Kazi hii isimamiwe vizuri na Halmashauri za Wilaya na Miji kwa kutumia fedha wanazogawiwa na Mfuko wa Barabara zikisaidiana na nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kurekebisha sekta ya uchukuzi ili kuongeza ufanisi na kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi. Sera ya Taifa ya uchukuzi pamoja na mikakati ya utekelezaji wake imekamilika. Zoezi la kurekebisha mifumo ya umilikaji, uendeshaji na utoaji wa huduma katika taasisi zilizo chini ya sekta ya uchukuzi linaendelea. Serikali ilikamilisha rasmi zoezi la kubinafsisha Shirika la Ndege la Tanzania mwezi Desemba, 2002 kwa kuiuzia Shirika la Ndege la Afrika Kusini hisa zake asilimia 49 na hisa asilimia 51 kubakia Serikalini. Kampuni mpya iitwayo *Air Tanzania Company Limited (ATCL)*, imekwishaundwa na itafanya kazi ya usafirishaji wa anga ndani na nje ya nchi yetu. Tunatarajia kampuni hiyo itaongeza safari za hapa nchini na nje kwa kuongeza ndege zake na pia huduma zake zitaimarika. Mipango ya ukodishaji wa Shirika la Reli, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia na Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, huduma za mawasiliano kwa njia ya simu zimeendelea kupanuka na kuimarika. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Kampuni ya Simu Tanzania imejenga mitambo mipya ya kuunganisha mawasiliano ya simu katika miji kadhaa ikiwemo ya Maswa (njia 1500), Bariadi (njia 512), Meatu (njia 512) na Ileje (njia 512). Njia ya mawasiliano katika Wilaya za Shinyanga, Maswa, Meatu, Bariadi imeboreshwa kwa kuwekewa mitambo inayojiendesha yenyewe. Uboreshaji huo umefanyika pia katika Mji mdogo wa Lalago. Miradi mingine iliyotekelezwa ni kuunganisha njia ya mawasiliano katika Miji ya Songea na Mbinga, kufunga mitambo ya *digital* kwenye njia ya mawasiliano ya Makambako - Ilembula na kuboresha mtambo wa kurusha mawasiliano ya simu kwenye njia ya Lindi, Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, upanuzi wa huduma za simu utafanyika katika maeneo muhimu ya kiuchumi ya migodi ya dhahabu ya Kahama na Buhemba, Kiwanda cha Saruji Tanga, Kiwanda cha Sukari Kagera, mashamba ya chai ya Kibena na Mufindi, eneo la hoteli za kitalii Bagamoyo na Pwani ya Mashariki ya Zanzibar. Aidha, mitambo ya kisasa itawekwa katika njia kadhaa muhimu nchini za Mbeya - Kaluwe - Sumbawanga, Nyololo - Songea, Mwanza - Geita - Bukoba, Njombe - Makete, Njombe -Ludewa, Kaluwe - Tunduma, Kaluwe - Mbozi, Kaluwe - Ileje na Sumbawanga - Namanyere. Upanuzi na uwekaji wa mitambo mipya utafanyika katika Miji ya Igunga, Nzega, Isaka, Babati, Bukoba, Kigoma, Singida na Mtwara. Serikali pia itafanya utafiti wa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mfuko Maalum wa kusaidia mawasiliano vijijini ili kuboresha huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni raslimali muhimu na ni mojawapo ya misingi mikuu ya maendeleo ya sekta zote za uchumi. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Serikali iliandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Wilaya ya Ileje, Namtumbo, Sikonge, Kilombero, Mvomero, Musoma, Urambo, Nzega na Mpanda. Mipango hiyo imetumika kutambua maeneo ya kipaumbele katika kuandaa mipango ya maendeleo wilayani. Katika ngazi ya vijiji, mipango hiyo imetumika kutambua na kuhifadhi haki za umilikaji na matumizi ya ardhi na raslimali zake kwa mtu mmoja mmoja au kwa vikundi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imetoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuchangia gharama za upimaji wa vijiji na kuongeza kasi ya kuvipatia vijiji Cheti cha Ardhi ya Kijiji kulingana na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999. Upimaji wa mipaka ya vijiji ulifanyika katika Wilaya ya Mbozi, Tunduru, Mbinga, Iramba na Singida Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ardhi pia hutumika kuwekeza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika juhudi za kuongeza na kurahisisha uwekezaji nchini, Serikali imeanzisha Hazina ya Ardhi ambayo itasaidia wawekezaji kupata maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Hadi tarehe 31 Mei, 2003, kiasi cha hekta 4.1 milioni zilitambuliwa kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara. Kazi ya kubaini maeneo ya aina hiyo inaendelea nchini kote kwa maeneo ambayo hayajafikiwa. Maeneo hayo yatapimwa kwa ajili ya matumizi ya wawekezaji wa ndani na nje katika shughuli mbalimbali za uzalishaji ambazo ni pamoja na kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini na viwanda. Napenda kuchukua fursa hii, kuwataka wananchi wote watoe ushirikiano mzuri ili Serikali ikamilishe zoezi hilo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya ardhi ni muhimu katika kuleta maendeleo ya jamii. Tusipokuwa na matumizi bora ya ardhi tunasababisha ardhi yetu kugeuka jangwa na kuwepo kwa migogoro mingi. Hivyo, ni muhimu raslimali hiyo ikatumiwa kwa busara. Njia mojawapo ni kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo inaheshimiwa na jamii kwa mujibu wa sheria zilizoko. Wale wanaokiuka waadhibiwe mara moja. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itaendelea kuhimiza na kusimamia

misingi ya matumizi bora ya ardhi kwa kupeleka mamlaka na uwezo wa kufanya maamuzi katika ngazi za Wilaya na Kata. Pia itaanzisha mfumo wa jumla wa utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi itakayowezesha mipango mingine ya kisekta kuandaliwa na kuwezesha kuwepo kwa misingi ya ushirikiano baina ya sekta mbalimbali kuanzia ngazi ya Taifa, Kanda na Mkoa. Aidha, itafanya utafiti wa matumizi ya ardhi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya ongezeko la idadi ya watu, maliasili na shughuli nyingine zinazofanyika humo. Kuhusu upimaji wa mipaka ya vijiji, Serikali itaweka alama na kupima mipaka ya vijiji 600 katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 mchango wa sekta ya nishati kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 kama ilivyokuwa mwaka 2001. Pamoja na mchango wake kutoongezeka, sekta hiyo bado ni muhimu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Serikali imeshirikisha sekta binafsi katika kuwekeza kwenye sekta ya nishati na kuendeleza vyanzo mbalimbali vya uzalishaji nishati vilivyomo nchini. Katika mwaka 2002/2003, Makao Makuu ya Wilaya za Sikonge na Mbarali na vijiji 90 vilipatiwa umeme. Kazi ya kupeleka umeme Wilaya za Biharamulo na Ngara imeanza. Mradi wa kusafirisha gesi ya Songo Songo hadi Dar es Salaam nao umeanza kutekelezwa. Kufikishwa kwa gesi hiyo kwenye mitambo ya umeme ya Ubungo kutasaidia kuwa na chanzo kingine cha umeme kitakachounganishwa katika Gridi ya Taifa. Aidha, wananchi wa Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es Salaam, watanufaika kwa vile gesi hiyo inaweza pia kutumika majumbani kupikia na hivyo kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Vile vile viwanda vikubwa vitaweza kutumia gesi hiyo moja kwa moja kuendesha mitambo ya uzalishaji. Katika mwaka 2003/2004, Shirika la Umeme nchini limetenga shilingi 100 bilioni kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ambayo kwa sasa inakabiliwa na uchakavu wa vifaa na mitambo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Serikali iliendelea kutoa huduma za jamii zilizo bora kwa wananchi wengi zaidi. Katika sekta ya elimu utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi umeendelea kutekelezwa katika kila Halmashauri nchini. Uandikishaji wa watoto wenye umri wa kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2003 uliendelea vizuri na ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa na ukarabati wa baadhi ya majengo ya zamani ulifanyika. Kati ya Julai, 2002 hadi Machi, 2003, vyumba vya madarasa 9,820, nyumba za walimu 155 na matundu ya vyoo 10,469 vimejengwa. Ujenzi na ukarabati huo umefanya majengo mengi ya shule za msingi yapendeze na kuwa na hadhi ya kutoa elimu. Utekelezaji wa mpango huo pia umehusisha ajira mpya kwa walimu na upatikanaji wa vitabu na vifaa vingine vya kufundishia vilipatikana.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi kifupi cha mpango huo yanaonesha jinsi Watanzania tulivyo na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo na kero mbalimbali pale tunapodhamiria. Mathalani, Halmashauri zilizofanya vizuri sana katika ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu ni zile zilizowashirikisha wananchi kwa karibu zaidi. Halmashauri ambazo viongozi wake wamepuuza nguvu za wananchi, wamejenga vyumba vya madarasa vichache na hivyo kuendelea kuwa na tatizo kubwa la upungufu wa vyumba. Serikali ilichukua hatua kurekebisha upungufu uliojitokeza katika Halmashauri chache zilizohusika. Napenda pia kuzikumbusha Halmashauri za Miji na Wilaya kuwa suala la utengenezaji wa madawati liendelee kupewa kipaumble ili ifikapo mwezi Desemba, 2003 kusiwepo na mtoto atakayekuwa anakaa chini kwa kukosa dawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwezo wa usimamizi wa mpango huo, Serikali imetoa mafunzo ya uwezeshaji kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za elimu nchini. Mafunzo hayo yamewasaidia viongozi hao kupata ujuzi wa kusimamia vizuri utekelezaji wa mpango wa kuboresha elimu ya msingi, pamoja na kuzisaidia kamati za shule za msingi, kutekeleza wajibu wake kikamilifu. Ni vyema viongozi na wataalam katika Halmashauri wachukue jukumu la kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi watambue kuwa mpango wa kuboresha shule za msingi ni wao na hivyo ni lazima wajihusishe nao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutayarisha mikakati ya kupanua elimu ya sekondari kwa kukarabati majengo, pamoja na kuimarisha ukaguzi wa shule ili ziweze kutoa elimu iliyo bora. Kwa vile wananchi wameitikia kwa ari kubwa wito wa kujenga shule za sekondari na ili kulinda ubora wa elimu hiyo, Serikali imeimarisha taratibu za usajili wa shule mpya ili kuhakikisha kuwa shule zinazosajiliwa ni zile tu zilizotimiza masharti. Katika kukabiliana na upungufu mkubwa wa walimu wa shule za sekondari, Serikali iliajiri walimu 1,859.

Hata hivyo, kutokana na uboreshaji wa elimu ya msingi, hivi sasa limezuka tatizo jipya la wanafunzi wengi kuachwa kuchukuliwa kuingia sekondari japo wamefaulu kwa sababu ya nafasi chache katika shule za sekondari. Hivyo, uongozi wa kila Wilaya nchini, uanze kuchukua hatua za kuongeza idadi ya shule za sekondari ili kukabiliana na tatizo hilo. Aidha, katika kuwasaidia watoto wenye matatizo maalum ya kushindwa kumudu gharama za elimu, Serikali ilitenga shilingi 1.1 bilioni na kuzigawa katika Halmashauri zote nchini kukabili tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya juu, Serikali imeendelea kutekeleza zoezi la uhuishaji wa taasisi mbalimbali za mafunzo ya elimu nchini ili kuzifanya ziwe na ufanisi zaidi. Zoezi la kusajili Vyuo Vikuu limeendelea katika ngazi mbalimbali za usajili na hivyo kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu vinavyoruhusu kutoa mafunzo nchini. Mfuko wa Elimu umeanza kazi rasmi na Serikali inaamini kuwa kujengeka kwa uwezo wa Mfuko huo kutasaidia kujenga miundombinu ya elimu katika ngazi zote. Vile vile Serikali imeanza kuchukua hatua za kuanzisha chombo maalum kitakachosimamia mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kuhusu elimu ya ufundi, Serikali imekarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali katika vyuo vya ufundi vya Arusha, Mbeya na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Serikali itakarabati majengo kwenye vyuo, itaimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na utumiaji wa teknolojia ya mawasiliano katika ufundishaji.

Aidha, Serikali itaendelea kupanua na kuimarisha mafunzo kwa wanafunzi wa kike wenye sifa za kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Vile vile kupitia Mabaraza ya Elimu ya Juu na Ufundi, itasajili vyuo vyenye uwezo wa kutoa mafunzo na kuendelea kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa. Napenda kutoa wito kwa wananchi kuhakikisha kuwa wanatumia huduma za vyuo au taasisi zilizosajiliwa na mabaraza hayo na kupewa idhini ya kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, taratibu za kuanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii katika Wilaya zote nchini, zimeendelea kutekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali katika Wilaya hizo. Hadi sasa Mifuko ya Afya ya Jamii imeanzishwa katika Halmashauri 42. Aidha, mfumo wa uchangiaji wa huduma za afya unatekelezwa katika Hospitali za umma za ngazi zote. Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya watumishi wa Serikali nao umeendelea kuimarishwa na mawasiliano kati yake na Hospitali, Zahanati na Vituo vya Afya vinavyotoa huduma yameimarishwa. Kazi nyingine muhimu inayotekelezwa ni kusaidia kuboresha mipango ya afya kwa Wilaya 113, ikiwa ni pamoja na kuwajengea Waganga Wakuu wa Mikoa uwezo wa kukusanya na kuhifadhi takwimu za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikamilisha awamu ya mwisho ya mpango wa kuzipatia hospitali vifaa muhimu kwa kuimarisha vyumba vya *X-Ray* na kufunga mashine mpya za *X-Ray* na *Ultrasound* katika hospitali 15 za Kanda ya Ziwa Victoria. Ukarabati wa majengo ya Maabara umefanyika katika Hospitali za Wilaya za Pangani, Lushoto, Ulanga na Handeni. Kazi ya ukarabati mkubwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imeanza, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia, vifaa vya mawasiliano na vifaa vya kuzuia. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Serikali kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali itakamilisha Sera ya Taifa ya Afya. Pia itaendelea kuwashirikisha wananchi katika kuimarisha Mifuko ya Bima ya Afya ya Jamii, uchangiaji wa huduma ya afya na kuwashirikisha wadau wote katika kuinua viwango vya ubora wa huduma zitolewazo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, mradi mkubwa wa kuongeza uwezo wa upatikanaji wa maji katika Mji wa Dodoma ulikamilika. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Dodoma kutoka meta za ujazo 24,000 hadi meta za ujazo 40,000. Mradi mwingine mkubwa unaoendelea kutekelezwa ni ule wa Chalinze ambao umefikia asilimia 80 ya utekelezaji. Aidha, ujenzi wa miradi ya maji katika Wilaya mbalimbali iliendelea kutekelezwa na baadhi ya Vijiji katika Wilaya hizo vimeanza kupata maji. Mamlaka za Maji Mijini zimeimarisha ukusanyaji wa mapato yao kutoka jumla ya wastani wa Shilingi bilioni 8.6 kwa mwaka 2000/2001 hadi wastani wa Shilingi bilioni 11.7 kwa mwaka 2001/2002. Uwezo huo wa kifedha umeziwezesha Mamlaka hizo kuwafikishia maji wananchi wengi zaidi Mijini. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, Serikali imekamilisha taratibu za ukodishaji wa uendeshaji wa huduma za miundombinu ya *DAWASA* kwa Makampuni ya *Biwater* na *Gaulf Engineer*. Kampuni hizo zimeunda Kampuni ya *City Water Services Limited* itakayosimamia shughuli za kila siku za *DAWASA* kuanzia Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa vyanzo vingi vya maji nchini vipo kwenye mabonde, Serikali imechukua hatua za kuanzisha Bodi Maalum za Maji zitakazosimamia raslimali hiyo muhimu kwa uhai na ustawi wa Taifa letu. Katika kuboresha utunzaji wa vyanzo vya maji, wananchi wameshirikishwa katika kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji katika Mabonde ya Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu na Ziwa Nyasa. Hata hivyo, bado wapo baadhi ya wananchi wanaoishi na kufanya shughuli zao kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Ili kuondoa tatizo hili, Bodi hizo za Maji na zile za mabonde kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali tangu ngazi ya Vijiji hadi Mikoa, zihakikishe kuwa vyanzo vyote vya maji kwenye mabonde na milimani vinalindwa na kuhifadhiwa. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itaendeleza kazi za upanuzi wa miradi ya maji katika Wilaya mbalimbali, uchimbaji wa visima virefu katika baadhi ya maeneo kame na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Shinyanga na Kahama. Serikali pia, itafanya utafiti kwenye maeneo 400 nchini ili kutambua maeneo yanayofaa kuchimba visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha jamii kutambua na kuthamini maendeleo yenye usawa wa kijinsia, Serikali imehimiza na kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanaingizwa katika sera, mikakati na programu mbalimbali za Kitaifa. Hivi sasa upo mwamko mkubwa wa masuala ya jinsia kote nchini. Mwamko huo umesaidia sana kuihamasisha jamii yetu kutambua haki za wanawake na kushiriki katika vita dhidi ya vitendo vyovyote vinavyowabagua, kuwanyanyasa na kuwadhalilisha wanawake. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itaimarisha utaratibu wa masuala ya jinsia katika ngazi za utawala na uongozi wa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Mikoani na Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Bunge lako Tukufu liliridhia Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto na Itifaki za Nyongeza Kuhusu Ushirikishwaji wa Watoto katika Migogoro ya Kivita na ile ya Biashara ya Kuuza Watoto, Ukahaba kwa Watoto na Upigaji Picha za Udhalilishwaji wa Watoto. Pamoja na kuridhia mikataba hiyo, jukumu la awali la malezi na matunzo ya mtoto ni la mzazi au mlezi. Natoa wito kwa Watanzania wote kuthamini watoto na kuwapatia fursa za kuendeleza vipaji vyao na kupiga vita kabisa utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuanzisha Cheo cha Afisa Mtendaji wa Mtaa katika maeneo ya Mijini. Kama ilivyo katika maeneo ya Vijijini, Maafisa hao ndio watakaokuwa na wajibu wa kuongoza na kuratibu shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Pale ambapo yupo Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa aliye mbunifu na mwenye uwezo wa kuwahimiza na kuwashawishi wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, Vijiji na Mitaa husika imepiga hatua kubwa katika maendeleo. Jukumu la Uongozi wa Halmashauri ni kuwajengea uwezo wataalam hawa ili waweze kutimiza wajibu wao kikamilifu. Serikali ya Mtaa au Kijiji ni Serikali kamili na kwa msingi huo ni wajibu wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuziimarisha na kuzijengea uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya na Miji zinao wajibu wa kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na taratibu za fedha za Serikali za Mitaa zinazingatiwa. Jitihada zinazochukuliwa na baadhi ya Halmashauri katika kutekeleza wajibu huo zinatia moyo. Kwa mfano, katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa hesabu za Halmashauri zilizoishia Desemba, 2001, Halmashauri 68 zilipata hati safi za ukaguzi ikilinganishwa na Halmashauri tatu tu, mwaka 2000. Aidha, Halmashauri 40 zilipata hati chafu ikilinganishwa na Halmashauri 76 mwaka 2000. Pamoja na juhudi hizo zinazoonekana, Viongozi wa Halmashauri zote nchini na wataalam wao, wanao wajibu wa kusimamia matumizi ya fedha kulingana na Sera, Kanuni na taratibu zilizopo. Wajibu huo unakuwa mkubwa hivi sasa kwa vile Serikali Kuu imeelekeza fedha nyingi zaidi katika Halmashauri. Halmashauri zote zizingatie kwa ukamilifu usimamizi wa matumizi ya fedha na zitoe taarifa za utekelezaji kwa wakati katika ngazi zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, Serikali imekuwa ikitekeleza programu mbalimbali ambazo malengo yake ni kuweka mfumo imara na endelevu wa Utawala Bora. Programu hizo zinahusu mageuzi ya utendaji katika utumishi wa umma, usimamizi wa fedha za umma, uendeshaji wa Serikali za Mitaa, marekebisho katika Sekta ya Sheria, mikakati ya kuondoa umasikini na kupambana na rushwa. Katika mwaka 2002/2003, Serikali iliendelea kujenga mazingira mazuri ya kuwawezesha watumishi wa umma kufanya kazi zao kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kuleta ufanisi, tija na nidhamu kazini.

Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ilipewa nguvu ya kisheria baada ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2002 kuanza kutumika hapo Julai mosi mwaka jana, 2002 na hivyo kurahisisha utekelezaji wake. Katika mwaka 2003/2004, mkazo utawekwa kwenye kukuza raslimali-watu kwa Wizara na Idara za Serikali kuanza kutekeleza mipango yao ya mafunzo. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ndio njia ya kuliwezesha Taifa kupata wataalam na wafanyakazi wenye elimu, ujuzi wa kutosha na uwezo wa kutoa huduma bora kwa jamii. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mifumo mipya ya utendaji kazi katika utumishi wa umma na kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, Utawala wa Sheria ni moja ya nguzo kuu ya Utawala Bora na Demokrasia nchini. Katika kuboresha na kuimarisha vyombo vya utoaji haki nchini, mafunzo yalitolewa kwa Mahakimu 600 wa Mahakama za Mwanzo, 300 wa Mahakama ya Hakimu Mkazi na Majaji 34 wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itaandaa sera itakayosimamia Sekta ya Sheria, pamoja na kuendelea kuboresha mikakati ya utoaji wa haki nchini, ikiwa ni pamoja na kuiongezea Idara ya Mahakama fedha zaidi ili kuongeza ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa ili kuziba mianya ya rushwa katika sekta ya umma, kuzuia matukio ya rushwa, kuboresha mifumo ya uendeshaji na kuweka uwazi katika maamuzi na manunuzi ya Serikali. Ili kusogeza huduma zinazotolewa na Taasisi ya Kuzuia Rushwa karibu na wananchi, Serikali imeajiri Watendaji wengi zaidi na kufungua Ofisi katika Mikoa 20 na Wilaya 46. Sambamba na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali ni muhimu kuhakikisha kuwa vitendo na matukio ya rushwa yanashughulikiwa mara moja. Hivyo, Wizara, Idara zinazojitegemea na wakala wa Serikali ziteue Maafisa wa kufuatilia malalamiko ya wananchi na kuyashughulikia mara moja. Serikali itaendelea na zoezi la kurekebisha sera, miundo, sheria, kanuni na taratibu za kazi, kwani marekebisho hayo kwa kiwango kikubwa yatasaidia kuziba mianya na mbinu zinazotumiwa kuendeleza vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, mashirikiano na mahusiano ya nchi yetu na nchi rafiki na Mashirikiano ya Kimataifa, yalikuwa mazuri. Umoja wa Afrika ulianzishwa rasmi tarehe 9 Julai, 2002. Lengo la Umoja huo ni kuimarisha uhuru na heshima ya Mwafrika kwa kuchochea maendeleo, kupiga vita umaskini na kujijengea misingi imara ya kiuchumi na kisiasa. Ili kutekeleza lengo hilo, Umoja wa Afrika una mpango wake wa maendeleo wa kiuchumi, unaoitwa *NEPAD*, ambao unawataka Waafrika kukubali kuwa wajibu wa kwanza wa kujiendeleza ni wao wenyewe ingawa Mataifa mengine ya nje yana wajibu wa kuwaunga mkono, kuwatendea haki na kutoa upendeleo maalum kwa nchi maskini zaidi. Mkakati mmojawapo ni ushirikiano wa kikanda kama ule wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiuchumi wa Nchi za Afrika Magharibi, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, taratibu za kuwawezesha raia wa nchi zote tatu kuvuka mipaka ya nchi yetu ziliendelea kuboreshwa kwa kutumia pasi za kusafiria za Afrika Mashariki. Aidha, nchi zetu zimefikia hatua ya kutia matumaini katika harakati za kuanzisha Umoja wa Forodha. Katika mashirikiano na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Tanzania ilishiriki katika shughuli zote za Jumuiya hiyo na hasa utekelezaji wa sera zake. Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wananchama wa Jumuiya hiyo utakaofanyika Mjini Dar es Salaam mwezi Agosti, 2003 na kuchukua Uenyekiti. Nachukua fursa hii kuwahimiza wananchi wote hasa sekta binafsi, kutoa mchango wa hali na mali katika kufanikisha Mkutano huo muhimu, ambao mafanikio yake yatazidi kuijengea nchi yetu heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa mstari wa mbele katika juhudi za kumaliza migogoro ya kisiasa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kutokana na ushawishi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kundi la *CNDD - FDD* lilikubali kutia saini mkataba wa kusitisha mapigano na Serikali ya mpito ya Burundi tarehe 2 Desemba, 2002. Juhudi bado zinaendelea kukishawishi kikundi cha *PALIPEHUTU-FNL* kutia saini mkataba huo. Utekelezaji wa mkataba wa amani nchini Burundi ulichukua sura mpya na wenye matumaini pale mabadiliko ya uongozi wa Serikali hiyo yalipofanyika kulingana na makubaliano ya Arusha ya mwaka 2000. Tarehe 30 Aprili,

2003, Rais Pierre Buyoya, alimkabidhi madaraka ya kuiongoza Burundi, Rais mpya ambaye ni Mhutu, wa kipindi cha mpito, Mheshimiwa Domitien Ndayizeye.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizofikiwa, kwa bahati mbaya amani bado haijarejea Burundi na bado kuna makundi yanayopambana na Majeshi ya Serikali. Hata hivyo, bado ni matumaini yetu kwamba hatimaye amani itapatikana Burundi. Katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, makubaliano yalifikiwa ya kuwa na Katiba mpya inayounda Serikali ya mpito. Tunawapongeza wananchi wa Kongo kwa hatua hiyo ambayo inajenga mazingira bora ya Uchaguzi Mkuu, ingawa bado kuna mapambano katika maeneo hasa ya Mashariki mwa nchi hiyo. Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali za nchi za eneo la Maziwa Makuu na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuleta pia amani katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa demokrasia ya kweli ni ule unaotoa fursa kwa wananchi kujadili masuala mbalimbali yanayowahusu, hatimaye kufikia maamuzi ya muafaka. Ili kushirikishwa huko kuwe na ufanisi, inabidi wananchi wafahamu vyema sera za Serikali na maendeleo ya utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuleta maendeleo. Ni jukumu la Vyombo vya Habari kutoa taarifa zenye uchambuzi wa kina utakaowapa wananchi fursa ya kujadili na kutoa michango yao ipasavyo. Jukumu hilo linawezekana ikiwa mfumo wa utoaji habari kwa kutumia utaalam na teknolojia ya kisasa na kuweka uwazi zaidi katika maamuzi yanayohusu wananchi utaboreshwa.

Aidha, vyombo vya habari inabidi viwe huru, imara na vinavyowafikia wananchi wengi na vinavyowajibika kwa jamii. Vile vile vyombo hivyo inabidi viwe na Watendaji wenye utaalam wa kutosha na unaozingatia maadili ya taaluma na ya jamii nzima. Vyombo vya Habari vikubali kuwa navyo ni sehemu ya Tanzania na wananchi wanatarajia kupata huduma nzuri na ya manufaa kutoka vyombo hivyo katika kujiletea maendeleo. Uhuru unaotolewa kwa vyombo vya habari isiwe ni leseni ya kuchapisha na kutangaza habari za uongo, zenye uchochezi na kashfa, zenye kuchochea vitendo vya ngono au kuvunja maadili ya jamii. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itaendelea kuimarisha na kuweka mfumo madhubuti wa mawasiliano kati ya Serikali na Vyombo vya Habari na kati ya Serikali na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Serikali ilisajili Magazeti na Majarida mapya 41. Hii inafanya nchi yetu kuwa na Magazeti na Majarida 422 yaliyosajiliwa na kati ya hayo 17 yanachapishwa kila siku. Idadi ya Vituo vya Redio ni 29, Televisheni za kawaida 13 na Televisheni za kulipia 19. Aidha, Halmashauri 11 za Wilaya na Miji zinaendesha huduma ya Televisheni. Taasisi ya Utangazaji iliyoundwa baada ya kuunganisha Redio Tanzania na Televisheni ya Taifa, imeanza rasmi Julai, 2002. Serikali imeteua Bodi ya Taasisi hiyo ambayo hivi sasa inatekeleza kazi ya kuunganisha vyombo hivyo viwili ili viwe chini ya utawala mmoja. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Taasisi hiyo itatekeleza majukumu mawili makubwa. Kwanza ni kuendelea kuboresha usikivu wa Redio Tanzania na kuhakikisha kuwa mitambo ya kurushia matangazo ya Vituo vya Dodoma, Kigoma, Nachingwea, Songea, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dar es Salaam inafanya kazi kwa uwezo wake wote. *(Makofi)*

Jukumu la pili ni kuendeleza ujenzi wa mitambo ya TVT ili kuwezesha matangazo yake kuonekana nchi nzima. Ili kutekeleza azma hiyo, hatua zimechukuliwa ili kurusha matangazo ya TVT kwa njia ya satelaiti ikiwa ni pamoja na kujenga Vituo vya kupokea na kurusha matangazo. Katika awamu ya kwanza Vituo vya Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya, Lindi na Tabora vitakamilika kujengwa na hivyo kuwawezesha wenye Televisheni Mikoani humo kupata matangazo ya TVT moja kwa moja. Vile vile, kukamilika kwa mtandao wa kuunganisha matanganzo ya TVT kwenye satelaiti kutawawezesha wananchi wa Mikoa mingine kupata matangazo hayo kupitia kwenye Televisheni za Halmashauri za Miji na Wilaya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Serikali iliimarisha Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali, kwa kuipatia mitambo ya kisasa yenye uwezo mkubwa zaidi kiteknolojia. Kwa ajili hiyo, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na zile za Bajeti na chaguzi ndogo zilizofanyika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ulikamilishwa kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Idara hiyo imeteuliwa na Bunge la Afrika Mashariki kuchapisha nyaraka zake pamoja na Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2003/2004, Serikali itaendelea kuipa uwezo Idara hiyo ikiwa ni pamoja na kuanza taratibu za kuifanya iwe Wakala wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na Makazi ilifanyika Agosti, 24, mwaka 2002 na matokeo yake yalitangazwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, tarehe 31 Desemba, 2002. Tanzania sasa ina wakazi 34,569,232. Kati ya hao 984,625 wanaishi Tanzania Zanzibar na 33,584,607 wanaishi Tanzania Bara. Ongezeko la watu Tanzania Bara ni wastani wa asilimia 2.9 kwa mwaka na asilimia 3.1 kwa mwaka Tanzania Zanzibar. Mkoa wa Kigoma unaongoza kwa kuwa na ongezeko la watu la asilimia 4.8 kwa mwaka, wakati Mkoa wa Lindi ndio wenye ongezeko dogo kuliko Mikoa yote la asilimia 1.4 kwa mwaka. Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na msongamano mkubwa wa watu katika kilometa moja ya mraba ambao ni watu 1,793 ukifuatiwa na Mkoa wa Mjini Magharibi wenye watu 1,700 kwa kilometa moja ya mraba.

Mkoa wenye msongamano mdogo wa kilometa moja ya mraba ni Lindi wenye watu 12, ukifuatiwa na Mkoa wa Rukwa wenye watu 17 kwa kilometa moja ya mraba. Mkoa wa Shinyanga una wakazi wengi zaidi ambao idadi yao ni milioni 2.8, wakati Mkoa wa Lindi ndio wenye wakazi wachache zaidi kwa Tanzania Bara ambao ni watu 791,306. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wenye wakazi wengi ni Mjini Magharibi wenye watu 391,000 na Kusini Unguja ndio wenye watu wachache wapatao 94,504.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa sensa ni chanzo pekee cha kupata takwimu sahihi inayowahusu watu wa marika na jinsia na hali yao ya kijamii na kiuchumi. Takwimu hizo ni muhimu katika kubuni sera za maendeleo, kujua ubora wa maisha ya wananchi na uwekaji wa mfumo endelevu wa maendeleo. Takwimu za sensa zitasaidia Wilaya kubuni mipango ya maendeleo kulingana na hali halisi iliyopo ya watu na Makazi yao. Kutokana na sensa hiyo, Serikali imeweza kupata takwimu zitakazotumiwa kuandaa viashirio vya hali ya umaskini. Aidha, sensa imetoa takwimu juu ya ongezeko la idadi ya watu na mtawanyo wake kwa umri, jinsia na mahali walipo.

Ni jukumu la Wizara na Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi za Taaluma na Utafiti, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Kimataifa, Vyama vya Siasa na wengineo, kuzingatia na kutumia takwimu zilizopatikana kutokana na sensa ya mwaka 2002 katika kutayarisha mipango ya maendeleo kwa wananchi.

Napenda kuwashukuru wananchi wote, Viongozi na Watendaji wa Serikali, kwa kufanikisha zoezi la sensa. Hali kadhalika, kwa niaba ya Serikali na wananchi wote wa Tanzania nashukuru nchi za Sweden, Marekani, Uingereza, Japan, Finland, Norway, Benki ya Dunia na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNFPA*, *UNICEF* na *UNDP* kwa michango yao mikubwa iliyofanikisha maandalizi na hatimaye kukamilisha zoezi zima la Sensa ya Watu na Makazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, nchi yetu ilikumbwa na maafa ya aina mbalimbali. Baadhi ya maafa hayo ni tetemeko la ardhi kama lililotokea Shinyanga, Dodoma na maeneo mengine ndani ya bonde la ufa. Vimbunga pamoja na mvua zenye upepo mkali vilivyotokea katika Wilaya kama za Kilombero na Mbozi ambapo nyumba na Shule ziliezuliwa. Aidha, yalitokea mafuriko katika Mikoa ya Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya na kwingineko yaliyoharibu majengo, mashamba, miundombinu na kusababisha maporomoko ya udongo. Janga la moto pia lilitokea na kuunguza Shule ya Sekondari ya Toyambe, Mkoani Kagera na ile ya Shauritanga Mkoani Kilimanjaro.

Maafa mengine ni ajali za barabarani na ile ya gari moshi iliyotokea Mkoani Dodoma tarehe 24 Juni, 2002. Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu 294 ikijumuisha waliofariki mahospitalini baadaye na wengine 539 kujeruhiwa. Aidha, Taifa lilipata hasara ya takriban Shilingi bilioni 5.1 kutokana na uharibifu wa mabehewa na reli. Kutokana na ajali hiyo, Serikali ilitoa kifuta machozi cha Shilingi 500,000 kwa kila aliyekufa, Shilingi 100,000 kwa kila aliyejeruhiwa na viungo vya bandia kwa waliopata ulemavu na kuhitaji viungo hivyo. Malipo hayo yalipelekwa kwenye Mikoa husika ili wahusika wote walipwe.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa nchi inajiandaa kukabiliana na maafa yanayotokea, Serikali imetoa mafunzo kwa Maafisa 40 watakaosimamia na kuratibu masuala ya maafa katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Taasisi zinazohusika na maafa na kufanya utafiti wa kubaini majanga yanayosababisha au yanayoweza kuleta maafa nchini.

Aidha, tathmini ya hali halisi ya udhibiti wa maafa ilifanyika nchini ili kubaini uwezo na upungufu uliopo kisheria na kimipango kwa lengo la kufanya marekebisho na kuandaa mtaala wa kufundishia Mafunzo ya Maafa kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Elimu na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtaala huo utatumika kutoa mafunzo katika Kituo cha Mafunzo ya Udhibiti wa Maafa kilichopo Chuoni hapo.

Katika mwaka 2003/2004, Serikali itakamilisha zoezi la kutambua maeneo yenye maafa katika Wilaya zilizosalia. Aidha, Mikoa itawezeshwa kuunda Kamati za Maafa na Kamati za Kisekta na kitaalam zitaundwa ili kuweza kutoa ushauri unaotakiwa pale inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, hali ya mvua katika msimu wa mwaka 2002/2003, haikuwa ya kuridhisha. Takwimu za mvua zinaonesha kuwa katika maeneo mengi nchini, mvua zilinyesha ama kwa kiwango kidogo au kwa mtawanyiko mbaya au kuchelewa mno kiasi cha kutoweza kuyanusuru mazao yaliyokwishapandwa.

Kulingana na uchambuzi wa taarifa kutoka Mikoa yote, athari za hali ya hewa kwa mazao zilifikia viwango vya kati ya asilimia 35 hadi 70. Ni dhahiri kuwa katika msimu wa mwaka 2003/2004, kutakuwepo na upungufu mkubwa wa chakula na uzalishaji wa mazao mengine ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa makini hali ya mvua na kutoa maelekezo kwa wananchi kuhusu hatua za kukabiliana na hali ya ukame. Kila mkulima atumie chakula alichovuna kutokana na mavuno ya msimu uliopita na ajiwekee akiba. Wananchi walioko kwenye Mikoa yenye vyakula vya ziada na ambao hawana akiba ya chakula cha kutosheleza mahitaji ya familia, wajinunulie chakula sasa na kujiwekea akiba.

Wafugaji wauze baadhi ya mifugo yao wakati huu ambapo bado ina afya nzuri na watumie fedha watakazopata kujinunulia chakula. Mikoa yote yenye maeneo yanayofaa kwa kilimo cha kiangazi ihakikishe kuwa wananchi wanalima maeneo hayo na kupanda mazao ya chakula yanayokomaa kwa muda mfupi.

Aidha, wafanyabiashara wenye uwezo wa kuagiza chakula kutoka nje ya nchi waagize chakula hicho ili kuziba pengo lililopo. Serikali imeongeza kiasi cha akiba ya mahindi katika Hifadhi ya Taifa ya Chakula kutoka tani 47,048 hadi kufikia tani 75,523.

Vile vile hatuna budi kutumia kwa ukamilifu mashamba yote yenye miundombinu ya umwagiliaji na uhakika wa maji. Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza skimu 65 za umwagiliaji zenye hekta 32,516 na kuwaagiza Wahandisi wa Kanda za Umwagiliaji na Mameneja wote wa Mashamba kusimamia kilimo katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, muundo wa utawala wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ulikamilika hivyo kuwezesha kuajiriwa kwa Watendaji wa kuratibu shughuli za Tume. Tume pia imekamilisha mkakati wa Taifa wa kudhibiti ukimwi ambao ulizinduliwa tarehe 10 Mei, 2003 Kwa kusaidiana na Wizara zinazohusika na asasi zisizo za Serikali, Tume imezijengea mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia na kudhibiti kuenea kwa UKIMWI katika maeneo yao. Uwezeshaji huo umefanywa kwa kutoa nyenzo na kuwaimarisha kiutendaji. Jumla ya programu 50 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.3 kutoka Halmashauri 50 ziliidhinishwa na Tume. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinao wajibu wa kushirikiana na wadau wote katika maeneo yao ili kuandaa mipango na programu zenye lengo la kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huu hatari.

Mheshimiwa Spika, Tume itaendelea kushirikiana na Sekta zote ili vita dhidi ya UKIMWI vipewe kipaumbele kinachostahili. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na Washirika wetu wa maendeleo katika jitihada za kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI na kutayarisha mpango wa matibabu kwa walioathirika. Serikali pia itaendelea kushirikiana na mataifa mengine kupitia Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ili kubadilishana uzoefu katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Napenda kusisitiza kwamba mafanikio ya kuondokana na janga hili yatapatikana pale tu vita dhidi ya UKIMWI vitakapokuwa sehemu kamili ya tabia ya Watanzania.

Majumuisho, Mheshimiwa Spika, nchi yetu iko katika dunia ya tatu na wakati mwingine tunaitwa nchi zinazoendelea. Nchi zinazoendelea zinaweza kuwa na raslimali nyingi, lakini kasi ya maendeleo yao bado ikawa ni duni. Hii ni kwa sababu vigezo vingine vinavyohusishwa na ukuaji wa uchumi kitaalam siyo sahihi. Kwa mfano, nchi inaweza kuwa na watu na ardhi, lakini uzalishaji wake ukawa duni kwa sababu watu wake hawana elimu ya kutosha, kiteknolojia wanayotumia ni duni ama ya kizamani, mbegu wanazotumia siyo bora na hawana fedha au mitaji ya kufanyia kazi.

Matokeo ya hali hiyo ni uzalishaji duni kwa ekari na mazao yenye ubora hafifu yasiyoweza kuingia katika soko la ushindani. Hali hiyo pia inajitokeza katika shughuli nyingine za uzalishaji kama utalii, madini na viwanda. Katika mazingira hayo wananchi watauliza kwa nini tuwe maskini wakati raslimali tunazo. Kwa nini tuwe tegemezi wakati nchi yetu ina ardhi nzuri, madini, mito, misitu na mbuga za wanyama. Kwa haraka haraka ni vigumu kupata majibu ya maswali haya. Lakini ukweli ni kuwa majibu yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina raslimali nyingi lakini ni maskini. Kama tulivyoelezwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge, Bajeti ya 2003/2004 ni tegemezi kwa asilimia 45 kutoka utegemezi wa asilimia 48 wa mwaka uliopita. Ukuaji wa Pato la Taifa umeongezeka ukilinganisha na mwaka 2001, wigo wa kodi kama asilimia ya Pato la Taifa nao umeongezeka japo kidogo na mfumuko wa bei umeendelea kupungua. Hivi vyote ni vigezo vizuri na vinavyovutia vya kuimarika kwa uchumi. Katika mwaka 2002/2003, takwimu zinaonyesha kuwa nchi yetu ndiyo iliyovutia waweke zaji wengi kuliko nchi yoyote katika Afrika Mashariki. Nchi marafiki na mashirika ya kimataifa wanatupongeza sana Watanzania kwa juhudi hizo njema.

Lakini pamoja na juhudi hizo, hali yetu bado ni ya umaskini. Ni vyema tuyatumie mazingira hayo mazuri kujenga uchumi imara na endelevu ili matunda yake yasambae kwa walio wengi. Lakini ni wazi kuwa kuna viunzi vya kuvuka kabla ya kufika huko tunakozungumzia. Watanzania ni lazima tufanye kazi kwa bidii sana ili kuongeza tija katika uzalishaji wetu hasa mas hambani na viwandani. Matumizi ya teknolojia ya kisasa nayo ni lazima yazingatiwe ili kuboresha bidhaa zetu ziweze kuwa na thamani kubwa na zishindane katika masoko. Tuchangamkie masoko ya ndani na ya nje hususan masoko katika kanda zetu za uchumi.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wananchi katika shughuli za uchumi wa kisasa bado ni duni. Wengi wao wameshindwa kushiriki kwa sababu ya uwezo mdogo kimtaji, ukosefu wa ujuzi na uzoefu wa biashara pamoja na matatizo yanayohusiana na kutokukopesheka. Hali hiyo inapingana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 na dhana ya kuleta maendeleo yanayoinufaisha na kutoa nafasi ya maendeleo kwa wananchi wengi.

Kutokana na hali hiyo, changamoto iliyo mbele yetu ni kuendelea kubuni na kuzingatia mikakati ya makusudi na upendeleo itakayomwezesha mwananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kuboresha mfumo wa utawala wa kodi, kurekebisha baadhi ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili ziendane na dhana ya uchumi wa uwezeshaji na kuimarisha na ufanisi wa utoaji huduma za hali ya juu kwa umma ili kufanikisha uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, hatuna budi vile vile, kuendelea kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitaji kwa kuhamasisha mabenki ili yakopeshe amana zilizopo kwa gharama nafuu. Sambamba na hilo, tuendelee kuimarisha na kuboresha vyama vya ushirika na vyama vya kuweka na kukopa kama vyanzo muhimu vya kuwapatia wananchi mitaji.

Katika kuwawezesha wananchi kushiriki na kumiliki uchumi wa nchi, kuna suala la kuinua elimu na ujuzi ili wawe na mtazamo wa kisayansi wa kukabiliana na mila na desturi potofu zinazodumaza maendeleo. Tunahitaji kuangalia upya mfumo wa elimu ili uweze kuwajengea wananchi misingi ya ujasirimali na moyo wa ushindani katika soko.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Watanzania kiuchumi katika mwaka huu wa 2003/2004, itawasilisha Sera hiyo kwenye Bunge lako Tukufu pia itawasilisha

Muswada wa Sheria wa kuwawezesha Watanzania kuingia katika uchumi wa nchi yao. Kuwepo kwa Sheria hiyo kutatuwezesha kuunda vyombo vitakavyosaidiana na vile vilivyoko kama Baraza la Taifa la Biashara na vinginevyo, ili kuwezeshaWatanzania kumiliki uchumi kikamilifu. Ni vyema Watanzania waelewe kuwa vyombo hivi pamoja na Sheria havitaendesha kilimo wala biashara. Vyombo hivyo, vitaweka mazingira mazuri ya kuwekeza na kufanya biashara. Jukumu la kufanya biashara ni la mtu au kampuni husika. Watanzania ni vyema tukachukua changamoto hiyo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ili tuendelee ni lazima mipango yetu itumie takwimu sahihi na iwe na malengo ya kutatua matatizo yaliyopo. Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 inatupa takwimu za kufanyia kazi katika shughuli mbalimbali za mipango yetu. Matumaini yangu ni kuanzia sasa takwimu hizo zitakuwa msingi wa kuandaa mipango mbalimbali ya maendeleo katika ngazi zote. Wakati tunafikiria kujikwamua katika umaskini tuone ni takwimu gani zitatusaidia haraka.

Kwa mfano, matokeo ya awali ya uchambuzi yanaonyesha watoto chini ya umri wa miaka 15 ni asilimia 44 na watu wazima wasio na uwezo wa kufanya kazi ni asilimia 4. Hivyo, idadi ya Watanzania tunaowategemea katika juhudi za kufufua uchumi ni asilimia 52 ya watu wote. Sasa tujiulize, je hao wanaotakiwa kufanya kazi, yaani hao asilimia 52 wote wanafanya kazi kweli? Ni wangapi hasa ambao wapo mashambani wanalima, wangapi wapo katika biashara zinazoeleweka, wangapi wapo katika ajira halali. Huu ndiyo umuhimu wa kufanya sensa. Takwimu zitusaidie kuruka baadhi ya viunzi vinavyotukwamisha katika kufufua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa dunia nzima inazungumzia mfumo wa utandawazi. Wapo watu wanaosema tusiukubali utandawazi kwa sababu ni mbinu za wajanja kututawala kiuchumi. Utandawazi ni mfumo wa ulimwengu ambao upo katika kila jambo. Hivyo, dawa siyo kukwepa utandawazi maana haukwepeki, bali ni kuuelewa na kuutumia kwa manufaa yetu. Masoko yetu yanaungana na sote tutashindana katika soko moja. Atakayekwenda na utandawazi kwa maana ya kutengeneza bidhaa nzuri atanufaika na utandawazi. Atakayejidai haendi na utandawazi na hivyo kutokutengeneza bidhaa bora, hatauza katika soko ila soko la nchi yake litapokea bidaa kutoka kwa wengine. Ili tusiwe soko la wengine tuutumie utandawazi vizuri na kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupambana na uhalifu itafanikiwa tu kama kila raia na kila mtu ataona ni wajibu wake wa msingi. Tukitegemea polisi peke yao mafanikio yatakuwa madogo, yatachukua muda mrefu na pengine kwa gharama kubwa. Mathalan, wapo majambazi wanaofanya uhalifu huku wakiwa wanaishi katika nyumba za wageni.

Hivi ni kweli wamiliki au waangalizi wa nyumba hizo wanakuwa hawaoni mienendo na tabia za wateja wao zinazotia mashaka? Hivi ni kweli majambazi hawa hawana ndugu au jamaa wanaoishi nao au kufahamiana? Mbona hatutoi taarifa polisi au katika vyombo vya usalama? Matumaini yangu ni kuwa kila mwananchi ataona jukumu la ulinzi ni la kila mmoja wetu. Serikali itaendelea kupambana na uhalifu bila huruma yoyote na inapobidi nguvu kubwa zaidi itatumika kukabiliana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri wote kwa ushauri wao ambao umewawezesha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutekeleza majukumu yao ya kitaifa kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Marten Lumbanga, pamoja na vyombo vyote vya dola kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuiwezesha kukamilisha maandalizi yote ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004 pamoja na makadirio ya matumizi ya fedha kwa kila Wizara, Mikoa, Taasisi na Idara zinazojitegemea. Nawashukuru Watanzania wote na Washirika wote wa Maendeleo kwa michango yao ambayo ndiyo imeiwezesha Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuwashukuru kipekee, Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, anayeshughulikia Sera na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, anayeshughulikia Habari na Siasa, wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa msaada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa

2002/2003, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani, alikuwa ndiye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Habari na Siasa. Napenda nimshukuru sana kwa msaada mkubwa aliotoa alipokuwa nasi. Ninamtakia kila la kheri katika wadhifa wake mpya. Nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Mheshimiwa Rose Lugembe, kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa mimi na Mawaziri wa Nchi.

Aidha, nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka huu wa 2003/2004. Namshukuru sana Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuichapa hotuba hii kwa unadhifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu katika mwaka wa fedha 2002/2003, imepata misaada na mikopo kutoka kwa wahisani mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa nchi rafiki, nchi fadhili, taasisi za fedha za kimataifa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, mifuko mbalimbali duniani, madhehebu ya dini na Asasi zisizo za Serikali. Misaada na mikopo hiyo imechangia sana katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo yao na tutaendelea kushirikiana nao katika jitihada za kuondoa umaskini na kujenga uchumi imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu 2003/2004, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake pamoja na Ofisi ya Bunge, inaomba jumla ya shilingi 44,245,876,300/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, Ofisi ya Waziri Mku na Taasisi zake inaomba jumla ya shilingi bilioni 32,906,480,700/= na Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya shilingi 11,339,395,600/=.

Aidha, Ofisi ya Waziri na Taasisi zake na Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya shilingi bilioni 20,094,794,900/= kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, fedha Shilingi 7,300,000,000/= ni fedha za hapa na shilingi 12,794,794,900/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina maelezo machache kabla hatujaendelea hasa kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wapya walioapishwa mwanzoni mwa Mkutano huu. Ni kwamba kuanzia leo na kuendelea mpaka tutakapokamilisha vikao vya Bajeti yaani mpaka Wizara zote zitakapokuwa zimekamilika kuwasilisha Makadirio yao tutatumia Kanuni ya 81(1) ambayo inasema hivi:

"Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Wizara inayowasilisha Makadirio yake au Mjumbe mwingine atakayeteuliwa kwa niaba yake atawasilisha Mezani Taarifa ya Kamati yake kama alivyofanya Mwenyekiti leo asubuhi".

Lakini pia baada ya hapo atapewa nafasi wakati wa mjadala kutoa maoni ya Kamati yake, muda wake wa kusema hautazidi dakika 30. Baada ya hapo Mwenyekiti atafuatiwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara inayohusika, ili atoe maoni ya upande wa Upinzani. Muda wake kusema vile vile hautazidi dakika 30. Mbunge mwingine yeyote atakayepata nafasi ya kuchangia atazungumza kwa muda usiozidi dakika 15, isipokuwa kwamba muda wa Waziri Mkuu kusoma hotuba yake utaamuliwa na Spika kadri atakavyoona inafaa. Ndiyo maana hakupigiwa kengele. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa tutafuata mpangilio huo ulioko kwenye Kanuni na kama nilivyoeleza asubuhi kwamba kwa Kanuni hizi mpya baada ya mjadala kumalizika kwa kila Wizara pamoja na hii tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi yaani Kamati ya Bunge Zima ya Matumizi na katika Kamati hiyo Mwenyekiti atawahoji Wabunge kuhusu kifungu kimoja kimoja ya Makadirio ya Matumizi ya mwaka na kila kifungu kitaafikiwa peke yake. Ndiyo utakuwa utaratibu.

Sasa baada ya hapo niseme tu kwamba katika orodha ambayo ina wasemaji 50 sasa tutawapa nafasi wale ambao hawajachangia, kwa wale ambao hawakuchangia hoja iliyopita. Ni katika kujaribu kuwapa nafasi Wabunge wengi zaidi wapate nafasi ya kutoa mawazo yao. Sasa tutaanza na wale ambao hawajachangia kabisa, nafasi ikiruhusu ndiyo tunakuja kwa wale waliokwisha kupata nafasi.

Mwisho dogo linahusu ratiba yetu. Kwa maombi ya Serikali, ratiba ya jinsi Wizara zitakavyofuatana, kwa maombi ya Serikali ni kwamba Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa hataweza kuwasilisha makadirio ya Wizara yake kwa siku aliyopangiwa ambayo ni tarehe 17 Julai, 2003 au siku hiyo ndiyo iliyopangwa kwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Kutokalna na shughuli alizopangiwa na Mheshimiwa Rais atakuwa nje ya nchi na anaweza tu kufanya kazi hiyo tarehe 29. Kwa hiyo, badiliko ni kwamba Wizara zitasogea moja moja kwa mtiririko huo huo, Wizara iliyokuwa imepangiwa tarehe 18 Sheria na Mambo ya Katiba sasa itakuja 17, hivyo hivyo tutasogea Wizara moja moja mpaka 29 halafu tutaendelea kama ratiba inavyosema.

Waheslhimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo sasa namwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Athumani Janguo atoe maoni ya Kamati yake. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 81 Kanuni Ndogo ya Kwanza, Kanuni za Bunge za mwaka 2003 naomba kuwasilisha taarifa na maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kuliomba Bunge lako tukufu lipokee na kuijadili. Nataka nikuhakikishie kwamba nusu saa ni nyingi. Nitamaliza katika kipindi hicho. Wajumbe wa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala walioshiriki katika kazi hii ni hawa wafuatao. Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis S. Ali, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko R. M. Lamwai, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Mwanne Ismaily Machemba, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary H.K. Nyerere, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri pamoja na mimi mwenyewe Mwenyekiti. Kamati yetu imehudumiwa na Makatibu Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ernest Zulu. *(Makofi)*

Tarehe 2 Juni, mwaka 2003 Kamati yangu ilikutana Jijini Dar es Salaam kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha wa 2002/2003 na Taarifa ya Makadirio na Mapato na Matumizi kwa mwaka 2003/2004 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Habari na Siasa), ilihudhuriwa pia na Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu(Sera). Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kama yafuatayo. Fungu 25 Waziri Mkuu, Fungu 27 Msajili wa Vyama vya Siasa. Fungu 37 Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 Ofisi ya Spika, Fungu 54 *Radio Tanzania*, Fungu 61 Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Fungu 91 Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya na Fungu 92 Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI.

Utekelezaji wa maoni ya maagizo ya Kamati katika mwaka wa fedha 2002/2003. Katika mwaka 2002/2003 Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo kadhaa. Maagizo yaliyolenga kuboresha utendaji kazi wa Ofisi hii muhimu sana kwa nchi yetu. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu imeyafanyia kazi maeneo karibu yote na hatua kadha za kutekeleza zimeonekana. Pale ambapo Wajumbe walihitaji ufafanuzi, nafurahi kusema kwamba ufafanuzi huo ulitolewa kwa kina. Pamoja na utekelezaji huo, bado Kamati yangu iliona kuna maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi. Hivyo Kamati iliagiza yaendelee kufanyiwa kazi ipasavyo.

Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2002/2003. Kamati yangu ilielezwa kwamba kwa mwaka wa fedha uliopita Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 35,682,928,400/= kwa ajili ya Bajeti ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6,235,419,200/= kwa Bajeti ya Maendeleo. Aidha, kwa mwaka huo wa fedha mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu yalitarajiwa

kukusanya shilingi bilioni 2,475,726,900/=. Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika mwaka 2002/2003. Kamati yangu ilielezwa kwamba katika kipindi cha 2002/2003 Ofisi ya Waziri Mkuu iliendelea kutekeleza jukumu lake kubwa la kuratibu shughuli za Serikali. Pamoja na hayo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake zilifanikiwa kukamilisha mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

Moja, kuratibu misaada ya maafa mbalimbali yaliyotokea nchini ikiwa ni pamoja na kulipa kifuta machozi kwa Wahanga wa ajali ya Treini ya Dodoma na ajali ya kivuko iliyotokea Kilombero. Nashukuru kwamba katika hotuba yake mtoa mada leo ameizungumzia hiyo. Na kwenye maswali ya asubuhi suala hili lilielezwa vizuri sana.

Pili, kukamilisha rasimu ya Sera ya Maafa na kuwasilisha kwa Mamlaka zinazohusika. Tatu, kuandaa rasimu ya mkakati wa kupambana na maafa nchini kwa mwaka 2003/2004 kama ilivyoelezwa tena na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake ya leo. Nne, kuanza kazi ya kujenga minara ya kurushia matangazo ya TVT katika Mikoa ya Arusha, Mwanza na Dodoma. Tano, kuratibu maandalizi ya Sera ya kuwawezesha wazawa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Nafurahi kwamba hayo mawili yote ya TVT na hizo ratiba za kuwashirikisha wazawa yameelezwa kirefu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kazi zilizopangwa kufanywa katika mwaka wa fedha 2003/2004. Kamati yangu ilieleza kwamba miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kufanyika katika kipindi cha 2003/2004 ni kusimamia mapambano ya vita dhidi ya UKIMWI, rushwa na madawa ya kulevya. Kuhamasisha shughuli za maendeleo ya wananchi. Kuboresha huduma za Bunge, kusimamia, kuratibu uhamiaji Makao Makuu Dodoma na kuendelea na matayarisho ya kuanzisha daftari la kudumu la wapiga kura. Maoni na ushauri wa Kamati. Kwa mwaka huu wa fedha Kamati yangu imetoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa. Sehemu kubwa ya ushauri wetu ililenga kuboresha ushauri na maagizo tuliyoyatoa katika mwaka wa fedha uliopita. Na pia kuziba mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kujadili Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka huu. Mpango wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma. Suala la Makao Makuu Dodoma linahitaji kukamilishwa. Kamati yangu imeishauri Serikali iwe na mipango thabiti kufikisha suala hilo ili kuondoa gharama zinazotumika sasa kwa kuwepo na Makao Makuu ya Serikali katika miji miwili. Aidha, kiasi cha fedha cha shilingi 71 milioni kiichotengwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *CDA.*, ili zitumike katika kuboresha miundombinu ya Makao Makuu Dodoma, ni kidogo sana kulingana na ugumu na umuhimu wa kazi yenyewe. Hivyo, Kamati inashauri kuwa mwaka ujao fedha itakayotengwa kwa ajili ya *CDA* iongezwe.

Kamati yangu inashauri Tume ya Uchaguzi iandae mikakati ya kuhakikisha kwamba mpango wa kuanzisha Daftari la kudumu la wapiga kura unatekelezwa kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005. Wadau wote wakiwemo vyama vya siasa washirikishwe kikamilifu. Kamati yangu imeona kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi hazitoshi kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ya kawaida na kuanzisha daftari la wapiga kura. Hata hivyo, maelezo ya Waziri ni kwamba kuna kiasi cha shilingi bilioni 3 kilichotengwa katika fungu la Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi hiyo ya maandalizi ya daftari la wapiga kura. Hivyo, Kamati yangu inashauri fedha hizo zipelekwe katika fungu la Tume ya Uchaguzi, Fungu 61 ili zitumike kama ilivyotarajiwa. Kamati yangu inashauri Sera ya Maafa ikamilishwe mapema iwezekanavyo na uwepo utaratibu wa kutenga fungu maalum katika Bajeti kwa ajili ya maafa yanayoweza kujitokeza badala ya kusubiri hadi maafa yanapotokea ndipo fedha zinaanza kutafutwa. *(Makofi)*

Nashukuru kusema kwamba, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake leo, maoni haya ya Kamati yamezingatiwa. Aidha, Serikali ianze maandalizi mapema ya kukabiliana na janga la njaa linaloikabili nchi yetu kwa mwaka huu kutokana na uhaba wa mvua. Hili pia Waheshimiwa Wabunge wamelisikia kama limeweza kuzingatiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Kamati yangu inashauri kuwa kuwe na utaratibu maalum wa kutathmini na kufuatilia misaada ya fedha inayotolewa na wafadhili kwa mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* yanayoshughulika na masuala ya UKIMWI ili kuona kuwa zinatumika kama ilivyokusudiwa. Aidha, kwa fedha zinazotolewa kwa Halmashauri zetu, Kamati yangu inashauri iwekwe wazi kwamba fedha hizo ziwafikie walengwa badala ya kuishia katika vikao vya viongozi.

Kuhusu Ofisi ya Spika, Kamati yangu inashauri kuwa ujenzi wa Ukumbi Mpya wa Bunge Dodoma, uende sambamba na ukarabati wa Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam na Ofisi ya Zanzibar ili ziwe na hadhi inayotakiwa. Nafurahi kusema kuwa, Kamati ilithibitishiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba matengenezo hayo yameanza. Kwa upande wa suala la michezo kwa Waheshimiwa Wabunge, Kamati inashauri litengwe fungu maalum badala ya kutegemea misaada ya wafadhili.

Redio Tanzania Dar es Salaam, Kamati yangu inashangazwa na kitendo cha vituo vya redio karibu vyote hapa nchini kutoa taarifa zao za habari kwa wakati mmoja. Kamati yangu inashauri kuwa, ili kuwapa wasikilizaji haki yao ya kupata taarifa muhimu, Serikali iunde utaratibu utakaoviwezesha vyombo hivyo vitoe taarifa hizo kwa nyakati tofauti. *(Makofi)*

Kuhusu majengo ya TVT, hayatoshi na pia yapo majengo ambayo ujenzi wake haujakamilika ingawa ulianza kwenye miaka mapema ya 1990 na yamesahauliwa. Licha ya umuhimu wa kazi inayofanyika Kamati yangu inashauri kuwa TVT ipewe kasma yake kikamilifu itakayoiwezesha kukamilisha ujenzi wa majengo yake na ili iweze kujiendesha. Wakati utaratibu huo unaandaliwa ni vema kituo hicho kipatiwe msaada na Serikali utakaoiwezesha kupata vifaa na nyenzo za kisasa. Pia maslahi ya watumishi yaboreshwe.

Mheshimiwa Spika, Utendaji Kazi wa Makatibu Tarafa, Kamati yangu imeelezwa kwamba Makatibu Tarafa wote wa Tanzania Bara wamepatiwa pikipiki kama moja ya nyenzo za kufanyia kazi. Hata hivyo, suala hili halikufanyika kwa tarafa zote.

Hivyo, Kamati inashauri jitihada ziendelee hadi tarafa zote zifikiwe. Jitihada hizo zihusishe mafunzo kwa watendaji hao ili kuboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, Tofauti ya Mishahara Serikalini, Kamati hairidhishwi na matabaka yanayojitokeza nchini kutokana na tofauti ya mishahara ya watumishi wa Serikali wenye viwango vya taaluma vinavyolingana kwa kigezo cha unyeti wa Taasisi. Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayoratibu shughuli za Serikali, Kamati yangu inashauri iandaliwe sera maalum juu ya suala hili ili kuwatendea haki watumishi wote na kuwahamasisha wafanye kazi kwa bidii zao zote.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa mwaka 2003/2004. Baada ya majadiliano Kamati yangu iliombwa iidhinishe Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mafungu yake yote kiasi cha shilingi bilioni 64,340,671,200/=. Kati ya hizo shilingi bilioni 20,094,794,900/= zikiwa ni kwa mpango wa maendeleo na shilingi bilioni 44,245,876,300/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ombi hili Kamati imeliridhia na inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wake, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa William V. Lukuvi pamoja na timu ya wataalam wao, kwa ushirikiano wao walioutoa wakati wakikutana na Kamati yangu. Aidha, nawashukuru pia kwa maandalizi waliyoyafanya na kufanikisha ziara ya Kamati hii katika Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa namna ya kipekee kabisa, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala kama nilivyowataja hapo mwanzo, kwa ushirikiano wao na michango yao muhimu katika kipindi chote cha Vikao vya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge ikiongozwa na Ndugu Kipenka M. Mussa. Shukrani zaidi ziwaendee Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ernest Zulu, kwa kazi yao nzuri ya kuihudumia Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda kuiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 43 (b) na (c) toleo la 2003, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa kudra zake zilizo nyingi na kwa ridhaa ya ndugu zangu na rafiki zangu wa Kambi ya Upinzani, nimesimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Bajeti yake nikiwa kama Waziri Mkuu Kivuli, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Nawashukuru sana walioniletea salamu mbalimbali za pongezi na nawaahidi utendaji ulio wa kutumainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa *CUF* na wapiga kura wa Majimbo yao ambao wameandika historia mpya ya kisiasa ndani ya nchi yetu ya kuonyesha dhahiri kwamba "mtafuta haki hachoki!". Na zaidi niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mkanyageni, kwa kumchagua Mheshimiwa Bakari Shamis Faki wa *CUF* kurithi kiti cha Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Mohamed A. Shein toka CCM. Ushindi wa Chama cha *CUF* ndani ya kiti hiki na hasa ikiwa ni baada ya kusainiwa muafaka na kuundwa Tume ya Uchaguzi yenye kuvishirikisha vyama vingine, ni ushindi unaotupa changamoto kubwa kwamba "kulikuwa na nini, kuna nini na kunatakiwa kuwa na nini katika uchaguzi wa mwaka 2005." *(Makofi)*

Kazi kubwa inayotukabili sisi wote ni kufanya kazi kwa pamoja bila hila, fitina na kinyongo, tukiwa na dhamira thabiti ya kumtumikia Mtanzania na kumwondolea maisha yaliyo duni.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi waliochaguliwa kutoka Majimbo manne na kujiunga katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Fredrick T. Sumaye, kwa hotuba yake aliyoiandaa yeye pamoja na timu yake ya wataalamu wakiongozwa na Waheshimiwa Mawaziri katika Ofisi yake na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo. Na kwa kuwa sikupata fursa ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na ile ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nao pia naomba niwapongeze kwa kazi kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupongezana kwa Bajeti nzuri iliyoandaliwa ni suala moja na kutekelezeka kwa Bajeti hiyo ni suala lingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Serikali, anawajibika kuhakikisha Bajeti inatekelezeka na tija inaonekana. Utamaduni, desturi na mazoea ya Mwafrika, kupongeza na kushukuru ni jadi na ni njia mojawapo ya kuonyesha ustaarabu. Lakini kwa dunia tunayokwenda nayo ya utandawazi ambayo kwa kiasi kikubwa haimwonei haya wala huruma yule anayepongeza au kushukuru wakati hana chochote, inatulazimu tujiangalie, tujichunguze, tujifanyie upembuzi ulio yakinifu na kuangalia iwapo kasi yetu ya kukua kwa uchumi ndani ya maisha na haiba ya watu wetu ni ya kusuasua; sababu hasa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuangalia nyuma tulikotoka ni jambo la msingi kwani kunaweza kutusaidia kujua tulipo na kule tunakoelekea. Mwaka 1966 Juni wakati Waziri wa Fedha alipomaliza kuwasilisha makadirio ya mwaka 1966/67 ya Shs. 486,000,000/=, Mbunge wa Tabora East, Bwana Kaombwe alisema katika hotuba yake. "Mheshimiwa Bwana Spika kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niwe mtangulizi wa kuweza kumpongeza Waziri wa Fedha kututolea hotuba yake nzuri sana ndefu na yenye kukata tumbo kwa sababu imetaja au inataja mambo ya pesa zinazotakiwa nchi hii izipate".

Na katika hotuba ya Mheshimiwa Jamal Ramadhan Nasile, Mbunge wa Mjini Unguja, akichangia katika hotuba ya makadirio ya mwaka 1978/79 yenye jumla ya Shs. bilioni 6.7 alisema: "Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu kwa Ndugu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hakika hotuba ya Bajeti ya ndugu Waziri wa Fedha na Mipango ilikuwa nzuri sana na iliyoandaliwa kwa utaalam. Si hivyo tu kwa utaalam, lakini kitu kikubwa kilichonivutia mie ni kwamba ile hotuba yenyewe ina hisia ya wananchi" na akapigiwa makofi sana.

Hivyo hivyo ukisoma Bajeti zote hata za 1991/92, 1992/93, 1994/95 na kuendelea hadi mwaka jana zinapewa pongezi na kuwatia matumaini Waheshimiwa walio wengi kwa asilimia mia kwa mia. Baada ya hapo lugha inayojitokeza na kujirudia rudia ndani ya Bajeti zote tangu mwaka 1964 hadi leo mwaka 2003 ni Bajeti Tegemezi, vyanzo vya ndani na nje vya kutupatia mapato kutotosheleza matumizi na mipango ya Serikali inayokuwa imepangwa. Pamoja na pongezi hizo za hotuba nzuri sana Watanzania wameendelea kuwa maskini mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia kwamba Bunge hili linawajibika kumpitishia Mheshimiwa Waziri Mkuu Mipango ya Bajeti inayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kama ifuatavyo: Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali, masuala ya Bunge na siasa, vyombo vya habari nchini, maafa, UKIMWI, ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma na uchapaji wa nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu hayo ni makubwa na ndio haswa utawala wenyewe wa nchi. Kama Serikali nzima haikujipanga vizuri kuanzia kwa Mheshimiwa Rais hadi Afisa Mtendaji wa Kijiji katika kuyasimamia kwa kutumia Bajeti iliyotayarishwa vizuri, kazi yote inakuwa ni bure.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Bunge la Tanzania tarehe 20 Juni, 1966 wakati huo wote tukiwa tunaimba *TANU* ya jenga nchi; hakuna CCM, *CUF*, CHADEMA, *TLP* wala *UDP* wakati, Bwana Migeyo Mbunge wa Kuteuliwa akichangia hotuba ya Bajeti alisema: “Bwana Spika, ninayoyataja ni mambo yanayowaumiza wakulima na wanalalamika sana ila hawafanikiwi tu. Sasa Bwana Spika, kusema kweli utunzaji wa fedha ni mbaya. Fedha zinapatikana nyingi ingawa tunasema sisi ni maskini ila utumiaji umekuwa mbaya. Wale Watumishi waliopewa kutenda kazi za madaraka wanayotenda sivyo ilivyo sawa. Watumiavyo fedha ni ovyo wala si kwa njia nzuri. Akiambiwa fulani nenda mahali fulani ukafanye kazi, basi yeye anakwenda huko na anajifanyia kama anavyotaka. Ule utumiaji wa fedha ni mbaya sana. Serikali inavyotumia fedha haiwaridhishi wananchi hata kidogo, lakini na mimi naongezea kusema kwamba zinatumika vibaya hivi hivi”. Hiyo ilikuwa mwaka 1966. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1966/67 Bajeti ilikuwa Shs. 480,000,000/=, mwaka 1978/79 Bajeti ilikuwa shilingi bilioni 6.9, mwaka 2001/2002 Bajeti ilikuwa trillion 1.7, mwaka 2002/2003 Bajeti ilikuwa trillion 2.2 na mwaka huu 2003/2004 Bajeti ni trillion 2.6.

Mheshimiwa Spika, miaka hiyo yote majibu bado ni yale yale ya kutotekelezeka mambo mengi na hasa la kuondosha umaskini, ujinga na maradhi, majibu ni Bajeti finyu, Bajeti ni tegemezi, Bajeti haitoshi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakuwa hatujamsaidia sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Bajeti yake aliyoileta iwapo tutakuwa hatujaondosha “unyanyapaa wa mipango ya Bajeti isiyotekelezeka”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hali ya Ulinzi na Usalama. Japo suala la Ulinzi na Usalama litajadiliwa wakati wa Bajeti ya Wizara husika, Kambi ya Upinzani inadhani suala la Ulinzi na Usalama sasa ni suala la sera na hivyo ni la Serikali nzima, ambayo uratibu wake uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Spika, kwa siku za hivi karibuni, jamii ya Watanzania imetishwa na matukio kadhaa ya ujambazi na hasa ujambazi ambao umechukua sura mpya kabisa kwa kuwahusisha wageni.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani imeshitushwa na kiwango cha ujambazi, aina ya ujambazi na maeneo yanayokumbwa na ujambazi huo. Kambi ya Upinzani pia imeshituka sana kuona jinsi Jeshi la Polisi lilivyocharuka baada ya kuona wenzao watatu wameuliwa katika ujambazi huo. Tunapenda kutoa pole kwa familia za marehemu Askari wetu waliouwawa wakiwa kazini. Lakini pamoja na hayo wakati Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla walipokuwa wakipiga kelele wakitaka hatua zaidi zichukuliwe, imechukua muda mrefu polisi kuchukua hatua. Hatua za haraka zimefanyika baada ya wao wenyewe kuuliwa na majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Serikali na vyombo vyake visiwe na tabia ya kupuuzia malalamiko na mapendekezo yoyote yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge na jamii kwa nia njema. Hatua za haraka zichukuliwe mara moja kwani wote tuna nia moja, kumhudumia

Mtanzania na kujenga mahali pazuri pa kuishi sisi sote. Kambi ya Upinzani haioni kabisa msingi wa malumbano yaliyotokea mwaka jana kati ya Waheshimiwa Wabunge na Jeshi la Polisi, wakati yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge yamethibitishwa kwa matendo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa tatizo la ujambazi halina majibu ya haraka haraka, kama vile kusema kuwa ni wakimbizi au silaha zinaingizwa nchini na wakimbizi. Wote tunafahamu jinsi Tanzania ilivyokuwa mstari wa mbele katika kupokea wakimbizi tangu enzi za Serikali ya Awamu ya Kwanza, lakini hatukuwahi kuona kiwango kikubwa cha ujambazi kama sasa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ichukue hatua ya haraka kutafuta sababu za msingi zinazosababisha ujambazi huo na kuishirikisha jamii katika kutafuta sababu hizo na ikiwa ni pamoja na hatua ya mapendekezo ya hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, Serikali isipuuzie maoni yaliyoko miongoni mwa wananchi wengi kuwa, miongoni mwa sababu za msingi ni umaskini uliokithiri nchini, kujengeka kwa matabaka ya wazi kati ya walionacho na wasio nacho katika jamii yetu. Tunaitaka Serikali itazame sababu za kisera kuliko kuwa na majibu ya mkato wakati tunaona jinsi wananchi wanavyoona usalama wao na wa mali zao ukiyoyoma kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali kuchukua hatua ya makusudi kabisa kulisafisha Jeshi la Polisi kwa kuwachukulia hatua thabiti Polisi wachache wanaoshirikiana na wahalifu kwa njia yoyote ile ikiwa ni pamoja na kutoa siri ya taarifa ya uhalifu, kuwaachia wahalifu wanaporipotiwa na raia wema na hata wanaosemekana kuwabambikizia wananchi makosa.

Jeshi la Polisi inabidi lifanye kazi kwa umakini na umahiri unaotakiwa, Sheria na kwa kadri ya mafunzo yao. Matukio kama yaliyotokea katika Kituo cha Polisi Mlimba ambapo wananchi sita (6) walikufa mikononi mwa Polisi na isitoshe kinyume na utamaduni wa Kitanzania, walizikwa wote katika kaburi moja Ifakara bila sababu ya msingi. Hadi leo hatujasikia hatua iliyochukuliwa kwa wahusika.

Vivyo hivyo Arusha na sasa Mbarali ambapo watu 19 wamekufa mikononi mwa Polisi na Mwanza vijana sita (6) waliouwawa wakitoka kwenye sherehe. Haya ni matukio ambayo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iyatolee tamko rasmi na kulieleza Bunge hili ni nani alisababisha maafa hayo, kwa sababu zipi za msingi na wahusika wamechukuliwa hatua gani. Kambi ya Upinzani ingelipenda hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama mratibu wa shughuli za Serikali alieleze Bunge hili. Kama ilivyotokea Pemba, Unguja, Mwanza na Mbarali vyombo vya Serikali vimeonekana kujikanganya na kutoa majibu ya kupingana wakati vinashindana kila chombo kuunda Tume ya Uchunguzi, Tume ambazo majibu yake yaliishia kwenye makabrasha. Hali hii haiwezi tena kuachiwa ikaendelea bila hatua kuchukuliwa kwa wahusika, familia za walioathirika zinapaswa kulipwa fidia na Serikali, iwapo itathibitika kulikuwa na uzembe wa chombo cha dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi. Mwaka jana katika hotuba yake ya Bajeti Mheshimiwa Waziri Mkuu aliliambia Bunge lako Tukufu kuwa “mwenendo wa ukuaji wa asilimia 4.9 ya uchumi kwa mwaka 2002, ni dalili nzuri ya kuondoa kabisa umaskini nchini ifikapo mwaka 2020”. Kufikia mwaka 2020 imebakia takriban miaka 17 tu. Kuanzia mwaka 2000 hadi leo ni miaka mitatu na hakuna dalili ya hicho kinachoitwa “kukua kwa uchumi” kilichoteremka katika mfuko wa mwananchi. Hali ya mwananchi wa kawaida imebakia pale pale na pengine kushuka chini zaidi. Watu waliokuwa na kazi leo hawana kazi na hivyo kutokuwa na uhakika wa maisha yao. Watu walioweza kununua kitu dukani miaka 20 iliyopita wakati dola moja ya Marekani ilipokuwa sawa na Sh. 17 leo hawawezi tena kumudu kununua vitu walivyoweza kununua miaka 20 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili linalolalamikiwa na wananchi ni kuhusu “kuchelewa sana kuchukua hatua. Mara nyingi Serikali haiwasikilizi Waheshimiwa Wabunge iwe kwenye majibu ya maswali katika Kipindi cha Maswali au wanaambiwa wao ni Madiwani wayamalize katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule nyuma wananchi walijua kuwa Chama ndicho kilichoshika hatamu na maamuzi mengi yalifanyika kwa njia ya Serikali na Bunge, walijikuta kutekeleza maagizo ya Chama. Wananchi wamejikuta kuachwa njia panda na Serikali hii imechukua nafasi ya Chama kufanya maamuzi

makubwa, maamuzi ambayo yamekuwa siri kubwa mpaka pale panapotokea migogoro. Hii imesababisha manung'uniko na malalamiko ya chini kwa chini na vile vile yanaanza kujitokeza kwa njia ya migomo, maandamano na wako wengi tu ambao wanashindwa kutokana na utamaduni tuliojijengea, kusema na kutoa maoni yao kwa maneno au kwa matendo.

Mheshimiwa Spika, katika maazimio mazito ya Kisera, kama uuzaji wa Nyumba za Serikali, si busara jambo kama hilo likasikika mitaani kabla ya wananchi kujulishwa rasmi. Uuzaji huo umezua maneno mengi mitaani na hata kwenye vyombo vya habari. Jambo kubwa kama hilo, kuuza nyumba zisizopungua elfu tatu (3,000) zilizojengwa kwa kodi za wananchi ziwe za zamani au mpya si suala la Serikali kuamua peke yake bila kupata mustakabali wa Kitaifa. Isitoshe, zingeliuzwa kwa Tenda za Wazi hasa baada ya kupitisha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 na Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kuuziana kinyemela nyumba hizo ndiko kunakoamsha hisia nyingi miongoni mwa Watanzania. Tendo hilo linafuta dhana nzima ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya "zama za ukweli na uwazi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wangetaka kujua hasa ni kina nani wameuziwa nyumba hizo na kwa bei gani? Uwazi na ukweli ndiyo unaojenga heshima ya Serikali miongoni mwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeshitushwa na matumizi ya mara kwa mara eti tuna ridhaa ya Watanzania. Ni kweli kuwa Chama cha Mapinduzi kilishinda uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama wakati wa uchaguzi, ni malengo mapana sana ambayo kimsingi hayaonyeshi katika utekelezaji ni hatua zipi zitachukuliwa. Wala wananchi si wataalam wa kufafanua vipengele vilivyoko katika Ilani za Vyama mbalimbali. Kimsingi, ndiyo maana Serikali inawajibika kupitia Bungeni kila mwaka ili kuweka mpango wake wa utekelezaji wa sera na Ilani zake. Ilani na sera siyo blanketi kubwa ambayo inatumika kuwafunika wananchi na kuwaambia kuwa sasa wao pamoja na Waheshimiwa Wabunge wao walale wakati Serikali inafanya maamuzi yote makubwa kwa niaba yao kwa kipindi chote cha miaka mitano. Matokeo ya dhana hiyo yameanza kujitokeza wakati wananchi hawana tatizo sana na sera ya ubinafsishaji, wana tatizo kubwa la utekelezaji wa sera hiyo. Serikali imejichukulia majukumu makubwa kwa kudai ni sera na Ilani zilizopitishwa na wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi na wananchi kwa kuonyesha kuwa hawakubaliani na utekelezaji huo na kuwa siyo waliyopigia kura; na kwa kuwa hawana mahala pengine pa kujadiliana, wanajitokeza kwa njia ya migomo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliyo makini itajiuliza ni kwa nini kwa muda huu mfupi Watanzania wameanza mtindo wa migomo, mtindo wa kuwafungia viongozi ndani kama wanavyofanya *TES* kwa wiki tatu sasa. Tumeshuhudia juzi wafanyakazi wa *TANESCO* walivyolazimishwa kwa kutumia Askari, kupokea utawala mpya. Haya siyo makubaliano kati ya wananchi na Serikali waliyoichagua. Serikali ina Idara nyingi na vyombo vingi. Kwa muda mrefu sasa inaelekea kuwa kila Wizara ilikuwa inafanya mambo yake. Hii imejionyesha kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, matukio ya hivi karibuni ya watu binafsi kuandikisha magari ya Serikali kwa namba za kiraia au kwa majina yao binafsi kama alivyothibitisha Mheshimiwa Rais, inatia wasiwasi mkubwa. Kambi ya Upinzani tunashangaa kuwa iliwekezakanaje kwa jambo hili kutendeka wakati Serikali ni Msimamizi Mkuu wa mali zote za Serikali kwa niaba ya wananchi. Je, Serikali ilikuwa wapi na Serikali inaweza kulieleza Bunge hili kuwa kwa mtindo huo ni magari mangapi tayari yalikwisha kuuzwa kinyemela na wahusika?

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani inadhani licha ya Mheshimiwa Rais kutoa agizo la magari hayo kurudishwa na magari mengi yamerudishwa na kusajiliwa upya, kulikuwa na uzembe mkubwa kwa upande wa watu waliopewa majukumu ya kusimamia mali za umma. Ni kwa sababu hiyo, tuliwakabidhi watu Mashirika ya Umma wakatuingiza kwenye hasara ya mabilioni na hatimaye tumepaswa kuyauza kwa bei ya kutupwa. *(Makofi)*

Ni vema tukajenga sasa utamaduni wa mtu aliyezembea kusimamia Wizara au Idara iliyokuwa chini yake awajibike na kujiuzulu mara moja. Pamoja na kuwa si rahisi kukokotoa gharama ya zoezi la kusaka magari hayo, lakini bila shaka ni gharama kubwa aidha kwa maana ya fedha au kwa maana ya muda wa maaskari uliotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kutoa mapendekezo yafuatayo kutokana na hayo tuliyosema hapo juu:

Kwanza, ili kujenga Taifa imara na lenye mshikamano, ni vema Serikali ikaondoa usiri katika mambo ambayo hayako katika Sheria ya usalama wa Taifa na yanayohusu maslahi ya Taifa. Pili, siku za hivi karibuni tumewaona Watanzania wakianza kumkumbuka Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, jambo ambalo linaashiria kuwa Watanzania wameona tofauti kati ya mambo waliyoyazoea huko nyuma na sasa wanaona mambo yanabadilika. Historia ya Taifa si mali ya mtu mmoja na hivyo Serikali isione kuwa ina ukiritimba wa historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Siasa Nchini. Tanzania sasa ina miaka 10 ya Siasa ya Vyama vingi. Ni kweli pia Ofisi ya Msajili wa Vyama angalau tangu ameingia Msajili wa sasa Bwana John Tendwa, kumekuwa na ushirikiano mkubwa kati ya Ofisi yake na Vyama vya Siasa japo vyama vingine vimefutiwa usajili. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali kukaa chini na viongozi wa vyama vya siasa kupata maoni yao juu ya mustakabali wa nchi hii. Pamoja na hali hiyo Kambi ya Upinzani inayo maoni yafuatayo:-

Waziri Mkuu ndiye kiungo kati ya Serikali na Vyama vya Siasa. Wakati bosi wake Mheshimiwa Rais ameshachukua jukumu la kukutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa, Kambi ya Upinzani inashangaa ni kwa nini Mheshimiwa Waziri Mkuu hadi leo hajachukua hatua zozote za kukutana na Viongozi wa Vyama ili kubadilishana mawazo na kuelewa malalamiko yao. Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye mlezi wa vyama vyote na Ofisi ya Msajili iko chini ya Ofisi yake, yeye anaelekea kuilea CCM tu. Ni vyema basi jukumu hili litoke chini ya Ofisi yake na Ofisi ya Msajili iwe huru. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani haikubaliani na tabia ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama ya kuvikarisha roho juu vyama ambavyo vimekuwepo kwa muda mrefu na kushiriki chaguzi zote mbili eti havijatimiza masharti ya kusajiliwa. Hali hii ni kuvifanya vyama hivi vijione kama vile vipo vipo kwa huruma ya Serikali na matokeo yake ni kuviathiri kiutendaji. *(Makofi)*

Ni vizuri na ninafikiri ni wakati muafaka kwa Serikali kutekeleza kwa vitendo vipengele 16 na 17 vya muafaka baina ya *CUF* na CCM vinavyosema:

Kipengele Na. 16 kinasema: “Vyama vyetu viwili vimeridhika kuwa mazungumzo yaliyofanyika baina yake na hatimaye kuwezesha kufikiwa kwa makubaliano haya ni kielelezo thabiti cha uwezo wa Watanzania wa kukabiliana na migogoro inayojitokeza nchini na kuipatia ufumbuzi muafaka. Vyama hivi viwili vinahimiza na kusisitiza kuendelea na mpango wa kuleta maridhiano na maelewano ya Kitaifa kwa msingi wa mazungumzo na kujenga imani miongoni mwa vyama vya siasa hapa nchini.” *(Makofi)*

Na kifungu Na. 17 kinasema: “Ili kufanikisha azma hii ya kuwa na mashirikiano ya kudumu baina ya viongozi wa vyama vya siasa, Vyama vya CCM na *CUF* vimekubaliana kuwa ipo haja ya kuwa na Kamati ya pamoja ya mashirikiano ya vyama vya siasa hapa nchini ambayo itakuwa ni ya kudumu na itakayojumuisha viongozi wa Kitaifa wa vyama vyote vya siasa vilivyopo nchini katika mfumo ambao utaamuliwa na vyama husika baadaye. Kamati hii itakuwa ndiyo jukwaa la kubadilisha mawazo na kujenga maelewano juu ya masuala mazito yanayoihusu nchi yetu”. Mtu muungwana ni yule anayetimiza makubaliano na miadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Upinzani vimekuwa vikishutumiwa na kusemwa na Viongozi wa Chama Tawala kwamba mambo yake ni ya kuishia Ukumbi wa Maelezo na haviendi kwa wananchi huko Vijijini. Viongozi na Waheshimiwa Wabunge wa baadhi ya vyama hivyo wameanza kwenda huko wanakoelekezwa kwenda, matokeo yake imekuwa nongwa na kununiana. Hivi ni siasa zipi na za mtindo upi ambazo vyama vyetu vinatakiwa vicheze?

Mbona viongozi wa Chama Tawala na wa Serikali hasa viongozi wakuu wakienda kwenye Majimbo ya Upinzani wanacheza mchezo usiokubalika wa kuwavuruga wapiga kura wetu na wala hatulalamiki? Na hivi sasa tunavyoongea Mheshimiwa Msome yuko Bukoba Mjini anafanya vitu vyake.

Sasa tunafikiri wakati umefika kwa Msajili wa Vyama pamoja na Tume ya Uchaguzi, kukaa na wadau wote zikatengenezwa *code of conduct* za kuendesha shughuli za kisiasa zinazokubalika kwa wadau wote.

Ofisi ya Waziri Mkuu imekabidhiwa jukumu la kuratibu shughuli za kudhibiti UKIMWI. Pamoja na kuanzishwa kwa *TACAIDS*, UKIMWI bado unasambaa kwa kasi kubwa. Kambi ya Upinzani ingetaka kujua iwapo Serikali ina mpango wowote wa kuanzisha kituo maalum cha utafiti na tiba ya UKIMWI na kutafuta misaada katika Taasisi za Kimataifa na *NGOs* kama ile ya *Bill Gates Foundation* ambayo imeisaidia Botswana dola za Kimarekani milioni 100 kupambana na UKIMWI. Rais Bush wa Marekani ametangaza Mfuko maalum wa dola za Kimarekani bilioni 15 kupambana na UKIMWI Afrika na Carribean. Je, Serikali imefuatilia kuwepo kwa Mfuko huu na kujiandaa kutimiza masharti yake ili Tanzania iweze kunufaika na kupata msaada mkubwa toka Marekani kuweza kupambana na UKIMWI? Na iwapo imefuatilia Tanzania itanufaika kwa kiasi gani na katika huduma zipi muhimu?

Mheshimiwa Spika, Kilimo na Tahadhari ya Njaa. Kambi ya Upinzani ingetaka kujua Serikali imechukua hatua gani kununua chakula cha kutosha mwaka huu kwani Taifa letu linakabiliwa na balaa la njaa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti haionyeshi fedha zilizopangwa kushughulikia tatizo la njaa. Shilingi bilioni 2.2 zimetengwa kununulia chakula cha hifadhi, ikiwa kilo moja ya mahindi itagharimu Shs.100/= kuinunua, kuisafirisha na kuihifadhi, fungu hili litanunua kama tani 22,000 tu. Fedha zilizotengwa kwa tahadhari, zitatumiwa kuagizia mahindi kwa wastani wa dola 200 kwa tani, basi Serikali itaweza kuagiza tani 43,500. Miaka ambayo tumekuwa na upungufu mkubwa wa chakula ni hasa mwaka 1974, 1980, 1984 na 1998, tuliagiza mahindi toka nje wastani wa tani 250,000. Bajeti haikutenga fedha za kugawa chakula bure kwa njia ya msaada kwani kama tunavyojua waathirika huwa hawana pesa za kununulia chakula wakati wa maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali isicheze na njaa, matumbo yenye njaa hayatulii majumbani. Taifa letu linaweza kuingia katika janga kubwa iwapo hatukujiandaa. Pamoja na Bajeti safari hii kukipa kilimo nafasi kubwa ya kuzungumziwa, bado Kambi ya Upinzani inaona kwamba suala la kilimo linazungumziwa kijuujuu. Tunazungumzia mbolea, tunazungumzia masoko ya nje, imezungumzia kuchagua mazao mawili, imezungumzia mazao ya chakula na biashara, kuwekewa mkazo kwa ajili ya ku-*export* na pia tumezungumzia kupeleka fedha Ma - wilayani.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo halihitaji lugha ya jumla jumla, inatulazimu kujikita na kuangalia huko nyuma tulikotoka. Akina Mheshimiwa Edward Barongo, Mheshimiwa Mzindakaya akiwa Morogoro na kadhalika walifanyafanyaje maeneo waliyoyaongoza wakati huo yakazalisha mahindi kwa wingi. Watu hawa bado wako hai tuwaite na kuwauliza. Vikao vingi vya kutokanisha mihutasari, kuchambua yatokanayo, kupata muafaka wa vikao, kusubiri *quorum* ya wajumbe, semina, warsha, kongamano hatutegemei kwamba zitabadili sura ya kilimo chetu miaka mia moja ijayo. Serikali inabidi na inalazimika kuunganisha jitihada za kiutafiti zinazofanywa na watalaam wetu katika taasisi mbali mbali, utashi wa soko la nje na la ndani, wakulima wadogo na wakubwa kule vijijini waliko, uboreshaji miundo mbinu na zaidi ya yote dhamira ya kweli toka kwa viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuhamia Makao Makuu Dodoma, Kambi ya Upinzani imefurahi sana kuona kwamba angalau kushindwa kutekelezeka kwa sera na mpango mzima wa Serikali kuhamia Dodoma kunaanza kuzungumzika ndani ya Bunge na Kamati zake. Hii ni ishara nzuri kwa Serikali ya CCM ya kuanza kupokea na kuukubali ukweli unaotolewa na Upinzani sawa na lile suala la kufuta Kodi ya Kichwa ambayo katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mimi mwenyewe nililipigia kelele na kumwomba Waziri alifute mara moja na mashahidi wakiwa Ma-*RC* ambao wamekaa hapo juu lakini Waziri alisema kwamba sio sera ya CCM. Tunashukuru Serikali imesikia. Sasa na suala hili la Dodoma, tunafikiri ni kuendelea kuwabebesha mzigo wa bure walipa kodi. Waziri Mkuu amekuwa akitoa ahadi za kuhamia Dodoma kila mwaka na mara nyingi tumemwona Dar es Salaam. Makazi ya Rais huko Chamwino wala hakuna anayeyagusia tena badala yake tunaendelea kutenda fedha za kuimarisha Ikulu bilioni 2.4.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhamia Dodoma limekuwa la muda mrefu, tunafikiri ni wakati muafaka kutokana na hali halisi tukubali kugeuka jiwe. Kambi ya Upinzani inaamini wana CCM kupitia

Wabunge wao wenye mtizamo mpya wa kimaendeleo wataweka msukumo wa kuibadili Sera hiyo ambayo imeshindikana kutekelezeka na hatimaye tusiendelee kuonekana wote ni vichekesho vinginevyo ufanyike uamuzi wa uhakika na wa kisheria utakaoifanya Sera hii ya CCM itekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uchaguzi ulio huru na wa haki, Tanzania inahitaji kuwa na daftari la kudumu la wapiga kura na suala hili limezungumzwa katika Katiba yetu. Shughuli za kutayarisha uchaguzi na angalau daftari la kuanzia kwa ajili ya uchaguzi wa marudio wa Majimbo 17 huko Pemba yenye wapiga kura 103,000, kumegharimu shilingi milioni 900, *Donor Community* walichangia 600 milioni na Serikali milioni 300, Tume ya uchaguzi Zanzibar imetumia miezi minne katika kazi hiyo na shughuli nyingine hazijakamilika. Kwa bajeti ya bilioni 1.8 kwa nchi nzima tena uchaguzi wenyewe ni wa mwaka 2005, *we must be joking*. Ni bora tuwekane wazi mapema yaishe. Mwaka 2005 nchi inaweza kuingia katika matatizo makubwa kama hapatakuwa na daftari la kudumu la wapiga kura na inawezekana uchaguzi usifanyike kabisa. Kambi ya Upinzani inatoa wito kwa Serikali iheshimu Katiba na sheria na pesa za kutosha kuanzisha daftari la kudumu zitengwe kwa ajili ya kazi hiyo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetengwa shilingi bilioni tano kuwa mishahara ya watendaji wa vijiji. Hili ni jambo zuri, Kambi ya Upinzani inalipongeza na linaweza kupunguza kero ya wananchi ya kutolewa michuzi na watendaji wa vijiji. Ni muhimu watendaji wa vijiji na watendaji wa kata waajiriwe kwa ujuzi na uadilifu wao badala ya kuangalia ukada wa Chama Tawala au fadhila kwa watu wenye nyadhifa fulani. Serikali imeona umuhimu wa kulipa *VEOs* nafikiri wakati muafaka umefika wa kuanza pia kuangalia Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa ambao wanafanya kazi kubwa *(Makofi)*

Nimalizie hotuba yangu kwa kuipongeza Serikali kwa kukubali bila kinyongo hoja ya kuifuta Kodi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kwa niaba ya Upinzani, naomba kuwasilisha na tunataka majibu ya uhakika na ya kutosheleza, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niwe msemaji wa kwanza katika hoja hii nzuri ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nataka nitumie nafasi hii awali kabisa kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu asilimia mia kwa mia. Aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake pamoja na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri sana ya hotuba hii ambayo imejumuisha maeneo mengi sana. Mengine itabidi tuyazungumzie katika Wizara husika ili tusipoteze muda wetu kuzungumzia yale ambayo nadhani undani wake tutaingia katika Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwakaribisha Wakuu wetu wa Mikoa kuja kusikiliza hotuba yake. Nasema hivyo kwa sababu mara nyingi tumekuwa tukizungumza mambo ya maendeleo ya Mikoa bila wao kuwepo. Zamani ulikuwa ni utaratibu Wakuu wa Mikoa walikuwa ni sehemu ya Bunge lakini tangu tubadilishe sheria yetu wenzetu wamekuwa hawaruhusiwi kuingia ndani ya Bunge lakini utaratibu wa kuwakaribisha ili wasikie nini Wabunge wao wanazungumza kuhusu maendeleo ni mwanzo mzuri sana ambao utasaidia kujenga umoja miongoni wetu. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maandalizi mazuri ya maeneo ambayo mengine nitayagusia tu haraka haraka kwa sababu muda hautoshi lakini mengine ni yale ambayo hata Waziri wa Fedha aliyazungumzia kwa ufupi sana kuhusiana na suala zima la kuondoa kero za wananchi na hasa Kodi ya maendeleo. *(Makofi)*

Napenda kuwaambia wenzangu upande wa Upinzani, katika maagizo ya CCM tulisema kila wakati uchumi wetu utakavyokuwa unaboreka tutaondoa kero za wananchi. Hatua ya kwanza tulianza na mambo ya elimu wote ni mashahidi, tumeingia Kodi ya Maendeleo wote ni mashahidi mtashangaa mwaka kesho hata uchangiaji wa Hospitali si ajabu tukaufuta. Ni jitihada za CCM kuhakikisha kero zinapungua awamu kwa awamu kadri uchumi unavyokua. Nasema hilo kwa sababu watu wanadhani ni ajenda zao, sio kweli.

Kazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kubwa sana na bahati nzuri nilishawahi kukaa katika Ofisi ile. Ni kazi ambayo hulali usiku na mchana katika kuratibu shughuli na matatizo ya wananchi. Hivyo moja ambalo nataka kusema wazi ni kwamba katika kipindi chake, napenda kumpongeza kwa sababu pamoja na matatizo aliyonayo amejitahidi, nasema hivyo kwa sababu najua. Kweli kama binadamu tuna udhaifu wetu lakini tuangalie pia na mazuri ambayo mwenzetu anayoyafanya. Tutaendelea kumpa kila msaada afanye kazi yake vizuri. Baada ya kusema hivyo, napenda nizungumzie mambo manne haraka haraka. Kwanza, ni suala zima la hali ya siasa. Hali ya siasa nchini sio mbaya kwa wastani lakini hali ya matokeo ya uchaguzi ulivyokuwa Zanzibar sikufurahishwa nayo. Mheshimiwa Waziri Mkuu itabidi kweli tulikalie kwa sababu dalili hii sio nzuri hata kidogo na dalili hiyo tusipoanza kuiziba mapema mbele ya safari tutakuwa na matatizo. Nitatumia nafasi hii wakati nitakapozungumza, nikipewa nafasi hasa tukianza kuchangia katika hoja ya Makamu wa Rais kwa sababu ni suala la Muungano, lakini nitoe tahadhari kwamba hili suala tusiliachie likaendelea linaweza kutuvunjia umoja wetu, muungano wetu na udugu tulioujenga kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi imezungumzwa kwamba unakua kwa asilimia 6.2 kutoka 5.6 bado sio nzuri. Nitasema kwa nini. Bado kwa kipindi kirefu kijacho ongezeko la watu linaloongezeka kutoka 2.8% sasa ni 2.9% halitatusaidia katika kupunguza umaskini. Wataalam wote wa uchumi mnafahamu kama watu wanaoongezeka kwa 1% lazima uchumi wako upande kwa asilimia tatu(3%). Usipofanya hivyo hutapunguza matatizo ya uchumi lakini sisi tunaongezeka kwa 2.9% sawa na 3%. Ndio nasema ili tuweze kukidhi mahitaji ya wananchi lazima uchumi wetu ukue si chini ya 9%. Ndio nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu ashughulikie suala la ongezeko la idadi ya watu, tusilifumbie macho katika Tanzania. Bahati nzuri mimi ni kiongozi katika Bara la Afrika ambapo nashughulikia masuala ya idadi ya watu. Utaona nchi nyingi ambazo ni maskini zaidi ni zile ambazo ongezeko la watu linaongezeka zaidi ya 2% na ni katika Kusini mwa Bara la Afrika pamoja na nchi ambazo tunasema wenzetu wako katika ulimwengu wa pili. *Asia* wanaongezeka kwa 1%, mwisho kabisa 1.5%. Sisi tunaongezeka na bado tunaona sifa kuongezeka. Shida sio suala la kuongezeka watu lakini muhimu ni idadi na umuhimu wa kuwa na watu ambao wanaongezeka kwa wastani wa 2% au chini ya 2% ili iendane na hali ya kukua kwa uchumi. Sasa hiyo ni kazi mojawapo ambayo lazima tuiifanye.

Mheshimiwa Waziri Mkuu umekuwa msemaji mkubwa sana katika suala hili. Nakumbuka Rukwa ulikuja ukazungumza sana na Rukwa kwa kweli sisi ni namba mbili tunaongezeka kwa 4.2% nadhani tunakimbizana na Dar es Salaam, Kigoma, Zanzibar ndio wanatushinda, ndio *Number One.* Hao wanaongezeka kwa 3.1% haya mambo sio ya kujivunia hata kidogo. Ndio maana tunaomba hata wataalam waende katika maeneo hayo kuona tatizo liko wapi. Bila kufanya hivyo idadi ya watu itazidi kuongezeka. Ni vizuri sera ambayo inashughulikia ongezeko la idadi ya watu ikasimamiwa na ikaanza kufuata utaratibu mzima wa kuhakikisha mambo haya yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima ambalo linashughulikia mambo ya chakula. Uzuri, mambo ya chakula Mheshimiwa Waziri Mkuu umeshalizungumza katika hotuba yako kwamba Serikali imeshatambua na kila jitihada inafanyika ili kuona nini kifanyike ili angalau athari za upungufu wa chakula katika maeneo yetu lisije likawa ni kero. Lisije kuwa ni siasa, *because food is politics.* Chakula ni siasa na tusipodhibiti hali hiyo tutaweza kupata matatizo makubwa sana. Lakini nashukuru maandalizi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nadhani atatupa taarifa ambayo itakwenda kwa undani kuhusiana na jambo hilo. Kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi ni Wabunge na Mheshimiwa Spika unafahamu Mbunge ndiye anayeunda Bunge. Sasa kiungo hiki kikitetereka Bunge halitakuwepo. Nasema hivyo kwa sababu ya mazingira ya utendaji wa kazi katika Majimbo yetu bado tuna matatizo makubwa sana ya namna ya kutoa huduma kwa wananchi. Mimi nimejionea kwa sababu niliwahi kuwa *frontbencher na backbencher* nimeona tofauti zilizopo. Hali ya Wabunge sio nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa sababu tungekuwa na kitu kinaitwa *Political Vote* ya kusaidia angalau huduma au kutoa michango kidogo kwenye miradi mbalimbali midogo midogo ingetusaidia. Wenzetu baadhi ya Wakuu wa Mikoa, nawashukuru baadhi yao, wanapopata vile vi-*political vote* wanasaidiana na Waheshimiwa Wabunge kujaribu kupeleka hela kidogo kidogo kule. Sasa sio wote wapo wengine wanaweza kuzitoa zile fedha kwa utaratibu mwingine. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbaya.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nadhani ni vizuri tukaliangalia suala hili zile *political vote* zinatusaidia sisi Waheshimiwa Wabunge ili ukikuta kuna tatizo la bati moja utoe ama sivyo tukitegemea mfuko wetu hatufiki mahali popote. Ndio maana wengine tunafikia mahali fulani hata unapotembelea Jimbo lako unakuwa ni mwoga sana kwa sababu utaombwa hata kitu kidogo utashindwa. Nadhani hilo ni vizuri likaangaliwa katika uzito wenyewe. *S*uala lingine ni vyombo vya habari, kwanza napenda kutoa pongezi za dhati kwa Ndugu Betty Mkwasa, kwa heshima aliyopata. Natoa pongezi hizo kwa sababu ni heshima kwa Tanzania lakini pia tuwapongeze viongozi wa *ITV* kwa kazi nzuri wanayofanya kupitia kwa Reginald Mengi. Wanafanya kazi nzuri kwa sababu kwa kweli wamefanya kazi ambayo ilikuwa Serikali iifanye kusambaza taarifa kwa nchi nzima lakini wanashirikiana wote pamoja. Itakuwa vizuri siku ya vyombo vya habari duniani tuwe na utaratibu wa kuwazawadia watu kama hawa, tutawapa hamasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Waandishi wa Habari pamoja na kuwapongeza lakini nadhani Ofisi hii ya Spika ingeandaa kauratibu ka kuwapa mafunzo maalum hasa mafunzo yatakayosaidia kutoa maelezo sahihi yanayosemwa na Wabunge. Juzi niliogopa niliposikia kwenye vyombo vya habari kwamba kuna baadhi ya Wabunge wameibiwa mamilioni ya hela. Unajua *psychologically* watu wanaposikia Wabunge wana mamilioni ya hela wanasema hawa kumbe wanatuficha wanalalamika bure tu. Sasa hizo taarifa hivi unazitoa kwa utaratibu gani? Sasa ni vizuri tukasaidiana tusije tukajenga hisia mbaya miongoni mwa watu wakaanza kutuvia barabarani wakidhani tuna mamilioni ya pesa, sio vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, dhana ya uwezeshaji. Hapa katikati pameanza kujitokeza, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni vizuri tukalielewa. Lisemwalo lipo kama halipo laja Waswahili wanasema hivyo. Kuna suala hili la uwezeshaji na nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu umesema kwamba sera inaandaliwa ambayo baadaye sheria itakuja izungumzie suala zima nini tunawafanya Watanzania waweze kupata nafasi ya kuendesha uchumi wao wenyewe. Sasa dhana ya uzawa inazungumzwa na wengi inawezekana neno uzawa watu wengine hawalipendi lakini bado ni suala lile lile la uwezeshaji. Lazima sisi wenyewe tuusimamie. Maendeleo ya Watanzania kwanza lazima tukubaliane yataletwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Ibara ya 89 alisema maendeleo ya Watanzania yataletwa na Watanzania wenyewe. Maendeleo ya akina mama nayo yataletwa na akina mama wenyewe. Lazima muanze ninyi msipopiga kelele siwafichi hatuwasaidii. Huo ndio msingi, Watanzania ni lazima tupige kelele ili tupate haki na tusipopiga kelele *who is going to do for us,* hakuna! Ndio maana lazima tuanzie mahali fulani. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni vizuri tusilichukulie kama jambo la kawaida lakini tulichukulie katika uzito unaostahili na Serikali ifanye kwa makusudi mazima kuwapa kila aina ya msaada ili wawezeshwe waweze kupambana na Mataifa mengine ya nje. Hatukatai wawekezaji kutoka nje wacha waje lakini sasa tumewaandaa vipi Watanzania ili kuwasaidia ili wapambane na hao wengine? Tutabaki tu ni watu wa kulalamika lakini ni kwa sababu hatujaandaliwa vya kutosha. Tungeomba sasa suala zima la sera zote zilizopo katika nchi hii ziandaliwe *program of action* kwa sababu zimebaki kwenye makaratasi tu lakini tungependa kila sera tujue ina ina programu gani ya utekelezaji. Hii itatusaidia kujua mambo yanakwenda katika misingi gani. *S*isi wengine kwa sababu ni *highly disciplined* hatutaki kupigiwa kengele nyingine, nataka kusema kwa dhati naunga mkono hoja na namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu na watendaji ili wafanye kazi yao vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyoweza kugusa Wizara karibu zote. Pia napenda kuwapongeza Mawaziri waliopo katika Ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa na kuingia katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunawakaribisha sana na tunawaahidi kushirikiana nao. Kipekee nawapongeza Wabunge wa *CUF* waliokuja kutuongezea nguvu katika Kambi yetu ya Upinzani iliyokuwa inakufa siku hadi siku lakini sasa tuko imara. Pamoja na kuwa mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Sheria na Katiba ambao tulipitia Bajeti hii ya Waziri Mkuu, naomba kuchangia machache ili kuendelea kuboresha yale ambayo tuliyapitia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nianze na suala la Makao Makuu kuhamia Dodoma. Nashindwa kuelewa suala hili limeanza kuzungumziwa siku nyingi nimeanza kulisikia toka nikiwa Shule ya Msingi, nimekwenda Sekondari sikutegemea kuwa Mbunge na leo niko ndani ya Bunge hili Tukufu bado linaendelea kujadiliwa na sijui msimamo wake ni nini. Ninaiomba Serikali hasa Waziri Mkuu kwa kuwa wanasema sera zao ni za uwazi na ukweli walieleze Bunge lako Tukufu ukweli na wananchi wapate kujua ni lini Makao Makuu haya yatahamia Dodoma rasmi. Pamoja na kuwa kuna Wizara ambazo tayari zimeanza kufanya kazi Dodoma lakini watendaji wake wakuu wengi huwa Dar es Salaam na huonekana tu wakati wa vikao vya Bunge lakini baada ya vikao vya Bunge watendaji wake wote wanarudi Dar es Salaam. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ana-*wind up* atueleze ni lini yeye atahamia Dodoma, mwaka gani na tarehe ngapi ili wananchi waweze kumsikia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala la UKIMWI. Janga la UKIMWI limeathiri sana nchi yetu na walioathirika zaidi ni vijana ambao ni raslimali ya Taifa letu na vijana wengi wameathirika na UKIMWI kutokana na ugumu wa maisha, hawana kazi na wengi wamejiingiza katika biashara ya ngono ambayo sio salama. Hivyo ninaiomba Serikali iweke mipango madhubuti ili iweze kuwaokoa vijana hawa ambao ni tegemeo la Taifa letu. Vile vile napenda kuwapongeza *TACAIDS* kwa semina na warsha mbalimbali ambazo wametoa kwa ajili ya ugonjwa huu wa UKIMWI. Lakini napenda kuwaambia kwamba umefika wakati wa kuachana na makongamano, warsha, twende vijijini kwa wananchi ambao hawana elimu hii ya UKIMWI tukawape elimu hiyo ili waweze kuwasaidia au kuwahudumia wagonjwa wale ambao wengi wao wanatoka mijini wanapelekwa vijijini ambako elimu hii kwa sasa hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchangia kuhusu Televisheni yetu ya Taifa. Kwanza niwapongeze wafanyakazi wa TVT kwa kazi ngumu wanayoifanya katika mazingira magumu ila napenda kuishauri Serikali kwamba wakati sasa umefika tukiangalie kitengo hiki tuboreshe mishahara yao kwa kuwa tumedhamiria tunataka matangazo haya yafike Mikoani basi tuwaangalie wafanyakazi, tuongeze mishahara yao na nyenzo za kufanyia kazi. Hatuwezi kufika Mikoani kama hatutaweza kuboresha mishahara ya wafanyakazi na vifaa ambavyo wanafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu rushwa. Sasa hivi rushwa imeota mizizi na Serikali yetu imeshindwa kupambana na rushwa kwa sababu wanaopokea rushwa ni watu wawili wanaokubaliana na hawapeani hadharani. Hivyo tungependa vijana wetu wa *PCB* kama kweli tunataka waweze kupambana na rushwa tuwawezeshe kutumia teknolojia mbalimbali maana rushwa imekuwa ni tishio na wananchi wanashindwa kupata haki zao kutokana na rushwa ilivyokithiri. Inavyosemekana kwa sasa hivi mtoaji na mpokeaji rushwa wanapeana kupitia mikataba ya nchi inayowekwa nje ya nchi na rushwa zenyewe zinapitia kwenye *Account* zao. Hivyo basi, tunaiomba Serikali iwe makini kama kweli inataka kuliondoa tatizo hili la rushwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuchangia kwa siku ya leo ni kuhusu jengo la Chimwaga. Mwaka jana tulitenga shilingi milioni mia tano na mwaka huu tena zimetengwa milioni nyingine mia tano. Sasa ninapenda kujua Serikali yetu inafaidikaje na jengo hili kutokana na fedha hizo ambazo zinatengwa maana yake milioni mia tano kwa nchi yetu ambayo tunadai ni maskini ni nyingi sana ambapo zingeweza kutatua matatizo ya wananchi kama vile maji, elimu, afya na kadhalika. Naomba basi tuambiwe Serikali inanufaikaje katika jengo hilo ambalo limekabidhiwa Serikali. Kuna Chama kimoja ambacho kinafanyia mikutano katika jengo hilo la Chimwaga je, kinalipia pesa kiasi gani kwa matumizi ya jengo hilo? Ili tuweze kuendelea kutoa hizo milioni mia tano bila manung'uniko, naomba Serikali ifafanue kuhusu suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu utawala bora. Nchi yetu ni ya Vyama vingi na kila mwananchi ana hiari ya kuingia Chama chochote bila kubughudhiwa na mtu mwingine yeyote kwa kuwa ni hiari yake mwenyewe. Lakini katika pitapita zetu katika mizunguko yetu tumekuta wananchi wa Vyama vya Upinzani hawatendewi haki, wanabughudhiwa kwa sababu wamejiunga na Vyama vya Upinzani.

**MBUNGE FULANI:** Toa ushahidi.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuniambia nitoe ushahidi wananchi wenyewe wanaweza kutoa ushahidi huo kwa sababu hawatendewi haki hasa katika biashara zao, wanasumbuliwa na hivyo kuwakosesha amani na kukosa uhuru katika nchi yao. Hivyo kwa kuwa wako kihalali na Vyama vingi vilipitishwa kisheria, tunawaomba wale ambao wanawabughudhi wananchi waache kwa sababu ni uamuzi wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliyokuwa nayo ni hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi, nitaunga mkono baada ya kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wasemaji wa mchana wa kwanza atakuwa Dr. James Msekela, atafutiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo. Hadi kufikia hapo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.51 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii ya awali mchana huu ili na mimi nichangie kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote katika ofisi yake kwa kazi nzuri waliyoifanya kupitia kwenye mawasilisho haya, ingawa details hazipo hapa lakini kwa kazi ambayo imefika kwenye Kamati napenda niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda niipongeze tena Serikali kupitia kwa Waziri wa Fedha kwa jinsi walivyowasilisha bajeti yao. Kwa kweli niseme tu pongezi hizi nazileta kwa sababu na mimi naamini na ni kweli ndivyo ilivyo kwamba bajeti ya mwaka huu ni bajeti ya watu. Sasa unaweza kuwa na yale machache ambayo kila siku lazima yawepo kwa ajili ya kuboresha, lakini kwa ujumla wake ni bajeti ya watu na ni bajeti ambayo inatupatia mwelekeo na matumaini katika siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kuanza tu kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa kwanza nionyeshe mshangao wangu ambao siku zote huwa ninautoa na naomba niutoe tena leo. Katika aya ya kwanza sentensi ya mwisho hapa anasema: “Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka huu”. Sasa mimi najiuliza kwa nini kama Waziri yeye ni branch nyingine, ni *branch* ya *Executive* na sisi ni Bunge kwa nini sisi tunawasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu. Kwa kweli hili huwa linanikera kweli kweli, sidhani kama sisi tunashindwa kuwasilisha mambo ambayo yanatuhusu. Lakini hii inaonyesha tu kwamba kuna kazi ya kufanya katika kujaribu kuona kila nguzo iliyopo hapa nchini kweli inajitokeza kama ambavyo dhamira ya Katiba ilikuwa.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kusoma makala yako, ukijaribu kuonyesha kujitokeza huko na jinsi ambavyo Katiba imejaribu kuonyesha na wewe umejaribu kuonyesha jinsi ambavyo vyombo hivi vinatakiwa viingiliane ili kuleta ile s*ection balances*. Nisingependa kutumia uwanja huu kujaribu kuleta malumbano ya *academic* lakini nafikiri bado kwa kweli Bunge angalau kwa kupitia kwenye kujiwasilisha lenyewe ndani ya Bunge lingetumia sauti yake yenyewe. Nafikiri tunaweza tukakutumia wewe, lakini kama umeketi hapo Naibu wako anaweza akafanya kazi hiyo au wale Wenyeviti wengine wanaweza wakawasilisha mahitaji yetu kwa mwaka wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba huu nafikiri ni utamaduni kwa sababu ukisoma kila makala ambayo utakutana nayo utakuta inaelezea hivyo hivyo kwa mila na utaratibu na nini, lakini sidhani kama dhamira ya Katiba ilikuwa hivyo. Mimi naomba tulitafakari sana hili na kwa kweli ningependekeza kwamba mwaka ujao ofisi yako ndiyo iwasilishe mahitaji yake ya bajeti mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kwenda ndani katika haya mahusiano ya hizi *pillars* tatu lakini ukweli ni kwamba kila ukiliongelea hili suala ambalo nimeligusia huwezi kukwepa ule ukweli kwamba tunatakiwa sisi kama Wabunge kuisimamia na kuishauri Serikali. Sasa unaposimamia dude kubwa kweli kweli na wewe ni kijitu kinyonge na kidogo sana wala huleti maana nzima ya kusimamia. Hapa nataka nilete tena

changamoto mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba nafikiri kuna haja sasa angalau kwa kupitia kwenye maandishi ambayo yatakuwa yanafahamika kwamba kama Bajeti ya mwaka huu ni asilimia mia moja basi *Executive* inapata asilimia kadhaa, Bunge linapata asilimia kadhaa na *Judiciary* inapata asilimia kadhaa. Hii inatakiwa ieleweke kwa sababu *otherwise* tutakuwa siku zote tunakuwa *mercy* ya *Executive* kitu ambacho nafikiri kina-*diminish* sana *power* ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee ya kwangu kidogo mwaka jana na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais aliyetangaza kwamba na sisi tumepata Wilaya ya Uyui na sasa kwa kweli nilikuwa natarajia katika bajeti hii itajitokeza waziwazi nia ya Serikali ya kutufikishia Wilaya hiyo kwa sababu ni mlolongo wa kufika kwetu kwa kupitia Serikali Kuu. Sasa nimejaribu kuangalia kwenye vitabu ambavyo vimekuja pamoja na bajeti hii nimeona maneno ambayo yamenichanganya. Sasa nilikuwa nataka nitumie nafasi hii kuwaomba wale wanaohusika waliangalie hili kwa sababu kwa kweli mimi mwenyewe nimejaribu kuangalia ni jinsi gani Serikali imepanga utaratibu wa kukamilisha yale ambayo ilidhamiria kuyafanya kwetu kwa kutupatia Wilaya

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kujenga boma, ukiangalia pale *figure* ambazo zimetolewa *against Uyui* zinakuwa tena kama zinachanganywa na jina lingine tena. Nisingependa nilitaje lakini ninachosema hapa ni kwamba hatujawa *very comfortable* na *figure* zile zilizotoka na uhakika kwamba kweli hizi pesa zinakuja kwetu. Lakini mimi naomba nitumie nafasi hii pia kuwakaribisha wale wote ambao wana nia ya kuja kuwekeza kwetu, kwa kweli kuna vitu vingi tu ambavyo wawekezaji wanaweza kuja kuvipata kwetu. Kwa taarifa za kina wanaweza kuwasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri yetu ya Wilaya lakini niseme tu *location* ya Wilaya yetu na hususan hayo Makao Makuu yanayotarajiwa inatoa nafasi nzuri sana ya wale hasa ambao wanataka kufanya biashara kuwa kwenye ramani ya biashara kwa sababu ipo karibu na *highways* ambazo zitakuwa zina-*connect* Mashariki ya nchi yetu na Magharibi ya nchi yetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, nina hakika *flow* ya pesa pale itakuwa nzuri sana na huduma za wawekezaji bado zinahitajika za aina nyingi za wawekezaji wa aina nyingi, kwa hiyo tunawakaribisha sana na hasa hawa watu binafsi ningependa niwakaribishe kipekee na niseme tu kwa uchache watu wa maeneo hayo hasa ambapo Makao Makuu ya Wilaya yatajengwa ni hodari sana katika kilimo cha mboga mboga na vile vile zao la tumbaku. Nafikiri mnafahamu kwamba Tabora tunalima sana tumbaku, lakini nataka nipanue wigo wa uelewa wao kwamba kuna mazao vile vile ya mbogamboga, nyanya na vitunguu, wanaweza wakaweka viwanda vyao vidogo vidogo wakasindika mazao haya na sisi tutawapatia nguvu kazi ya kutosha kabisa. Maji na umeme navyo vitapatikana, hiyo nina uhakika, karibu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo suala la nyumba za Serikali au majengo ambayo yanajengwa kwa fedha za Serikali. Kwanza naomba hatimaye na mimi niseme tu kwamba kwa kweli kwa sababu zoezi la kuuza nyumba za Serikali limekwishaanza na hatua iliyofikia kwa kweli wala haina maana tena kuanza kulipinga. Kwa kweli nia na dhamira ya kufanya hivyo ni nzuri kwa sababu watu ambao *eventually* wanapata hizo nyumba ni Watanzania na unataka kuboresha makazi ya Watanzania na hasa kama wanafanya kazi katika Serikali yao. Lakini nataka niseme kwa kufanya hivyo tu tuliambiwa kwamba Serikali imekwishauza nyumba 3000 kati ya nyumba 9000 za Serikali na kwamba zile nyumba ambazo zilijengwa kwa madhumuni ya kuwatunza viongozi wa Kiserikali au wa Kitaifa kule Dar es Salaam hazijauzwa. Sasa kama ndivyo basi hii pia inaonyesha kwamba Serikali kwa kweli haina nia ya kuhamia Dodoma. Kwa sababu kama una nia ya kuhamia Dodoma uta-*keep* namna gani nyumba za *Executives* wa Serikali yako Dar es Salaam. Hiyo tayari inaonyesha kwamba hakuna nia ya dhati au mpango mahsusi wa kuhamia Dodoma angalau kwa kupitia uuzaji wa nyumba hizi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa napenda nilete pendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba kama kweli wana nia ya kuhamia hapa, basi watafute utaratibu wa kuziuza hizo nyumba kwa bei ya soko, watapata fedha nyingi sana, watakuja hapa, watajenga majengo yao na Serikali itahamia kweli hapa Dodoma. Ni kitu ambacho kinawezekana lakini pia napenda nitumie nafasi hii kuonyesha kuwa jinsi ambavyo Dodoma itakuwa na matumaini ya kujengeka kwa sababu nia ya Serikali ya kujenga hii barabara na kuunganisha *The Great North Road* mpaka *South Africa* na hii ya kwenda mpaka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, vimeonekana na vitu ambavyo ni *proud* kwa sasa hivi na kwa kweli barabara imekwishafika Tabora ingawa siyo kwa hali nzuri sana lakini matarajio tayari yapo. Sasa nilikuwa nataka niseme kwamba kwa namna hiyo biashara hapa itakuwa imeshamiri na nina hakika kitakachofanya

Dodoma ijengwe ni biashara na wala siyo Serikali. Serikali inatakiwa kuhamia hapa kwa kuleta wafanyakazi wake lakini Mji utajengwa na biashara ambayo lazima itakuja kama utajenga hizi barabara mbili haswa ya Kaskazini Kusini na ya Mashariki kwenda Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie *particularly* Mji wa Dodoma na kwa kupitia Mji wa Dodoma Miji mingine yote nchini ambayo imejengwa kwa mtindo huu. Kwa kweli hatuna msamaha wa jinsi ambavyo tunatumia ardhi yetu vibaya vibaya tu bila mpango mzuri tunapojenga Miji yetu. Ukiangalia *density* ya Miji yetu ni ndogo sana kulinganisha na Miji ya wenzetu, unakuta Mji ume-*stroll* na hii *strolling* ya Miji yetu kwa kweli inakatisha tamaa inafanya hata gharama za kuishi katika Miji hii zinakuwa kubwa sana. Inabidi ujaribu ku- *extend services* sehemu ambazo kwa kweli hata uwezo wako si mzuri. Kwa mfano, angalia hapa Dodoma kuna *unit* kama 47 zitajengwa au zinaendelea kujengwa hapa, kumi zimekwishajengwa tayari, zipo kilomita mbili tu kutoka *City Centre*. Sasa unapojenga nyumba ndogo ndogo namna hiyo kilomita mbili tu kutoka kati kati ya Mji na huu ni Mji ambao unatarajiwa kukua kibiashara pia kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya Serikali nia yako ni nini? Umetazama umbali wa miaka gani mbele? *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwamba kwa kweli kuna haja ya kufanya marejeo ya jinsi ambavyo tunatumia ardhi yetu na hasa jinsi ambavyo tunapanga Miji yetu na hatimaye jinsi ambavyo tutaokoa gharama nyingi sana ikiwa ni pamoja na nishati na maji na kila kitu ambacho kinatumika kwa jinsi ambavyo unasambaza Mji bila kuwa na c*oncentration proper* kama ambavyo wataalam wetu wanakuwa wana-*recommend*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia muda wangu nilikuwa napenda nigusie suala la jumba la Bunge ambalo linatarajiwa kujengwa. Naomba niseme kwamba nafikiri hiyo nayo ni hatua kubwa na ya kupongezwa. Lakini naomba niseme kwa nini halijafika hili suala hapa Bungeni tukalijadili kwa sababu nina imani kwamba kutakuwa na mchango mkubwa tu wa mawazo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama hoja hii ya jengo la Bunge itafika hapa na sisi tuijadili tuelewe ni kitu gani kinakuja na tushiriki katika kuboresha. Nafahamu hatua ambayo imeshafikiwa nafikiri hata wachoraji wamekwishachaguliwa, sasa nafikiri hatua imefika mbali sana. Lakini nasema bado hatujachelewa sana, nafikiri tuta-*benefit* sana kama hili jengo litakuja hapa tulijadili.

Mheshimiwa Spika, nisingependa niendelee zaidi ya hapo kwa sababu natunza muda wangu. Kwa hiyo, naomba niongelee kidogo kuhusu Televisheni ya Taifa na *particularly* kupitia hili gari la matangazo *(OB Van)* ambalo tunaliona hapo nje. Kwa kweli vitu hivi vina gharama, lakini huwezi kukwepa gharama kama unataka kuleta vitu ambavyo vitawafumbua na kuwasaidia wananchi wako. Utaratibu ambao tunao sasa hivi wa kuzuia Televisheni binafsi kutangaza kama wanavyojiweza unafanya kwa kweli Televisheni ya Taifa iendelee kuwa muhimu sana kuongezewa fedha ili iweze kuwafikia wananchi wengi na kwa kuanzia nilikuwa napenda kwa kweli nipendekeze kwamba hili gari ambalo tunalo hapo nje *Digital OB Van* nafikiri badala ya kulikodisha ni bora sasa likawa *owned* kabisa na Serikali ya Tanzania, hilo au lingine la namna hiyo na kwa kupitia hiyo uwe ni mkakati wa mwanzo wa kuboresha na kuongeza nguvu ya Televisheni yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabla muda wangu haujaisha nilikuwa naomba niseme hivi, kwa kweli suala la Ukimwi kama ambavyo limeongelewa katika hotuba ya Waziri Mkuu halijapewa *prominence* ambayo ungetarajia watu ambao tumebanwa kwa kweli na suala hili na limetangazwa kwamba ni janga la Kitaifa halijapewa kabisa umuhimu ambao unastahili.

Kwa mfano, ukiangalia hapa ukurasa wa 65, hotuba inasema kwamba: "*TACAIDS* imezijengea mamlaka ya Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia na kudhibiti kuenea kwa Ukimwi. Mimi sidhani hili kama kweli limefanyika. Mimi ninavyofahamu hili labda lipo kwenye zero *charter* ya kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kupitia aya hii fupi kama ilivyo ambayo haijai hata ukurasa mmoja kuhusu janga la Ukimwi, inaonyesha *commitment* yetu ambavyo pia inahitaji kuongezeka katika kupambana na Ukimwi ili tuweze kuwa na uhakika zaidi wa hatua ambazo tunataka kupiga katika

kuboresha hali ya maisha ya wananchi wetu kwa sababu kwa kweli bila kuangalia hili ni janga ambalo lipo na ni *reality* ya maisha yetu sasa hivi hatuwezi kukwepa.

Watu wanaathirika kila kukicha na kwamba watu wanapoteza maisha na matumaini kwa kweli ya kuendelea kupata nguvu ambayo itakuwa haijaathirika yanazidi kupungua kama mikakati na hasa kupitia hawa *TACAIDS* ambao kama ilivyosemekana hapa haitakuwa juhudi yao ya dhati.

Mimi nafikiri hapa bado kuna haja kubwa ya kuboresha na hasa ningependa kupitia kwenye mchango wa Ofisi hii ya Waziri Mkuu sasa atakapofika mhusika nafikiri ni Ofisi yake Waziri Mkuu, lakini pia na watu wa Afya wajaribu kuonyesha kwa mapana kama itakavyowezekana, Serikali imetenga kiasi gani na ina utaratibu gani wa kupambana na maambukizi ya UKIMWI na kuzuia kuenea na kusambaa kwa UKIMWI?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu nimeruka ruka sana naomba niseme kwamba naunga hoja mkono, tumpatie fedha Waziri Mkuu afanye kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jioni ya leo. Niitumie pia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioshinda kwenye chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni, hususan Wabunge wa CCM. Karibuni tushirikiane kutunga sheria za nchi, kutetea maslahi na kuinua uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Seif Khatib, anayeshughulikia Habari na Siasa pamoja na Makatibu Wakuu wao na wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa nchi na kusaidia wananchi kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia bajeti hii kwa kuwa imetamka bayana kuwa itaboresha kilimo kwa kufufua Vyama vya Ushirika na kuhamasisha mabenki mbalimbali kwa kuandaa mazingira mazuri ya kuwakopesha wakulima zana za kilimo na mitaji mikubwa ya kupanua kilimo na kulima kilimo cha kisasa kitakachowasaidia kuvuna mazao mengi ya biashara na ya chakula ikiwa ni moja ya sera ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Serikali itakubaliana na mimi kuwa washikadau wakuu wa suala zima la kilimo ni wanawake. Ninasema hili nikiwa na mfano hai kwa Mkoa wa Singida kupitia zoezi la Mpango Shirikishi Jamii. Mkoa wa Singida ulibaini kuwa wanawake wanafanya kazi masaa kumi na tisa kwa siku wakati wanaume wanafanya kazi masaa tisa. Hivyo basi kwa juhudi hizi za wanawake endapo watawezeshwa ninaamini watatumia nguvu zao kuinua uchumi kwa familia zao na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ina kitengo cha kutoa msaada pale panapotokea maafa, huu ni ubinadamu wa hali ya juu na mila ya Mtanzania na Mwafrika kwa ujumla. Niiombe basi Serikali iwakumbuke wafanyabiashara wa kituo cha basi Singida Mjini waliounguliwa maduka yao yenye thamani ya mamilioni ya fedha kati yao wakiwemo wanawake wajane ambao sasa hivi hawana mbele wala nyuma na wao wapewe kifuta machozi kitakachowasaidia kuanza maisha yao upya kwani hatua waliyofika ilikuwa ni kubwa lakini wameunguliwa mali zao zote wakati wengine walikuwa hawana hata akaunti benki, hivyo hawana hata mtaji wa kuanzishia miradi hiyo upya.

Mheshimiwa Spika, ndani ya bajeti hii vile vile imeainishwa Mikoa itakayojengwa minara ya kurushia matangazo ya Televisheni ya Taifa ikiwemo Mikoa ya Dodoma, Tabora, Mwanza na kadhalika. Kwa kuwa Mkoa wa Singida tayari tulishapata salam za awali kwamba na sisi tungeweza kujengewa mnara wa kurushia matangazo ya Televisheni ya Taifa ingawa kwenye bajeti hii Singida haijatamkwa.

Niombe basi kama imesahaulika ikumbukwe kwa kuwa hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema popote pale panapoonekana kuna umuhimu yeye ana uwezo wa kuchacharika usiku na mchana kufanikisha lile ambalo linakuwa na umuhimu wake.

Nina imani kupitia Bunge lako Tukufu wananchi wa Mkoa wa Singida wakitamkiwa rasmi kwamba Televisheni ya Taifa wataipata lini itakuwa ni changamoto kubwa sana kwao kwani hivi sasa wanaona *TV* kupitia mtu binafsi ambaye kuvuta kwake ni gharama kubwa, ni elfu hamsini na bado kuna gharama ya kila mwezi ya shilingi 10,000/= kitu ambacho ni ghali sana kwa mwananchi wa kawaida.

Hivyo wanaoiona *TV* sasa hivi Singida ni wale wachache wenye uwezo wa kuvuta *TV* hiyo. Naiomba Serikali imwongezee Mheshimiwa Waziri Mkuu bajeti yake ili iweze kuwasaidia wana Singida kwa hili la TVT.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuipongeza Serikali kwani ni mambo mengi mazuri inayoyafanya kwa Taifa likiwemo suala la kupamb ana na UKIMWI. Kitendo cha kupeleka mafungu ya fedha kwenye Halmashauri zetu ni changamoto kubwa na msaada mkubwa utakaosaidia Halmashauri zetu kuweza kutoa elimu ya kupambana na ugonjwa huu hadi Vijijini kwani gonjwa hili hakuna sehemu ambapo halijafika. Familia nyingi zinawatunza wagonjwa wao kwa mazingira magumu kwani hawana elimu ya kutosha na wala hawana tahadhari ni jinsi gani wawatunze wagonjwa wao.

Vile vile ni vizuri basi Mfuko huu ukaainishwa bayana ni namna gani utakavyotumika katika kusaidia kupambana na gonjwa hili la Ukimwi kwa sababu inawezekana Mfuko huu ukaja ukatumiwa kwa malengo tofauti na jinsi Serikali ilivyolenga lakini endapo itaainishwa itawasaidia Maafisa Wahasibu wetu kujua ni jinsi gani Mfuko huu wautumie.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii pia imepewa kipaumbele kwenye suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Ni kweli kilimo hiki tukikitilia maanani kitakuwa mkombozi kwani mvua zetu hazitabiriki, hivyo ni vema kutunza maji yanayopatikana wakati wa masika. Kwa kuwa Serikali imeshaainisha mabonde yaliyopewa kipaumbele naiomba Serikali kupitia bajeti hii ikumbuke na mabonde yaliyoko Mkoani Singida.

Singida ina mabonde mengi yanayoweka maji. Ninaamini mabonde hayo yakiwemo mabonde ya Kintinku, Chikuyu, Sepuka, Kata ya Mtoa iliyoko Tarafa ya Shelui na mengine mengi yakipewa kipaumbele kama kilivyotolewa kwenye mabonde ya Mikoa mingine ninaamini hata wana Singida watakuwa na kilimo cha umwagiliaji na tutavuna mazao mara mbili kwa mwaka kama wanavyovuna Mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli juhudi za Serikali si haba kwani tayari ilishaanza mpango wa kuwasomesha wanafunzi wanaofaulu kujiunga na masomo ya sekondari ambao ni yatima au wenye wazazi wasiokuwa na uwezo.

Kwa kuwa Serikali huchukua kiasi kidogo na wengine husomeshwa na Halmashauri zao kwa mazingira magumu kwani Halmashauri nyingi hazina fedha, naomba basi Serikali kupitia Bajeti hii iongeze idadi ya wanafunzi, iwachukue wote waliothibitishwa na Halmashauri zao kwamba kweli ni yatima ama wazazi wao hawana uwezo. *(Makofi)*

Hii ni kwa sababu wanafunzi kusomeshwa kiasi fulani na Serikali na wengine kusomeshwa na Halmashauri ambazo hazina uwezo kunaleta matabaka ya usomeshaji kwani wale wanaosomeshwa na Halmashauri wanalipiwa ada tu na vitu vichache vingine wanashindwa kuvipata, wakati mwingine hata nauli za kusafiria wanakosa. Ni imani yangu kwamba Serikali ikiamua kuwasomesha wale wote walioainishwa na Halmashauri utakuwa ni ukombozi kwa wanafunzi wenye vipaji vya kuendelea na masomo ya sekondari kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa kuona kwamba Bajeti hii haipo mbali na huduma ya afya kwani tayari imeshaanza kukarabati hospitali zetu za Mikoa, Wilaya pamoja na Vituo vya Afya na kupeleka vifaa vinavyohitajika mahospitalini, mfano, vifaa vya *X-ray* na mashine za maabara.

Kwa hiyo, hapa niiombe Serikali ikumbuke kitengo cha mazoezi ya viungo kwenye hospitali zetu za Mikoa. Kwani ongezeko la wagonjwa katika kitengo hicho ni kubwa. Itoe vifaa vinavyohitajika kwani

wataalam wa kitengo hicho wanafanya kazi katika mazingira magumu, wengi wao wanatumia nguvu zao kutoa mazoezi ya viungo kwa wananchi wenye matatizo hayo kiasi kwamba hawa watu watakapozeeka watakuwa wameathirika kiasi kikubwa kwa sababu nguvu wanayotumia ni kubwa wakati wangekuwa wamepewa vifaa vya kufanyia kazi tungekuwa tumewarahisishia kazi zao. Ndiyo maana wataalam wa kitengo hiki wengi wanakimbilia katika hospitali za binafsi kwa kuogopa ama kushindwa kufanya kazi hizi katika mazingira magumu ambayo wanafanya kazi bila vifaa vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa hata Serikali imetambua kuwa wapo Maafisa Wahasibu wanaoshindwa kuweka kumbukumbu sahihi za fedha hususan fedha za Serikali Kuu na fedha za uhisani. Mawazo yangu ni kwamba huenda Maafisa hawa wamepitwa na wakati. Hivyo naishauri Serikali kupitia Bajeti hii ikumbuke kutoa semina mbalimbali kwa maafisa hawa ili waweze kutunza kumbukumbu sahihi za fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zao kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sikushukuru juhudi za Serikali katika ujenzi wa barabara. Tayari Serikali imeshapata wahisani wa kutengeneza barabara ya Dodoma Manyoni na Manyoni Singida, huu ni ukombozi wa hali ya juu. Maendeleo ya Mikoa yetu yanasababishwa vile vile na usafiri. Ninaamini sasa hivi baada ya muda mfupi tutakuwa tumeondokana na usafiri wa mabasi yaliyochakaa ambayo yanawalaza wananchi wetu siku moja au mbili njiani kwa sababu ni mabovu.

Ninaamini ujenzi huu ukikamilika wananchi wa kutoka Dodoma kwenda Singida badala ya kutumia masaa sita mimi naamini watakwenda kwa masaa mawili. Hivyo nimeona niipongeze Serikali kwa sababu haya si haba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yetu ina tabia ya kufanya mambo yake kwa hatua kulingana na uwezo. Hivyo basi ni imani yangu hata Mikoa mingine barabara zao zitakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia mchango wangu napenda nitamke rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. Mungu awabariki walioandaa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Mimi nitachangia kwa ufupi sana kwa sababu kwa ujumla yale yote ambayo yamezungumzwa katika kipindi cha Bajeti kwa maana ya hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji yamenikuna na kuniweka katika mazingira mazuri sana. Kwa hiyo, nasema nashukuru sana katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea napenda kusema kwamba naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ya kwangu kwa kweli yatakuwa ni kuishukuru tu Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu toka nilipotoa mchango wangu katika kipindi cha Bajeti cha mwaka 2001 niligusia masuala mengi ambayo yalikuwa ni kero katika Jimbo langu. Lakini napenda niseme kwamba kwa kweli katika kipindi cha mwaka moja na nusu Serikali imejitahidi sana kuweza kufuatilia na kunisaidia katika mambo mengi ambayo yalikuwa ni kero katika maeneo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na suala la Wizara ya Afya. Mimi katika Jimbo langu nilikuwa na matatizo makubwa sana, nilikuwa sina *Ultra Sound*, nilikuwa sina *X-ray*, tulikuwa hatuna gari la wagonjwa na wagonjwa walikuwa hawapati hata chakula walipokuwa wanalazwa hospitalini pale, lakini kwa sasa hivi mambo yote hayo yapo na yanafanyika. Napenda nichukue nafasi hii, kwa niaba ya wapiga kura wangu kuishukuru Serikali na kuiomba iendelee kutuangalia ili tuweze kumaliza matatizo yetu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitagusia vilevile suala la Mawasiliano na Uchukuzi. Nilipoingia Ubunge, reli yetu ilikuwa na mataluma yale ambapo reli inapita ya ratili 45. Lakini nilipomweleza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, bila kuchelewa alijitahidi sana kuhakikisha kwamba reli hiyo inabadilishwa kutoka ratili 45 kuwa ratili 56, ambapo sasa hivi kwa kweli tunasafiri *so smooth* haturukiruki

kama ilivyokuwa reli ile ikiwa na ratili 45. Lakini bado naiomba Serikali tutoke katika hizo ratili 56 ili twende ratili 80 ili tuweze kusafiri kama wenzetu wa Reli ya Kati. Kwa sababu kama navyofahamu Mkoa wa Rukwa hususan Wilaya yetu ya Mpanda ni *very potential* kwa mazao na kwa uchumi, kwa kweli kinachotukwamisha hasa ni usafiri. Lakini tunaiomba sana Serikali ituangalie katika hilo ili na sisi tuweze kupiga hatua kama maeneo mengine wanavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nigusie suala la kilimo. Mwaka 2001 tulikuwa na utata kidogo katika suala la kilimo kwa maana ya mbolea ingawa hapa katika Bajeti ya mwaka 2001 tuliambiwa kwamba mbolea itakuwa *subsidizes* na Serikali lakini badala yake mbolea ilipanda. Ilipanda kwa sababu usafiri wa kuisafirisha kutoka Dar es Salaam mpaka huko kwetu, kwa sababu tuko pembezoni na barabara zetu ni mbaya hali ilikuwa hairidhishi na ikaonekana kwamba mbolea imepanda bei na hatimaye wakulima kwa kweli wakashindwa kumudu kununua mbolea hiyo, hata wale walioweza kuinunua waliinunua kwa bei ya juu ambapo kwa kweli haikuweza kuleta *impact* au kuleta mazao kutokana na mbolea yenyewe kupanda bei. Lakini katika Bajeti hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amelizungumza hili na sote ni mashahidi kwamba Mkoa wa Rukwa ni mmoja kati ya Mikoa 4 inayoitwa *the big four* na pembejeo kwa kweli tutaweza kuhudumiwa katika bei nafuu sana. Kwa hiyo, katika hilo naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu nadhani nyote mnafahamu kwamba Mkoa wa Rukwa tulisharuhusiwa kuuza mazao nje na hiyo ndiyo inayoleta changamoto kubwa ya kuinua hali ya uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Rukwa hususan Jimbo langu la Mpanda Kati.

Kwa hiyo, kwa kweli suala la kuturuhusu kuweza kuuza mazao yetu nje kumetusaidia sana kuweza kuinua hali zetu za uchumi kwa wananchi wetu wa Wilaya yetu ya Mpanda hususan Mkoa wetu wa Rukwa kwa sababu imetusaidia sana. Walanguzi walikuwa wakija, lakini wananunua mazao kwa bei ya chini sana, lakini hii imetusaidia tumetoka kwenye gunia shiling 6,000/= tumekwenda mpaka kwenye gunia shilingi 18,000/= mpaka shilingi 21,000/= kwa hiyo, hali hii kwa kweli inaonyesha kwamba ruhusa hii imetusaidia sana kuweza kuleta maendeleo na kuweza kuinua kipato kwa wananchi ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika suala la madini sisi kule Mpanda maeneo yetu yalikuwa ni maeneo ya migodi na migodi hiyo inajulikana ni ya toka miaka hiyo ya nyuma toka enzi za ukoloni na niliweza kumwomba Waziri wa Nishati na Madini, aweze kuwaomba watu wa *MEREMETA* waje wafanye utafiti kule ili labda utafiti huo uweze kutusaidia kuibua tena upya migodi hiyo ili nasi tuweze kuinua hali yetu ya uchumi kwa msingi wa kuwa na migodi.

Sasa katika hili ningeendelea tu kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aendelee kuiomba na kuisisitiza Wizara ya Nishati na Madini, watusaidie hawa watu wa *MEREMETA* waje ili waweze kuja kuona nini ambacho kinaweza kikafanyika ili angalau migodi hiyo ambayo imelala kwa muda mrefu iweze kufanyiwa kazi na mimi nina imani kwamba dhahabu tunayo ya kutosha, lakini kwa sababu wananchi sasa hivi wanatumia zana duni ambazo huwezi ukaipata dhahabu kule chini, lakini kwa teknolojia ya kisasa, mimi nina imani Mpanda tunaweza tukapiga hatua kubwa sana kama migodi hiyo itaanza ku-*exploit* kama ilivyokuwa siku za nyuma. Kwa hiyo, naiomba Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, nitapenda vilevile nigusie na suala la maji. Maji katika Jimbo langu bado ni tatizo, lakini kwa kiwango fulani nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, nilimweleza tatizo la maji katika Jimbo langu la Mpanda na aliweza kufanya kila alichoweza akamtuma Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, akaja akatembea katika Jimbo langu. Lakini niendelee kusema kwamba kwa kweli wametusaidia kwa kutuongezea *motor* za kusukuma maji ili maji angalau yaweze kupatikana katika Mji wetu wa Mpanda. Lakini tatizo kubwa tulilonalo hivi sasa ni mtandao wa mabomba ambapo mabomba yale yameishia katika maeneo machache, ukiangalia kwamba sasa hivi mji wetu wa Mpanda umepanuka sana na labda kama tunasema Halmashauri ya Wilaya inaweza ikafanya juhudi hizo za kuweka mtandao mpya wa maji itakuwa siyo rahisi kwa sababu uwezo wa Halmashauri si mkubwa kiasi cha kukabiliana na tatizo hilo la kuweka mtandao wa mabomba ya kutosha katika mji wote mzima wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali watusaidie sana katika hili kwa sababu mtandao uliopo sasa hivi upo toka enzi za ukoloni au toka enzi za mwaka 47 na kama mnavyofahamu mji wetu wa Mpanda ni wa siku nyingi. Lakini ulianza katika hali ya udogo sasa hivi mji huo umepanuka sana.

Kwa hiyo, kutokana na kupanuka huko kwa kweli tunahitaji kupata mabomba ambayo yatasambaza maji mji wote wa Mpanda ambao unakwenda kilomita 5 kwa mzunguko. Kwa hiyo, nataka niiombe Serikali iendelee kuliangalia hilo ili iweze kutusaidia zaida ili tatizo la maji liweze kwisha katika Mji wetu wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, sisi tatizo letu kubwa sana ni nikichukulia hasa katika Mkoa wa Rukwa ni barabara. Barabara ni kweli sasa hivi kuna barabara ambayo imeshaanza kutengenezwa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alishalizungumza, barabara ya kutoka Tunduma kuja mpaka Sumbawanga, madaraja yalishaanza kujengwa na tulishaahidiwa kwamba lami itaanza kutengenezwa kipande cha kilomita 50 toka Tunduma ukiwa unaelekea Sumbawanga. Lakini bado nilikuwa nadhani kwa sababu hali ya barabara zetu kule kwa sababu ya mvua nyingi kwa kweli huharibika mara tu barabara inapotengenezwa, kwa sababu ufumbuzi wa barabara ni lami tu. Tukizungumza barabara za tope kwa kweli ni kama vile tunamwaga fedha kwenye shimo ambazo hazileti *impact* yoyote.

Kwa hiyo, mimi nataka niiombe Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkoa wa Rukwa ni vizuri ukaupa kipaumbele, wewe mwenyewe ni mwenyeji kule, mara nyingi unakuja na kwa kweli unatupa kila aina ya ushirikiano. Tunaomba utuangalie kwa kweli kwa macho zaidi ya hayo mawili, ili tuweze kuona kabisa kwamba Serikali inatusaidia sasa tunaanza kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mazao mengi, tuna wanyamapori wengi na hata utalii unaweza ukaingiza fedha nyingi za kigeni, kwa sababu tuna wanyama wa kila aina kule, tuna mbao nyingi, hasa za mti wa mninga ambao unapendwa kila mahali. Sasa kuweza kuzisafirisha mbao za mninga ni tatizo na bei ambayo wanaipata watu wa Dar es Salaam ni bei kubwa sana. Lakini yote hiyo inatokana na tatizo la barabara au usafiri tulionao kule kwetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nataka niiombe Serikali yako itusaidie sana kuuangalia Mkoa wa Rukwa na kutupa kipaumbele ili tuweze kuwa na barabara nzuri. Kwa kweli tukishapata barabara nzuri zitatusaidia sana kwa maendeleo ya nchi yetu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nichangie hayo, lakini narudia tena kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza katika Bunge hili Tukufu ili niweze kuchangia machache.

La kwanza, kwa sababu sasa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili la Bajeti, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuingia katika Bunge hili kutokana na chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni. Mimi ndiyo nilikuwa Mbunge wa mwisho kuingia katika Bunge hili sasa mimi ni *senior*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti. Kwa kweli inazidi kuongezea uzito kwa yale mambo ambayo tumeyasikia katika hotuba za Mawaziri wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Kwa hiyo, kwa ujumla naomba niipongeze sana na kushukuru hotuba hii safi na kabla sijaeleza lolote naona niunge mkono hoja hii moja kwa moja sasa hivi mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo ambayo naomba niyazungumzie kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu mzito na pengine Mheshimiwa Spika, hatanipa nafasi ya kuzungumza tena katika hoja ya Wizara inayofuata, lakini siombei hilo. Basi ukikutana na *chief* uzungumze yote wakati huo huo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amezungumzia kwamba kutakuwa na Mfuko wa kusaidia mawasiliano katika maeneo ya vijijini. Jambo

hili ni zuri na mimi nalipongeza na naomba katika Wilaya yangu tumekuwa tukizungumza sana habari ya kuboresha mawasiliano sisi tuko pembezoni. Maeneo yale ambayo sasa hivi yamekuwa *center* za shughuli za kibiashara maeneo kama ya Mlangali, Lugalawa, Mundindi, Mavanga na kule Manda, kwa hiyo huu Mfuko unaweza kusaidia sana. Kwa sababu sasa hivi mawasiliano ndiyo kitu muhimu na kinaweza kusaidia kuchochea maendeleo katika eneo husika. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulikuja kwenye eneo letu, lina miinuko mingi, hivyo kama mawasiliano hakuna inakuwa tatizo kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, vile vile amezungumzia suala la vyanzo vya umeme. Naona ndugu yangu Dr. Ibrahim Msabaha, ananitazama hapa anajua hii ni Mchuchuma tu. Vyanzo vya umeme ambavyo tunavianzisha katika nchi yetu nafikiri viwe vinazingatia umeme utakaopatikana kwa bei nafuu na mimi naamini kwamba bei nafuu ya umeme katika nchi yetu ni *source* mbili tu kubwa.

Mheshimiwa Spika, *source* ya kwanza ni maji kwa hiyo, kila juhudi ifanyike tupate umeme kutokana na maji kwa sababu ya unafuu wake. Lakini *source* nyingine nzuri na yenye unafuu kabisa katika nchi hii ni makaa ya mawe ambayo yamelundikana katika Wilaya ya Ludewa.

Wilaya ya Ludewa mkaa wake siyo wa kuchimba mgodi mrefu, mkaa huo upo juu, unaweza kuusomba kwa *spade*, sasa leo tuunguze gesi kwa mifano ya Songosongo ndiyo mradi ungekuwa wa tatu huo, kwa *spoon* tu unaweza kuuchota mkaa wa mawe wa Mchumama.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji walikuwepo, sasa nimeambiwa kwamba baada ya Mkataba ule na wawekezaji, kuna hatua iliyochukuliwa ya kufanya *Micro-Economy Survey,* sasa hatujui Mheshimiwa Waziri anayehusika labda atatueleza ni lini *Micro-Economy Survey* ripoti itatolewa. Halafu nasikia tu kwamba sasa hivi tunajaribu kutazama kuunganisha umeme kutoka nchi jirani. Sasa mimi nafikiri kwa busara yangu ndogo tungejaribu kuzingatia kuanzisha *sources* za kwetu na Mchuchuma *is the best source,* kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue hilo. *(Makofi)*

Halafu lingine nilikuwa nashangaa na naendelea kushangaa iko mipango mingi sana ya kuboresha mazingira katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, lakini sijaona hata siku moja mpango ukaletwa katika Bunge hili au mahali popote unaozungumzia kuboresha mazingira ya Ziwa Nyasa tatizo liko wapi. Hawa watu wamekosa nini! Kwa sababu nazungumza hivi, ni juzi tu kule Kyela watu walikuwa wanalalamika kwamba maji ya Ziwa Nyasa yanaongezeka sana na kuharibu mabonde yote ya Ziwa Nyasa. Kule Manda sehemu zile tunaita *Folk Land* ambazo ni sehemu zenye rutuba ya kutosha mvua zilikuwa chache lakini maji yalijaa kwa wingi sana. Lakini tulipoulizia tukawaambiwa kwamba wenzetu wa nchi jirani tunaogopa kutaja, nchi jirani walifunga mto pekee unaotoa maji kwa sababu ya ku- *rehabilitate dam* huko huko nchi jirani.

Sasa nasema hivi kama kungekuwa na mpango au pangekuwa na ushirikiano tungeweza kujua kwamba sasa hivi eneo lile linafanyiwa hivyo na maafa yatakayotokea yatakuwa ni haya. Sasa naomba Serikali iwe na mpango unaoeleweka wa kuendeleza maeneo yale. Zamani kidogo tuliweza kuwa na *research* ya *fisheries.* Lakini nimeona ile *research* ya *fisheries* sasa imekufa haifanyi kazi angalau ilikuwepo hiyo *research* na kulikuwa na *Project* moja ilianzishwa miaka ya zamani ya kuvua sehemu zile za Manda na kule Itungi, lakini naona nayo imekufa. Nadhani ni kwa sababu hatuelewi hasa Ziwa lile limekaaje na la nani na mpaka uko wapi, nawaachia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nizungumzie habari za kilimo, maana nimesema hapa siyo lazima kupata nafasi ya kuchangia Wizara zote. Kilimo kimeelezwa hapa na baada ya kutangazwa Bajeti wananchi wengi wa Ludewa wamenipigia simu kwamba kwa kweli wanafurahia kitendo cha Serikali cha kufidia zana za kilimo na mbolea. Sasa wasiwasi wao ni kwamba pamoja na mwaka 2002 kuwa na Mfuko ule wa mbolea, bado waagizaji wanaochukua mbolea kutoka sehemu za uzalishaji kupeleka sehemu za Ludewa walikuwa watu wa kutoka nje ambao kwa kweli hawakufikisha ile mbolea katika Wilaya. Wananchi wanaomba wateuliwe wafanyabiashara wanaotoka katika Wilaya ya Ludewa yenyewe na ndiyo wanaoleta mbolea miaka yote.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa Mheshimiwa Waziri kama takwimu zinavyoonyesha kwamba kahawa inayolimwa Mkoa wa Iringa nusu ya kahawa inatoka Wilaya ya Ludewa. Kwa hiyo, ninachotaka

kueleza ni kwamba pembejeo zinaletwa na wafanyabiashara hao hao walikuwepo katika Wilaya hiyo hiyo kwa nini hawa wasipewe nafasi ya kusambaza mbolea ambayo ina mpango wa Serikali katika Nyanda za Juu Kusini. Kwa hiyo, hilo nalo ni moja katika maombi naona litasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya hiyo tungeomba vile vile kwamba kwa kuwa sasa hivi katika uboreshaji wa kahawa tunahitaji sana ubora wa kahawa katika ushindani. Sasa kulikusudiwa kuwa mitambo *pulpery* za kukobolea kahawa katika *centers* na tulikuwa na *centers* kama tatu kule Mawengi, Lupande na Lugalao. Lakini *pulperies* hizo mpaka sasa hivi hazifanyi kazi. Tungeomba Waziri wa Kilimo na Chakula, wakati anazungumzia Bajeti yake atueleze kama kuna mpango huo kwa sababu kahawa tunayo na tunazalisha, lakini mara nyingi ubora wake unatokana na jinsi ya matayarisho yake na *pulpery* pengine ni moja ya vitu ambavyo vingeweza kusaidia kuboresha kahawa katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nielezee kidogo kuhusu mambo yanayohusiana na barabara. Katika barabara ambayo ilikuwa inakusudiwa kutengenezwa na wananchi walielezwa katika Bodi ya Barabara ya Mkoa ilikuwa ni barabara kutoka Ludewa hadi Manda, kwa maana ya kwamba barabara hiyo wata-*fund* watu wa Shirika la Benki ya *ADB*. Lakini huu ni mwaka wa pili, wananchi wana matumaini, lakini bado Serikali haijaonyesha utekelezaji wake. Barabara hiyo ilikuwa kwenye nadhani *El - Nino Rehabilitation Programme* ya barabara hizo. Tungeomba Serikali ichukue hatua ya kutimiza ahadi ambazo walikuwa wameziahidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono tena hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba za Bajeti zao ambazo wameziwasilisha Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza hasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa sababu ameweza kuwaridhisha wananchi wangu wa Kigoma ambao walikuwa wanalalamika mara nyingi kuhusiana na kodi ya maendeleo. Sasa kwa kuondoa kodi ya maendeleo naomba nimpongeze sana.

Vile vile nampongeza kwa kuwafikiria wastaafu ambao mara nyingi tulikuwa tukiuliza maswali mengi hapa Bungeni kwamba wasaidiwe waongezewe fedha za kustaafu. Sasa nadhani kilio chao kimesikilizwa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na naomba vile vile kwa wastaafu wale ambao walichukua fedha zao kwa mkupuo uweze kuwafikiria kwa Bajeti ijayo kusudi nao waweze kufaidika. *(Makofi)*

Baada ya kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri, naomba nitoe pongezi pia kwa Waheshimiwa Wabunge wapya ambao wameingia Bungeni nawakaribisha karibu sana hasa hasa Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, ambaye ametoka Mkoani Kigoma na ambaye amerudisha Jimbo la Kigoma Kusini katika himaya ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Mbunge wa Kigoma Kusini, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ujaribu kumpunguzia matatizo ambayo yapo katika Jimbo la Kigoma Kusini. Jimbo la Kigoma Kusini ni Jimbo ambalo ni kubwa nafikiri kuliko yote na lina matatizo makubwa sana. Kigoma umeeleza kwamba kuna matatizo ya ujambazi na haya matatizo ya ujambazi sana sana utapambana nayo katika Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kigoma Kusini halina barabara na Jimbo la Kigoma Kusini ndiyo linatuunganisha na Mikoa yote ya Tanzania Bara ukiondoa kidogo Mkoa wa Kagera. Barabara ya Kigoma kwenda Tabora ni ya muda mrefu, lakini mpaka sasa hakuna maendeleo yoyote, daraja limekamilika, lakini barabara haipitiki. Kwa hiyo, wananchi wa Kigoma Kusini pamoja na Kigoma kwa ujumla wanashindwa kuwasiliana na Mikoa mingine kuweza kupeleka mazao yao.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma haujawahi kukumbwa na tatizo la njaa na kwa sasa hivi tunacho chakula cha kutosha. Tunao mhogo ambao wananchi kama walivyosema wenzangu wa Mkoa wa

Mtwara hauna soko. Tunao mpunga mwingi sana katika kata ya Kalya, lakini namna ya kuutoa ule mpunga huo inashindikana kwa sababu hakuna barabara. Usafiri pekee wa kuifikia kata ya Kalya ni kwa njia ya maji, kama unavyofahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ziwa Tanganyika lina matatizo, kuna ujambazi mwingi na kuna mawimbi.

Kwa hiyo, ni vigumu kuchukua mpunga kwenye kata ya Kalya kuusafirisha na kuuleta Mkoani Kigoma. Wakati wenzetu wa Mikoa ya jirani wana shida mazao yamekauka kutokana na jua kali, sisi mpunga ni mwingi lakini namna ya kuusafirisha kuutoa Kalya inashindikana.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba tumepata barabara kutoka Ilangala kwenda mpaka Sunuka ambayo ni kwa mpango wa *TASAF*, lakini barabara hiyo tunaomba ifikie kiwango cha lami kusudi iweze kuwafikia wananchi. Vile vile tunaomba kama ikiwezekana hiyo barabara iweze kwenda mpaka Kalya kusudi tuweze kupata huo mpunga na kuondokana na janga la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayoshughulikia maafa, Mkoa wa Kigoma kama alivyosema umepambana na maafa ya aina nyingi. Tumepata maafa ya mafuriko kama alivyosema na wananchi wengi wameathirika hata vifo vimetokea. Tunashukuru sasa hivi wanajaribu kutusaidia kutengeneza mitalo ambayo na yenyewe imesaidia katika maafa ambayo yametokea sehemu ya Gungu Mkoani Kigoma. Lakini vile vile tunaomba haya maafa tusiyashughulikie wakati ambapo yametokea, kwa sababu wanasema *prevention is better than cure*, tujifunze kutokana na maafa ambayo tayari yameishatokea. Tungejifunza kutokana na maafa yaliyotokea Kivukoni nadhani tusingepatwa na maafa ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, naomba kama tumejifunza kutokana na maafa ya Kilombero, tukaweza kuwatengenezea daraja basi ajue Kigoma kuna matatizo katika Mto Malagarasi. Kivuko cha mto Malagarasi upande wa Irangala ni kile cha mwaka 1947. Ni kile ambacho kinavutwa kwa kamba na kiko hatarini. Kwa hiyo, tunaomba katika makadirio kama siyo ya mwaka huu kwa sababu Bajeti imeshapita basi Bajeti ya mwaka 2004 watujengee daraja katika kivuko cha mto Malagarasi upande wa Irangala. Ni huu mto ambao tunategemea tukivuka pale tuweze kusafirisha mpunga baada ya kutengeneza barabara kutoka Kalya kwenda Kigoma na kivuko hicho sasa hivi kiko hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi Katibu Mkuu wa CCM bado kidogo atumbukie majini. Kwa hiyo, tunatahadharisha kivuko cha mto Malagarasi kitengenezwe ikiwezekana tujengewe daraja. Kwa sababu mto huo vile vile una mamba. Kwa hiyo, ikitokea kwamba kivuko kinazama hata wale wanaojua kuogelea watapambana na mamba.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama aliiongelea Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba basi kwa sababu usalama katika Mkoa wa Kigoma sana sana ni matatizo ya wakimbizi. Tunaomba kwa sababu sasa hivi wakimbizi wanaamua kurudi wenyewe basi tuwape moyo na sisi wenyewe tujaribu kuhimiza kwamba warudi makwao kusudi Mkoa wa Kigoma uweze kuwa na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea usalama katika Mkoa wa Kigoma. Katika maafa ambayo tunapata vile vile kuna maafa ya Ukimwi. Lakini kwa suala la Ukimwi, mimi ninachofikiria ni kwa ajili ya kuwasaidia wale ambao tayari wameathirika. Madawa ya ugonjwa wa Ukimwi yana gharama sana na siyo kila mtu anaweza kuyanunua. Kwa hiyo, katika fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya kupambana na Ukimwi, basi wasaidiwe kuwanunulia dawa watoto yatima pamoja na wajane yaweze kuwasaidia kuwaongezea muda wa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya Ukimwi tunaomba basi sehemu ambazo hazijaweza kupata elimu ya Ukimwi ambazo najua zipo kutokana na kwamba miundombinu ni mibaya ziweze kushughulikiwa haraka sana. Ni sehemu nyingi ambazo kwa kweli fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya kupambana na Ukimwi, lakini hata hamasa hazijafika katika sehemu hizo.

Naomba Wizara inayohusika ikisaidiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali waweze kuziona hizo sehemu na kuweza kufikisha huduma zinazohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko. Kama nilivyosema kuna vitega uchumi vingi katika sehemu nyingi Tanzania. Mkoa wa Kigoma tunayo asali na nilikwishaongelea. Hii asali sio kwamba imekosa soko, tumeshughulika soko limepatikana, lakini namna ya kuitoa asali Mkoa wa Kigoma na sehemu nyingine kuipeleka Dar es Salaam imekuwa ni matatizo. Kwa kuwa kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kusaidia viwanda vidogo vidogo basi tunaomba wananchi au wanaushirika wa *UKI* wasaidiwe kupata fedha kusudi waweze kusafirisha asali yao, waweze kununua vifaa vya kuhifadhi asali na iweze kufika Dar es Salaam kusudi iweze kuuzwa nchi za nje na kuwapatia kipato wananchi. *(Makofi)*

Vile vile kwa sababu sasa hivi kuna mashine ndogo ndogo ambazo zinauzwa na tunajua zilipo tunaomba akinamama ambao wanajishughulisha na ufugaji nyuki basi wasaidiwe katika hizo fedha zilizotengwa kusaidia waweze kununua mashine ambazo zitawasaidia kuchuja asali na kuweza kuuza nje na kujipatia kipato. Nashukuru sana kwamba kuna chombo maalum kimeundwa kuwashughulikia wanafunzi wa Elimu ya Juu, kuwapa mikopo. Naomba basi hiki chombo kiwe wazi kusudi wanafunzi ambao ni watoto wa maskini waweze kupata mikopo na waweze kujiendeleza kielimu.

Mheshimiwa Spika, huduma za mama na mtoto kwa upande wa afya bado zinahitajika katika sehemu nyingi. Katika sehemu ya Ilagala nimeshangaa kwamba kuna sehemu ambapo mwanamke anatembea kilomita 15 kwenda kujifungua au kupata huduma za kliniki. Tunaomba sehemu kama hizo ziweze kufikiwa kusudi akinamama waweze kusaidiwa na wenyewe wafaidi nchi yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa Nchi wanaofanya kazi kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ndiyo nasimama mara ya kwanza toka tuanze Bunge hili nichukue nafasi hii kwa kweli kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioingia Bungeni kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi kutoka kwenye Majimbo mbalimbali na kwa nafasi hiyo hiyo niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa tiketi ya Chama cha *CUF* walioingia Bungeni. Vile vile niwapongeze waliorudi kwa tiketi ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kuipongeza kwa utekelezaji wa kazi wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mambo mengi ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyoahidi katika uchaguzi wa mwaka 2000 yanafanyika na yanaonekana dhahiri kwa wananchi wa Tanzania. Nataka nichukue mifano michache tu niipongeze kwa ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu. Nipongeze ujenzi wa barabara kwa kutumia fedha za ndani na hili lililofanyika sasa kwa kuwaondolea wananchi kero ya kodi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze vile vile Serikali kwa miradi mbalimbali ambayo inafadhaliwa na *TASAF* kwa nchi nzima na kwa jimbo langu la Sikonge niipongeze kwa kukamilisha Mradi wa Umeme Wilayani Sikonge. Ujenzi wa Nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge na kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya *DC* na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Haya yote yanafanyika kwa Serikali kutekeleza Ilani ya Uchaguzi mambo ambayo iliahidi katika uchaguzi wa mwaka 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kule jimboni huwa nawaambia wananchi unajua kuna tatizo unaweza ukifika mahali usiaminiwe kwa kauli unazozisema. Haya yote niliyoyasema yanaonekana machoni mwa wananchi. Sasa uwe unatoka Chama Tawala, lazima ujue kwamba haya yanafanyika na yanaonekana. Wewe unatoka Upinzani lazima ujue kwamba haya yanafanyika na yanaonekana machoni kwa wananchi. Sasa ukienda kwa wananchi ukasema kwamba hayo hayapo utaonekana ni mwongo na hata siku moja huwezi ukapata kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nataka kusema kwa ufupi leo Kiongozi wa Upinzani alipokuwa anawasilisha hotuba yake nilikuwa namfuata sana. Nataka ninukuu maneno machache katika kifungu kidogo tu alichosema kwamba: “Mheshimiwa Spika, Vyama vya Upinzani vimekuwa vikishutumiwa na kusemwa na viongozi wa Chama Tawala, kwamba mambo yake ni ya kuishia Ukumbi wa Maelezo na

haviendi kwa wananchi huko vijijini. Viongozi na Wabunge wa baadhi ya vyama hivyo wameanza kwenda huko wanakoelekezwa kwenda matokeo yake imekuwa nongwa na kununiana.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachosema twende tukafanye kazi ya kisiasa ya kuamsha vyama vyetu au kuweka nguvu ya vyama vyetu. Tusiende kule kwa wananchi kuwatusi, kuwatukana wawakilishi halali wa wananchi.

Mimi kwangu hamjafika, lakini nawakaribisheni njooni kwa sababu mtasema kesho mimi nipo, lile Jimbo nakaa nalo mimi siku zote. Kwa hiyo, wewe utasema siku moja unaondoka. Hii itatuletea vurugu leo nilikuwa nasoma gazeti moja limeandika na lilikuwa linamnukuu Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa linasema: “Baada tu ya kikao cha Bajeti Jimbo la Mheshimiwa Sumaye na Simpasa litavamiwa.”

Jamani haya ni majimbo halali na wananchi walipiga kura, wakawachagua hawa kwamba ni wawakilishi wao. Sasa mtindo wa kwenda unavamia Jimbo mwisho unaweza ukafika mahali ukasahau Jimbo lako, kafanyeni kazi kwenye majimbo yenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la Utawala Bora nathamini sana mchango wa Mahakama, lakini kwangu kule Jimbo langu la Sikonge nilikuwa naleta kero na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli kama hili haliwezi likafanyika kwa muda mfupi mpaka mwaka 2005 basi wananchi wa Sikonge wataendelea kubaki katika hali ya kunyimwa haki ya Mahakama. Kutoka Sikonge mpaka Tabora Mjini ni kama kilomita 71 hivi. Tunayo Mahakama moja tu ya Mwanzo huitegemei Mahakama moja ya Mwanzo ifanye kazi ya kuwahudumia wananchi wa Jimbo lote la Sikonge katika matatizo yao mbalimbali. Mtu akishajiona ana kesi basi anatafuta utaratibu wa kuihamisha kesi yake Tabora. Kwa maana ya kwamba huyu aliyekwenda kushtaki pale kama hana uwezo wa nauli ya kila siku kwenda na kurudi Tabora maana yake kesi hiyo ikishakosa mashahidi kule Tabora kesi imekwisha. Sasa huku ni kuwanyima haki wananchi ambao kwa kweli hawana uwezo kutafuta haki yao ya Mahakama. Hilo moja.

La pili, suala la Polisi. Nimekuwa naisikia Wizara ya Mambo ya Ndani kila wakati hapa inajibu kwamba ili tulete *OCD* ni lazima tujenge nyumba ya *OCD* na tujenge kituo kikubwa cha Polisi.

Mimi hili silielewi kwa sababu baada tu ya uteuzi mwaka 1995 *DC* alikuja hana silaha alikuja akakaa na wananchi wa Sikonge mpaka sasa hivi tuna Ma-*DC* karibu wawili walipita, yule mwingine tunaye wa tatu tunaendelea kufanya naye kazi. Sasa kwa *OCD* ambaye kwa kweli ana silaha, walinzi hawawezi kuja kukaa kwenye yale mazingira, inakujaje ina mantiki gani. Nilikuwa naomba uteuzi unapofanyika wa *DC* basi Mahakama ya Wilaya iwepo mara moja na *OCD* awepo mara moja pale kumsaidia kufanya kazi.

Sasa *boss* nani yaani *DC* wangu wa Sikonge awe anatoka Sikonge kumfuata *OCD* Tabora kila wakati kweli. Kwa sababu huu Ukuu wa Wilaya unaelea elea, hapa unakuwa hauna hadhi.

**MBUNGE FULANI:** Au Mbunge.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mimi simfuati *OCD*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatuahidi mambo makubwa mawili. Sasa nataka niseme ingawa zile Wizara hazijafikia mimi niko hapa kwa kweli kusubiri hizo Wizara. Ya kwanza Wizara ya Ujenzi. Kwa kweli barabara yetu ya kutoka Tabora, kupita Sikonge, Ipole mpaka Rungwa, ninaomba sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, wakati utakapokuwa unawasilisha hoja yako yaani hili liwepo. Nimeanza kusikia fununu kwamba inawezekana ipo, lakini mimi nitakaa siku hiyo nasubiri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nilikuwa naiomba sana Wizara inayohusika na masuala ya simu. Kwa Makao Makuu ya kila Wilaya hebu hili mngeliharakisha mnawapa shida sana watendaji wa Serikali kwenye Wilaya hata zile Wilaya mpya na si Wilaya mpya tu kuna Wilaya zingine za siku nyingi mpaka sasa hazijapata simu za kisasa. Urambo imepata Mkuu wa Wilaya mwaka 1975 mpaka leo wana simu za kukoroga. Hii kwa kweli naomba Wizara hii ihakikishe inalifanyia kazi na mlikwisha tuahidi

kufikia mwaka 2003 mwishoni mtahakikisha Urambo na Sikonge tuna simu. Kwa hiyo, tunakaa tunasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kusema kwa ufupi sana suala la kilimo. Nianze na suala la kilimo cha umwagiliaji bado halijaenea sana katika maeneo mengi sana nchini. Lakini nilichokuwa nashauri bado Serikali kwa kweli ihakikishe inaendelea kuwashawishi watu wafuate kanuni bora za kilimo. Waliolima mapema mwaka huu ambao hakukuwa na mvua nyingi waliolima mapema wamepata chakula. Kilimo cha kwanza mvua zile za mwanzo zinaponyesha ni za kupanda sio za kuanza kulima huwezi ukafukuzana na mvua. Sasa watu tumekaa tunasubiri umwagiliaji, umwagiliaji utakuja lini? Tuendelee kuwafundisha wakulima wetu waendelee kuhakikisha kwamba wanalima kwa kufuata kanuni bora za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni suala la tumbaku hili siwezi nikaacha kulisema. Sasa wale wanaosema tumbaku. Nianze kuishukuru sana Serikali na Makampuni yanayonunua tumbaku kwa kweli mwaka huu hatuna mgogoro mkubwa sana katika masoko ya tumbaku. Kazi iliyofanyika ni nzuri na mimi yule Bwana Collins, amekuja mpaka ofisini kwangu tumekaa naye inaelekea sasa muafaka upo katika suala la soko. Mimi nina jambo moja tu ambalo nataka kushauri Bodi ya Tumbaku inawezekana ikaendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa shughuli zetu za soko hasa katika kipindi hiki.

Mwaka huu tulifungua masoko yetu mapema sana. Mheshimiwa Makamu wa Rais, alikwenda kufungua masoko mapema sana. Lakini Bodi ya Tumbaku imepanga ratiba za masoko mara moja kwa mwezi. Hutegemei tumbaku iishe, inaweza ikaenda ikaisha mpaka mwezi wa kumi. Watu wanataka maandalizi mengine ya kilimo kingine kijacho.

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali ihakikishe kwamba Bodi inahakikisha kwa namna yoyote ile masoko yanakwisha haraka ili wakulima wetu waanze maandalizi upya kwa kilimo kinachofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaida yangu sipendi kugongewa kengele. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu jioni hii.

Kwanza kabisa, ningependa nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja hii bila matatizo yoyote na ningeiomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tuunge mkono hoja hii ili Serikali iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Vile vile nimepata faraja kubwa kwamba Bajeti tumeipitisha wote tuliokuwepo kwa asilimia mia moja, hakuna hata Mbunge mmoja aliyetoka nje safari hii. Hili ni jambo la kujipongeza na kwamba katika hoja hiyo ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kulikuwepo na mambo mengi mazuri sana yanayolenga wananchi wetu na hasa hii kero kubwa ya kufuta kodi ya maendeleo.

Sasa suala hili la kufuta kodi ya maendeleo kumekuwa na maneno kwamba Chama cha Mapinduzi kimedaka sera za watu wengine. Hili si kweli, kwa sababu suala hili la kufuta kodi ya maendeleo limeanza kuzungumzwa ndani ya Bunge hili kabla Mfumo wa Vyama Vingi haujaanza, likizungumzwa na Wana-CCM. CCM katika Ilani yake na Ilani zake huko nyuma imekuwa inaweka wazi kwamba itaendelea kuondoa kero za wananchi hatua kwa hatua kulingana na hali ya uwezo uliopo wakati huo. Sasa kufuta kodi ya maendeleo ni kipimo halisi kwamba tumezidi kujiimarisha ukusanyaji wetu wa kodi za Serikali Kuu umekuwa ni mkubwa na ndiyo maana tunaweza tukakusanya zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi, kwa hiyo, tunaweza kufanya uamuzi mkubwa kama huo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, si jambo kwamba sera yetu inasema futa kodi unasema futa kodi, haitekelezeki namna hiyo kwamba uamuzi huu ulikuwa mkubwa ningependa pengine nitoe *dilemma* moja niliyoipata mimi katika ziara zangu vijijini.

Mama mmoja mzee alikuwa anaomba kodi ya akinamama ifutwe. Kwa hiyo akaeleza hivi kwamba: "Wakati wa ukoloni kulikuwa na kodi ya kichwa waliokuwa wanalipa walikuwa wanaume." Kwa hiyo, kwa wale ambao walikuwa hawana uwezo ukifika wakati wa msako wanaume walikuwa wanakimbilia porini, lakini akinamama wanabaki nyumbani na watoto na baadaye akinamama wanawafuata waume zao kwenda kuwapa chakula huko walikojificha. Baada ya hapo anasema lakini sasa tunalipa kodi ya maendeleo wanaume na wanawake. Kwa hiyo, ikitokea wakati wa msako kama hatuna uwezo baba anakimbilia porini na mama anakimbilia porini tunaacha watoto peke yao nyumbani."

Kwa hiyo, akaniuliza Mheshimiwa Mbunge hivi kati ya hali hizo mbili ni upi ulio utawala bora zaidi? Nisingependa nieleze nilijibu vipi, lakini sasa baada ya uamuzi huu tulioufanya Bungeni hapa ni kwamba nitarudi kule kijijini nikaonane na yule mama kumwambia kwamba Chama cha Mapinduzi kimedhamiria kuondoa kero si kwa wanawake tu ni kwa wananchi wote na ndio uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa nizungumzie juu ya kilimo. Ambapo katika Bajeti imeelezwa pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mbegu bora za kisasa, mbolea na madawa yatasimamiwa na Serikali kwamba yanapatikana kwa bei iliyo nafuu kwa mkulima na kwamba Serikali itafidia bei ya mbolea kwa mikoa ile minne yaani Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Huu ni uamuzi mzuri wa kupongeza. Lakini ningeiomba sana Serikali isimamie mpango huu maana imeelezwa kwamba mwaka jana fedha za mboleo katika ule Mfuko wa Pembejeo wa Taifa niliwahi kuzungumzia huko nyuma kulikuwa na mkataba kati ya Serikali na *Exim Bank* halafu ndio wame-*administer* hiyo. Kama ilifanya kazi mahali pengine mimi sifahamu. Lakini kwa upande wa Iringa, Wilaya ya Iringa ninayoifahamu mimi huu mpango haukuwafikia wakulima kabisa na umeleta kero kubwa sana, kwa sababu mbolea hiyo haikuwafikia wakulima. Kuonyesha haikuwafikia ni kwamba Mfuko wa Mbolea ambao *average* unaweza kuwa shilingi 9,000 au 10,000 ulifikia mpaka shilingi 20,000 mpaka 25,000. Ndiyo kusema kwamba hawa Mawakala waliopewa hizo fedha hawakununua mbolea yote na hawakufikisha kwa walengwa.

Kwa hiyo, lazima hizo fedha zimetumika kwa mambo mengine. Kwa sababu kwa nini mbolea ipande namna hii kama ilikuwa nia ni kusaidia iweze kufika kwa wakulima.

Kwa hiyo, ningependa safari hii Serikali katika kusimamia ikabidhi madaraka kwa Halmashauri za Wilaya, zipewe uwezo wa kusimamia fedha hizo katika ununuzi wa mbolea kwa kuwatumia wafanyabiashara, *Local businessmen*, ambao wanaweza wakafungua maduka vijijini. Uwekwe utaratibu mzuri kama ulivyowekwa wa elimu MMEM kwamba fedha zinakwenda moja kwa moja kijijini katika shule. Haiku-*hang around* hapa na ndio maana tumeweza kuwa na mafanikio makubwa sana.

Kwa hiyo, nazo hizi zipelekwe kule na Madiwani walioko kule wapewe dhamana ya ku-*monitor* sio kusimamia maana Serikali ipo mpaka vijijini. Lakini ku-*monitor* kwamba kweli mbolea imefika, hiyo bei ni nafuu tunayosema sisi hapa. Mpango ni wazi lazima una fedha nyingi. Sasa kuna msemo wa busara kabisa wa Kihehe. Unasema hivi: *"Inzangwa ngaya mvina."* Maana yake kudanganyika hakuna mkubwa.

Kwa hiyo, wakiwemo wajanja sisi wakubwa watatudanganya. Kwa hiyo, lazima tuweke utaratibu ambao ni *water tight* ambao tukiamua hapa basi mambo haya tunayoamua kweli yafike kwa walengwa. Lakini kuwategemea Mawakala ambao wanakuwa na Kampuni mpaka kumi mtu mmoja kwamba ndiyo atawanye mbolea hiyo haiwezekani. *(Makofi)*

Halafu mikopo kwa vyama vya ushirika. Safari iliyopita kutokana na mpango huo kwa upande wa Iringa hakuna chama hata kimoja cha ushirika kilichopewa mkopo, kwa sababu kwamba hawana *collateral*. Lakini sheria ya ushirika nimeshazungumzia hata huko nyuma, sheria ya ushirika inaelekeza kwamba Serikali ihakikishe kwamba *at its inception* inavilea vyama vya ushirika kuhakikisha kwamba wanapata mikopo ili vyama hivi viweze kupata mtaji vikue na kujitegemea.

Sasa fedha zikipelekwa *Exim Bank* ndio hao wanatafuta *collateral* na wale hawana wajibu wa kuvilea vyama vya ushirika, kwa hiyo wanakataa.

Sasa mimi naomba pamoja na kwamba wakulima hawana *collateral* waaminike wakulima na wanaaminika kwa sababu hata wakati wa uchaguzi tunakwenda kwao tunaomba kura

tunawaamini kabisa kwamba watafanya maamuzi yaliyo ya busara. Ndiyo maana huweza kutuchagua Wabunge wa CCM kushika Serikali kwa sababu ndicho chama pekee kilicho na uwezo wa kuweza kuongoza Taifa hili kwa muda mrefu ujao. *(Makofi)*

Tazama safari hii mwaka uliopita kupitia mradi wa MMEM tumepeleka fedha kwa mabilioni vijijini na matokeo yake hakujawahi kuwa na mafanikio makubwa kama haya ya MMEM kwa sababu tumewaamini wakulima.

Sasa hili suala la *collateral* ya wakulima huku vyama vyenyewe havijafufuka vinafufuliwa sasa inakuja wapi. Kwa hiyo, tuhakikishe hii ni wajibu wetu Serikali kuhakikisha kwamba kweli hawa wakulima ambao ndio walio wengi tunawapa huduma hiyo. Maana kuna wengine ambao huwa wanaonyesha hizo *collateral* wafanyabiashara wakubwa wamepewa kupitia *import support* fedha nyingi sana, lakini je, si tunajua wamekuwa wanadaiwa kiasi gani mbona walionyesha *collateral*.

Lakini baadhi yao ndio wengine wamekuwa wadanganyifu, lakini sio wakulima. Kama MMEM kutaweza kuwa na *shortage* ya fedha kidogo ni fedha kidogo kidogo ile ya kulamba lamba, sio ile ya kuchota. Pengine ni vyema kuzitumia Kamati za Bunge sasa jinsi ilivyokuwa *constituted* ili kunapotokea matatizo tuweze kupeana mawazo ya kuondoa matatizo hayo mapema na Kamati za Bunge zisiwe za kufanya *post-mortem* baada ya kuona jambo limeharibika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni juu ya kusindika mazao ambalo limeelezwa vizuri. Kwa upande wa Iringa. Mimi ningependa kweli Serikali iweke mpango madhubuti kwa ajili ya kusindika matunda kama nyanya, vitunguu, *pears* na kadhalika. Kwa sababu nyanya tunapata kwa wastani wa zaidi ya tani 120,000 kwa mwaka, nyingi zinaoza tu. Kwa hiyo, naiomba Serikali maana yake imesema itaweka *guarantees* kwa ajili ya mikopo ya watu ambao wanaweza wakawekeza. Tuanze na wawekezaji wa ndani wapewe *guarantees* kwenye Mabenki yetu ili waweze kujenga viwanda vya kusindika mazao. Tusingojee tu wanaotoka nje tutumie watu wetu tusindike mazao. Kwa mfano kama kule Iringa kuna kiwanda fulani kinaitwa *Asas Diaries* kina-*process* maziwa. Kimefanya kazi nzuri sana mpaka kimepewa tuzo ya kwanza kwa nchi nzima.

Ningependa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana *Asas Diaries* wa Iringa kwamba wameweka mfano wa namna ya kuwa na viwanda ambavyo vinaweza vikasindika mazao yetu. Kwa hiyo, kama tulivyobinafsisha Benki kama *NBC* za nini hizi kama haziwezi kutumika kutoa mikopo ambayo wananchi wakatumia kuanzisha viwanda vya kusindika. Tumebinafsisha vya nini. Kwa hiyo, Benki hizi zijue kwamba zina wajibu huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya tumbaku. Mwenzangu toka Tabora amesema mambo ni mazuri, lakini mimi Iringa mambo sio mazuri hata kidogo. Kule kuna wakulima wakubwa na wadogo. Hao wanunuzi ni *monopoly* pana ukiritimba katika ununuzi wa mazao kwa hiyo wanatoa bei ndogo sana ambazo zimevuruga kilimo cha tumbaku na sasa hivi wakulima wadogo Kata ya Nzishi na kata ya Kiwere wameacha kabisa kulima tumbaku na hata wakulima wakubwa nao wamevurugwa sana kiwango kwamba nao wanafikiria walime mazao mengine.

Ningeomba Serikali ilitazame suala hili kwamba hili suala la ununuzi kuwa *monopoly* halafu kama hamna namna ya kuondoa *monopoly* lakini tuweke *safeguards* ambazo zitalinda kilimo cha watu wetu yaani hao wakubwa na wadogo na hasa hao wadogo ambao wanahitaji msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningeweza kuzungumza mengi lakini nafikiri haya ambayo nimewasilisha kwa leo yanatosha na kwa vile sina Upinzani wa hoja yoyote iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ila tu kuongezea nguvu ili mambo yatekelezwe ipasavyo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia maneno mawili, matatu, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imekamilika na vile vile, ukiangalia yale mambo ambayo yaliainishwa katika hotuba yake ya mwaka 2002/2003, mengi yametekelezwa ipasavyo. Kwa hiyo, sina jambo lolote isipokuwa kuisifu na kusema kwamba na tujaribu mwaka huu kumsisitiza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ajaribu kusimamia kuona mambo yote yanatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea zaidi, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Bibi Betty Mkwasa, kwa kushinda Tuzo ya Afrika hivi karibuni. Mama huyo ametuletea sifa kubwa sana Tanzania, kwa sababu ushindi alioupata si ushindi wake peke yake, lakini ni ushindi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi hapa Bungeni tuliwapokea warembo na tulijumuika na kusheherekea nao kwa sababu ya urembo wao. Nadhani kwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Bibi Betty Mkwasa, naye angeletwa Bungeni tukampongeza kama tulivyowapongeza warembo wale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naendelea kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Waziri Mkuu alijitahidi sana kusimamia Wizara na Taasisi zote, kwa sababu yeye ndiyo Mkuu wa Askari wa miamvuli, lakini nadhani jicho lake alilitupa zaidi katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aangalie baadhi ya mambo katika Wizara hasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kupitia Kamati yangu ambayo ndiyo inashughulika na akinamama pamoja na vijana.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara ndogo ndogo wanaotoka Zanzibar kwenda bandarini Dar es Salaam, wanapata shida sana. Nadhani wote mnaelewa kuwa katika kipindi kilichopita madai makubwa ya Wizara ya Fedha yalikuwa ni kwamba, ushuru unaotozwa Zanzibar ni kidogo na ilibidi wafanyabiashara hao watozwe ada nyingine. Lakini kufikia mwaka 2000, Wizara ya Fedha upande wa Muungano ilihakikisha kwamba ushuru wote unaotozwa Bara na Visiwani ni sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sielewi ni kwa nini wale wafanyabiashara akinamama wanyonge na vijana wanateswa bandarini Dar es Salaam, wanapekuliwa mizigo yao, wanatozwa pesa na risiti hawapewi kwa madai kwamba hii ni *VAT* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kwamba, baada ya Bunge hili, Waziri wa Fedha aende na Manaibu wake wawili Zanzibar, wakati wa kurudi wavae mabaibui wapite pale bandarini ili waone jinsi Wananchi wanavyonyanyaswa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama kweli unataka kusimamia kazi, wakati mwingine ni lazima ufanye ujanja kama alivyofanya Waziri wa Ujenzi kukaa ndani ya basi na akakamata wale wanaopima mizani barabarani. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha atanipa Manaibu wake, kwa sababu wao ni wenyeji pale na wafanyakazi wote wa *TRA* ni wao wenyewe, wakivaa mabaibui hawatajulikana, watawakamata siku moja tu. Kama si hivyo itolewe kauli hapa Bungeni, kwamba vitendo vile vikomeshwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita tarehe 17 Juni, 2003 alipokuwa anazungumza Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, sikuona sababu hata moja ya yeye kuingiliwa kati kama vile amefanya uhalifu! Hata ile mada yake aliyokuwa anazungumza akakatishwa kwa sababu ameisema *TRA*, ni kwa nini asiiseme *TRA*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hapa Bungeni mwaka 2002, Inspekta Omar Mahita, alisemwa na nusu ya Wabunge na wakamtaka aje hapa ajieleze! Hakuna Mbunge hata mmoja aliyesimama hapa akamtetea ndugu Omar Mahita na yeye alikuwa hana uwezo kuja kujitetea nafsi yake. Matokeo yake, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ndiye aliyemwombea msamaha. Sasa, watu hawa wote

ni sawa sawa, ni lazima Wabunge tuwe waadilifu katika kuzungumza na katika kutetea Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kauli ya Waziri wa Fedha kuhusu Wahasibu kuwa na uelewa mdogo wa kanuni mpya za ununuzi wa vifaa na huduma, pamoja na uhaba wa elimu. Tangu mwaka 1995 tumeingia hapa Bungeni, kila Bajeti kipengele hiki kinatajwa na waliokuwepo ni mashahidi tosha. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, Mhasibu yeyote ambaye hana taaluma ya Uhasibu haibi kabisa, bali Mhasibu mwenye taaluma ya Uhasibu ndiye anayefanya mambo ya wizi ndani ya Serikali.

Sasa, sioni sababu ni kwa nini Wahasibu hawa wanakumbatiwa siku zote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kwamba baadhi ya Wahasibu wameingizwa kazini kwa sababu ya mbawa za watu wengine na nitatoa mfano mdogo tu. Hapo zamani katika nchi moja ambayo sitaki kuitaja kulikuwa na Chuo cha Udaktari. Walipelekwa wanafunzi 50 wafanye *course* ya udaktari pale kwa ajili ya maradhi ya macho. Mwaka wa kwanza walipofanya mtihani watano waka-*fail,* kwa hiyo, kati ya wale watano walio-*fail,* wanne wakaambiwa nendeni zenu, mmoja akabakishwa pale.

Mwaka uliofuata waka-*fail* tena wanafunzi watano, miongoni mwao akiwemo yule aliyebakishwa, akaambiwa abakie pale. Watu wakaulizana: “Huyu ni nani?” Wakaambiwa: “Msimguse, huyo ni wa mkubwa.”

Mheshimiwa Spika, walipofanya mtihani wa mwisho kila mmoja alikuwa katika chumba cha *operation* ili kufanya *operation* ya macho. Wanafunzi waliobakia pale walikuwa ni 40 na wagonjwa nao walikuwa 40. Sasa huyu mtoto wa mkubwa aliyekuwa kila siku anatunzwa, alipofanya *operation* akaharibu jicho moja la mgonjwa akawa anababaika, hana njia, akaenda jikoni akamkuta paka, akamtoa paka jicho lake akamuwekea mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, siku mgonjwa alipoanza kupona wakamwambia afumbe jicho moja na akaulizwa: “Mbele unaona nini?” Akasema: “Namwona Spika” akaulizwa tena: “Na pale mbele kidogo unaona nini?” Akasema: “Namwona Waziri Mkuu.” Alipobanwa jicho lingine akaulizwa unaona nini, akasema: “Naona panya.” Alisema hivyo kwa sababu paka anaona panya tu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makosa hayo yalifanyika kwa sababu huyo aliingizwa tu pale. Sasa, naomba tatizo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimamie kikamilifu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Juni, 2003 liliulizwa swali namba 72 kuhusu Nyumba za Mawaziri na Manaibu Waziri. Nyumba hizi za Dodoma nyingi zilikuwa ni za Mashirika mbalimbali. Sasa, walipokuwa wanaishi Mawaziri, Manaibu na Makatibu Wakuu, walikuwa wanalipiwa na Serikali yetu moja kwa moja, lakini ikatolewa taarifa kwamba wenye uwezo wa kununua nyumba hizo wanunue. Walionunua wamenunua, wengine wakapanga nyumba za nje na wengine wakahama, lakini katika kupanga nyumba ya nje, Serikali inagharimika fedha zaidi kuliko ilivyokuwa katika nyumba za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza zaidi na ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati ni kwamba, wale Mawaziri na Manaibu walionunua nyumba hizo wao wenyewe kwa fedha zao Serikali haitaki kuwalipia kodi, umeme wala maji, wamekosa nini hawa? Wao wamei-*save* Serikali ni kwa nini hawalipwi kima kile kile ambacho walikuwa wakilipwa zamani? Ninaomba watu hawa waonewe jicho la huruma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Naibu wake. Katika kila hafla wanazohudhuria kuhusu simu za mkononi wanapiga kelele ili bei za simu za mkononi zipunguzwe, lakini cha kushangaza mpaka leo bei hizo zipo juu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa gharama kubwa za kutumia simu za mkononi. Katika mwezi Machi, 2002 kulikuwa na mkutano Marekani, mtoa mada mmoja alisema kwamba, simu za mkononi zilianza kutengenezwa katika nchi zilizoendelea. Alisema:

“Napongeza sana kwamba watumiaji wengi wa simu hizi za mkononi wanatoka Bara la Afrika.” Kama si kejeli ni kitu gani? Mnatuminya fedha zetu, mnatutoza kodi nyingi, gharama ni kubwa, halafu eti unawasifu watu wa Afrika kwamba wao ni watumiaji bora wa simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, simu ya Dola 5 katika nchi yoyote nje ya Tanzania, ukaenda Ulaya au Arabuni unaweza ukapiga simu tatu Tanzania ukazungumza maneno yako yakamalizika. Lakini Dola 5 hizo hizo ukinunua kadi yoyote ya simu yoyote hapa, akiitikia: *“Hallo, hallo mummy,”* simu imekatika! Serikali imsaidie Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa sababu anapiga sana kelele, angekuwa hapigi kelele ningesema kwamba yeye mwenyewe ana makosa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu mama lishe. Hivi karibuni Kamati ya Maendeleo ya Jamii tulitembelea pale Mnazi Mmoja, kuna vibanda vizuri kabisa vimetengenezwa kwa ajili ya kuwasaidia hawa akinamama ambao wanatoa huduma za mama lishe ambavyo vimeanzishwa na Manispaa ya Ilala. Ninawapongeza sana na huu ndiyo utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, ikiwa tunataka kuondoa umaskini ni lazima Manispaa zetu ziweze kujenga kitu cha aina ile. Ninachoomba ni kwamba, Manispaa nyingine ziige mfano ule, lakini kodi wanazotoza ni kubwa sana yaani shilingi 15,000/= kwa mwezi. Kama kweli tunataka kuondoa umaskini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Kuondoa Umaskini) yupo na anasikia, tunaomba Manispaa waambiwe wawapunguzie akinamama wale kodi ili angalau iwe shilingi 7,500/= kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, vibanda vya aina hiyo visiishie kwa hawa akinamama tu, viende pia kwa vijana. Kuna hawa vijana wanaotembeza vitu mitaani wanaoitwa Wamachinga (japo sipendi kuwaita jina hilo) nao watengewe sehemu za kufanyia biashara zao ili wao wapate fedha na Serikali ipate kodi. Kwa kufanya hivyo, Serikali itawapunguzia shida.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia kuhusu habari za ujambazi. Nalishukuru Jeshi la Polisi na Wizara kwa ujumla kwa kufanya kazi nzuri, lakini wasilaumiwe Wananchi, wenye mahoteli, wenye *Guest Houses* na wala haitasaidia kitu kufunga *groceries* saa tano za usiku kama vitambulisho vya Taifa havitaanzishwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suluhisho pekee la uhalifu ni vitambulisho, kwa sababu hao wenye *Guest Houses* watamwelewa mtu huyu kwamba ni raia au siyo raia. Mwenye hoteli hataweza kujua huyu ni Mheshimiwa Haroub said Masoud, anatoka Unguja kwa sababu ya sura yake, huyu anatoka Burundi na wala huyu anatoka Congo, kitambulisho ndicho kitakachomtambulisha mtu, kwa sababu anatakiwa awe nacho kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwashukuru Wataalam na Viongozi wote wa Wizara zilizoko chini ya Ofisi yake kwa kuchangia katika mawazo ambayo ameyawasilisha hapa hii leo. Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wameshukuru kwa sababu ameongea kwa upana sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika suala hilo nimshukuru Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, ingawa yeye alikuwa pekee bila Wataalam, lakini aliweza kutoa mawazo mazito baada ya kuyapima na kuyaweka katika mizania.

Kwa hiyo, hii inaonyesha kwamba, ni jukumu la Waziri Mkuu ambapo Ofisi ya Bunge ipo, kujua kwamba suala la kuwa na mawazo kwa ujumla katika utajirisho wa mawazo, yeye anapokuwa na Wataalam pia ni vizuri katika Ofisi ya Waziri Kiongozi wa Upinzani kuwa na Wataalam ili kuweka mawazo yaliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amezungumzia suala la mahabusu kujazana sana katika magereza na kadhalika. Katika suala hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo ya kwa nini watu wanajazana sana. Hapa kulikuwa na mgongano wa mawazo katika kile kilichopelekea pengine watu wengi kujazana katika mahabusu hasa katika suala la ulipaji wa kodi ya maendeleo ambalo limefutwa, maana kila Chama kinataka kujigamba kwamba ndiyo bingwa kilichopelekea kodi ile kufutwa.

Mheshimiwa Spika, nadhani tusijigambe sana tukijua kwamba Watanzania walikuwa na kero na waliumia sana wakati wa kutozwa kodi ya maendeleo. Kwa hiyo, si ushindi wa CCM wala wa Chama kingine chochote. Mfano, akija Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, hapa atasema: "Nilifuta kodi ya maendeleo kwa Wanawake" Watu wa *CUF* pamoja na wa Vyama vingine walizungumza kwamba kodi ya maendeleo ifutwe, wakaambiwa ni Maprofesa uchwara! Lakini Waziri wa Fedha alipotamka kwamba kodi ya maendeleo inafutwa, Wabunge wote tulipiga makofi na nilipokwenda kule Vijijini, bahati nzuri tulikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na watu walitaka kumpokea kwa kumshangilia na kumpongeza kweli, lakini hiyo tuiache. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ni kwamba, Wananchi walisikia Wabunge tukishangilia kwamba kodi ya maendeleo ilikuwa ni kero. Kwa kawaida ukifanya kitu chochote kile kibaya hata kama umemuibia mwenzako, umempiga kofi au umemfanyia kitu kibaya, unapomrudishia kile ulichomuibia au ukakiri kwamba nilikupiga kofi, basi unamuomba radhi.

Kwa hiyo, kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetambua kwamba ilisababisha kero kwa miaka zaidi ya 20 kwa Watanzania, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa ana-*windup,* basi awaombe Watanzania radhi kwa kuwasababishia kero hiyo kwa miaka hiyo ya utozaji kodi kwa kuwapiga mbele ya wake zao na mbele za mama wakwe zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alivyotoa takwimu zake Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, kule Ileje kuna watu zaidi ya 17 walikufa, lakini kuna watu kama wawili hivi....

**MBUNGE FULANI:** Siyo Ileje, ni Mbarali.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** *Okay,* ninakubaliana na ninyi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na watu wengine kama wawili hivi walituhumiwa kwa kutolipa kodi na hivi ninavyozungumza kuna watu magereza kwa sababu hawakulipa kodi ya maendeleo shilingi 5,000/=, shilingi 3,000/= au shilingi 2,000/=.

Sasa, mtu ambaye hakulipa kiasi hicho, anamwacha mke wake miezi sita anakwenda rumande (siwezi kusema anamuacha mume wake kwa sababu wanawake walikuwa hawalipi kodi), na maana hakuna na chochote! Kwa hiyo, katika kuwaomba radhi Watanzania tungeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, awasilishe hoja hii kwa Mheshimiwa Rais kwamba awasamehe wote walioko magerezani waliofungwa kwa kutolipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba mtu mzima huwezi kuacha mke wako, familia yako, shamba na nyumba ili ufungwe eti kwa sababu hukulipa shilingi 3,000/=. Ninaamini hayo yalitokea kwa sababu Watanzania wengi ni maskini na watu hao hawakuwa na uwezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia suala la ulinzi na usalama na wengi tumezungumza. Lakini napenda kusema kitu kimoja kwamba, Rais wa Uganda katika kitabu chake kinachosema "*What are the African problems?*" ambacho Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikitolea utangulizi anasema, alitoka *Ntare High School* kuja Tanzania kumsikiliza Mwalimu Nyerere anapozungumzia kuhusu amani anazungumza nini. Ingawa wote hapa mnaelewa sitaki kuendelea huko, lakini alijifunza *system* moja katika masuala ya usalama wa Balozi wa Nyumba Kumi, yeye anasema Manyumba Kumi.

Mheshimiwa Spika, Rais Yoweri Museveni, amekwenda akaifanyia *system* hiyo, utaratibu mpya ndani ya nchi yake ambapo sasa anapigana na Kongo, Rwanda na kadhalika, lakini kwa wote wanaokwenda Bukoba ukitaka kupitia Nairobi utaingia kule usiku, bila kujali ni saa kumi au ni saa ngapi na hakuna anayepigwa na wala hakuna anayeibiwa!

Mheshimiwa Spika, system ile aliifanyia kitu ambacho huko wanaita yellow sea, tunawaomba watu wa usalama na wengine mwende mkaone, kwa sababu Waziri Mkuu amezungumza suala la watu waliokwenda JKT na mgambo kushiriki katika ulinzi kama jukumu la Watanzania wote kwamba wanalinda nchi yao. Alivyofanya Rais Yoweri Museveni nadhani si vibaya, kwa sababu alikuja akaiba kwetu na akaenda kufanya *modulation*, sasa na sisi tunaweza tukaangalia amefanyaje. Ukifika pale Mwenyekiti wa Kitongoji ana silaha, machine gun mbili, tatu, pamoja na mgambo wake, kwa hiyo, kama wewe ni jambazi watakukamata tu.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema hapa kwamba, majambazi ni ndugu zetu, wengine wanasema siyo ndugu zetu. Lakini ukweli ni kwamba, ni ndugu zetu na tunawafahamu kabisa, kama siyo ndugu zetu, basi wamelala kwenye lodging zetu, Kijiji chetu au Kata yetu, tunawafahamu.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, hata Vyombo vya Usalama vinafahamu. Ninataka nilete ushahidi, lakini siyo hapa nitauleta kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, sijui kama Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, yupo hapa?

**WABUNGE FULANI:** Yupoo.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Kama yupo anajua, mumuulize na mmuombe awasaidie, kule kwetu ni mpakani amewakaba kweli majambazi. Vyombo vya Usalama wanajua fulani ana bunduki, hakuna cha kwamba yeye ni Mwenyekiti wa *TLP* wala wa CCM, ni Diwani wa *TLP* au CCM au ni Mbunge wa *TLP* au wa CCM. Kama una silaha kinyume cha utaratibu wanakukaba kweli, aliwakaba sana na ninampongeza. Tunaomba katika kuchangia uzoefu tumuulize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Marekani wakajua *Al-Qaeda* wanafanya nini, sisi tuna watu wa usalama hapa tunawalipa, pamoja na Polisi, Mgambo, Sungusungu, Balozi wa nyumba kumi na kadhalika halafu tusiweze kujua ni nani anavuruga na nani ana bunduki, tunawajua lakini tunaangaliana usoni. Kwa hiyo, nadhani tukishirikiana katika hilo majambazi tutawakomesha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia suala la Ubinafsishaji. Katika suala hili ni lazima tuwe makini kwa sababu nchi yetu ikiwa katika mfumo wa kijamaa pamoja na nchi nyingine walikuwa wanazungumzia suala la mabepari, bepari ni bepari tu, yaani suala la kumiliki uchumi kuwa mikononi mwa watu wachache.

Mheshimiwa Spika, wakati ule *Marxist* wengi akina Nabdele na Profesa Issa Shivji pale *University of Dar es Salaam*, walizungumza jinsi watu hawa ambavyo wangeweza kusababisha Mabenki na nchi hizo kufilisika! Sasa, hili la kusema kuhusu wazawa haiwezi kutusaidia. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, Serikali inajitoa kule kote kwenye biashara, inakwenda kwenye huduma za jamii. Katika utandawazi utawapa wageni Mabenki, Viwanda, dhahabu na kadhalika, siku nyingine wakiamua kukuadhibu watasimamisha kila biashara. Je, utamtoza nani kodi na hiyo huduma ya jamii na afya utailipaje? Ni lazima ujiulize hilo swali, huwezi kuwaachia hivi hivi tu!

Mheshimiwa Spika, katika suala hili *we have to be very careful*, Tanzania ni nchi ndogo. Alisema Kim Jong II katika kitabu chake cha *The immortual Juche Idea*, akim-*quote* baba yake Kim Ill Sung anasema: *"Even the best medicine should be best prescribed in order to cure the disease that was intended for."* Huwezi kuwa na *chloroquine* unataka kuwatibu, kwa sababu hujui tu unataka kumpa mara ya kwanza vidonge kumi, mara ya pili kumi, atakufa au unampa mgonjwa kidonge kimoja kimoja! Sasa, hilo suala la kujua kwamba hiyo dawa ipo inatibu Malaria, lakini inatibu kwa utaratibu gani? Kwa hiyo, katika suala hili la ubinafsishaji, siyo suala la kwamba tumeagizwa na *World Bank* au tumeagizwa na Wataalam kutoka nje, basi sisi tunakubali tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Taifa tunaachia tu raslimali halafu mnazungumza tuna-*reserve*. Wamekuja watu wanawekeza pale kwenye Mgodi wa Dhahabu, wanakwambia tumekopa fedha kutoka Benki ya Dunia au Benki nyingine wala hujui, kumbe anavyokwambia amekopa Dola milioni 10 yeye amekopa Dola milioni 5 na ili aweze kuilipa itamchukua miaka mitano na ili achimbe dhahabu ile anajua ni miaka sita, ili akudanganye kwamba baada ya mwaka ule mmoja uliobaki ndiyo nitapata faida. Atakudanganya utapata shida kweli na ndivyo wanavyotufanya, halafu tunakuja hapa tunacheka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la *AGOA*. Alikuwa anashangaa na analalamika na sisi tunashangaa na tunalalamika na watu wengine walioko Vijijini kwa sababu hawalijui, kwa hiyo, hawashangai wala hawalalamiki! Sasa, katika hatua hii nani anamsaidia nani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *AGOA*, ukienda Afrika Kusini wanauza magari, wala siyo bidhaa za kilimo, ni magari! Nilikuwa nasoma taarifa moja hapa ya Afrika Kusini, wanauza magari kwenye soko la Marekani chini ya mpango wa *AGOA*, ninyi mna nyumbu mmeharibu tu. Mna *gallery* la nyumbu tu, wala hamtaki kuendeleza wala nini, mnaharibu tu!

**MBUNGE FULANI:** Nyumbu! Nyumbu ndiyo nini? *(Kicheko)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, katika suala la *AGOA*, utaratibu uliokuwepo katika mila na utamaduni wa Watanzania na wafanyabiashara chini ya Siasa ya Ujamaa kwa vyovyote waliofanya biashara walikuwa ni Waarabu na Wahindi waliokuwa na uraia wa Tanzania na mwelekeo wao na incarnation yao ni Uarabuni na Bara Hindi. Ukiwaambia *incarnation* yao iende Marekani sasa hivi katika mpango wa *AGOA* na wao wanaanza upya, huo ni ukweli na ni lazima tuutambue na tuubaini na tukiishaubaini tuweke mkakati kwamba tunakwenda kwenye *AGOA* kwa namna gain? Ni nani anamuelimisha nani? Wale Watanzania Waarabu wao wanauza mafuta, wana vituo vya mafuta *everywhere* na Wahindi wengi wana biashara za maduka tu.

Mheshimiwa Spika, haya mazao ya kilimo, mfano Kahawa ya Kagera uweke kwenye kiwanda kama kile wanachokoboa, sijui kinaitwaje Mheshimiwa Wilfred Lwakatare! Kiwanda hicho kipo pale, wanakoboa na wanasaga hadi ile Kahawa inakuwa ya unga kabisa, usipoosha hawatajua!

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, Mawaziri wetu kila mara wanafanya kazi *on the table*. Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Edward Sokoine, walikuwa wanakwenda kutembelea mashamba, lakini huyu Waziri anakaa tu pale, tunataka mwende kule. Waziri wa Kilimo na Chakula, uende Kagera uone jinsi mashamba yalivyoharibika, *it's a shame*. Nilikuwa na Mheshimiwa Nazir Karamagi, pamoja na wengine, nawashangaa, sijui hapa mnafanyaje! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukienda *practically* kujua kwamba ni kitu gani kipo kwenye *field* itatusaidia katika ku-*device* na kufanya *projects* tunazofanya, lakini ukisubiri wataalam wakuletee, wanakuletea kwa nadharia gani? Nadharia ya hali halisi ya Kitanzania au nadharia aliyosoma Marekani au kule Urusi ama kwingine?

Mheshimiwa Spika, kuna mwaka watu wa Burundi walikwenda Uarabuni wakawa wanachukua maharage ya Karagwe wanayapeleka huko, wanapewa mafuta halafu sisi tunaaangalia tu kumbe wao wanafaidi na yapo mambo mengi ya namna hiyo.

Kwa hiyo, mpango wa *AGOA* si suala la kuwahutubia watu, tunataka watu wawe makini, wafanye utafiti, tuelimishane, tujadiliane na kila mmoja ajue, kwa sababu tuna utamaduni fulani wa kufanya biashara na watu wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kama Waziri atajibu kwamba atamwomba Mheshimiwa Rais awasamehe wafungwa walioko magerezani kwa sababu ya kutolipa kodi ya maendeleo na kwamba anawaomba Watanzania radhi kwa sababu Serikali iliwasababishia kero, basi nitaunga mkono hapo baadaye. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabla sijasahau, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wa Nchi, wataalamu wote, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutuletea hotuba ambayo imejaa vitu vyote ambavyo tulitaka tuvisikie. Hotuba hii kwa kweli imesheheni mambo yote ambayo tulipenda kuyaona hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini na kwa niaba ya Mkoa wa Tabora, naomba nitoe tena shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuja kutuwashia mwenge mwaka huu. Wananchi wa Mkoa wa Tabora tumefarijika sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuja Tabora kuwasha mwenge tarehe 7 Juni, 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nawaita wanasiasa wachanga ambao wanabeza mbio za Mwenge. Wanawaambia wananchi Mwenge haufai, msije kwenye Mwenge. Kule Tabora waliambiwa wananchi kwamba msiende kwenye Mwenge, waacheni waende hao watu wa CCM.

Sasa mimi nasema hawa wasiasa wachanga wangekuja pale Tabora tarehe 7 Juni, 2003 wakasikia majibu ya wana Tabora waliyoyatoa. Uwanja wa Tabora ulijaa, ukajaa na kujaa na kusheheni, haijapata kutokea. Ulijaa kama vile ilitokea namna hiyo wakati wa kampeni za mwaka 2000 na kwenye ujio wa Papa John Paul II. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania wana akili timamu kabisa, wanajua mbio za mwenge zinaleta mshikamano, udugu, upendo, na miradi bwelele kwa wananchi. Kwa hiyo, wanawashangaa hao wanaosema Mwenge umepitwa na wakati. Wananchi wa Tabora wanashukuru sana Serikali kuwapa nafasi ya kuwashwa Mwenge Mkoani Tabora mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wanyamwezi tuna msemo mmoja wa Kinyamwezi. Leo Mheshimiwa George Mlawa, alisema kwa Kihehe, mimi nitasema kwa Kinyamwezi halafu nitatafsiri kwa kiswahili. Wanyamwezi wanasema: *"Vudugu lupambala"* maana yake undugu ni kutembeleana, kwa hiyo, wanasema viongozi wakubwa wa Serikali mje muwatembelee ndugu zenu wa Tabora. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu hatujatembelewa na viongozi, lakini tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini alikuja kwa siku moja na nusu hivi na vile vile Mheshimiwa Makamu wa Rais naye alikuja kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Tabora wamenituma kwamba Viongozi wa Serikali njooni Tabora muwatembelee ndugu zenu wa Tabora. Maana waswahili wanasema mgeni njoo mwenyeji apone. Tunajua kabisa viongozi hao wakubwa watakapofika Tabora hawawezi kuja mikono mitupu au siyo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Naomba msikie rai ya wananchi wa Tabora. Napenda kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa juhudi zake kubwa za kuungana na wananchi wa Mkoa wa Tabora. Serikali hii imeunga nguvu za wana Tabora katika kuufungua Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Tabora maombi yao ni kama yafuatayo. Wanaomba Mkoa wao ufunguliwe, wanaomba barabara ya Dodoma - Manyoni - Itigi, ijengwe na kuwe na mpango wa mbele wa kutuwekea lami kwa sababu na sisi tunataka lami. Hili suala la kila siku kuwa na kokoto, kokoto hapana na sisi tunataka lami. *(Makofi)*

Barabara ya Tabora- Ipoe - Koga - Mpanda, barabara ya Tabora kwenda Kigoma, Tabora kwenda Nzega barabara hizi zote ni za changarawe, sasa tungependa tuanze na changarawe lakini kuwe na mpango madhubuti ambao utasema mwaka 2007 na kadhalika, barabara hizo zitakuwa za lami ili na sisi tuonje matunda ya Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika ukurasa wa 55 naishukuru sana Serikali kwa mpango mzuri wa kueneza *Television* ya Taifa, tumeambiwa kwamba Mwanza, Dodoma, Arusha, Tabora, Mbeya na Lindi watapata huduma hiyo. Niseme kwamba wananchi wa Mikoa hii kwa kweli wanasubiri kwa hamu kubwa kabisa kupata huduma hii ya *Television* ya Taifa. Sisi wananchi wa Tabora tumeshajitolea kupeleka kokoto kule hata kwenye mlima ili kujenga hiyo minara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tuambiwe ni lini wanataka kujenga na tutakuwa bega kwa bega na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ili kuwaletea huduma ya *Television* ya Taifa wananchi wa Mikoa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Katika *speech* ya Bajeti ya Waziri wa Fedha alikuwa amependekeza pale mwanzo kuongeza *excise on airtime* kwa asilimia 2 kutoka asilimia 5 mpaka asilimia 7. Ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inawajali wananchi wao na kusikia kilio cha wananchi na ikaiondoa hiyo kodi kwa kusikiliza ushauri wa wananchi.

Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Maana kama mwenzangu Mheshimiwa Haroub Said Masoud, alivyosema mpaka hivi sasa huduma ya simu bei yake bado iko juu sana ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Sasa ushauri wangu kwa Serikali naomba kupendekeza, kwa nini tusiangalie uzoefu wa wenzetu wa nchi jirani Uganda na Kenya wanatoza kodi gani katika huduma hii? Ili na sisi tutoze kodi hizo hizo maana tunaungana sasa na hizi nchi. Tusipokuwa na mawasiliano mazuri tutashindwa kufanya kazi na tutashindwa kuweza kushindana na hawa wenzetu wa Uganda na Kenya, tuangalie hizo kodi zinatozwaje ili na sisi tuweze kufikisha huduma hii kwa wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili ningependa Serikali itueleze imefikia wapi kwenye *Rural Telecom Fund* maana tungependa wananchi wetu wa vijijini ambako ndiko kuna watu wengi, wapate huduma hii. Wananchi wa Sikonge, Urambo, wananchi wa Uyui na vijiji vingine vyote vya Tanzania hii wangependa waweze kumudu hizi huduma. Kwa kweli huduma hizi kama tulivyoona zinaweza kuwafikia wananchi kwa haraka kabisa kuliko ilivyokuwa zamani kwa kutumia waya, tunataka hizi ambazo si za waya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie kasi ya ubinafshaji na urekebishaji wa mashirika ya umma. Sisi pale Tabora kilio chetu kikubwa ni ile kampuni ya *TABTEX,* kampuni ya *TABTEX* kwa kweli kwa wananchi wa Tabora ndiyo mhimili mkubwa wa maisha ya wananchi wa Tabora.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye haraka iwezekanavyo ili hicho kiwanda kiweze kuwapatia kazi na kama ni kubinafsishwa au kurekebishwa basi wafanye haraka ili wananchi wa Tabora wapate ajira. Kiwanda hiki ndiyo kilikuwa kinaajiri wananchi wengi wa Tabora na hivi sasa hakifanyi kazi. Tunaambiwa kimepelekwa *LART,* sasa hawa wa *LART* wasianze kupiga miguu, miguu, mwaka mmoja, miaka miwili na wananchi wanaendelea kukosa kazi. Tunaomba mtusaidie kufanya haraka kwenye kiwanda hiki ili wananchi waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala kubwa la reli. Reli zetu hizi kama tunavyojua huko mbele tuna mpango wa kubinafsisha ile biashara tu, lakini barabara za reli nazo zinahitajika kujengwa. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba tuanze sasa kuwekeza kwenye barabara za reli maana sisi wengine kama wa Tabora mpaka sasa tunategemea sana reli, ndugu zangu wa Kigoma wanategemea reli, ndugu zangu wa Mpanda, Singida reli ndiyo muhimili wao katika Songea bado, wangependa reli itoke Mtwara kwenda Songea.

Hizi ni fedha nyingi sana za kujengea barabara za reli. Mara nyingi mtaalam wa mambo haya ya uchumi wa barabara za reli ndugu yangu Mheshimiwa Ally Karavina, kama alivyosema tukiziendeleza hizi reli kwa kweli tutapata fedha nyingi sana. Kuna soko kubwa sana nchi za *Democratic*

*Republic of Congo*, Burundi na Rwanda, ambalo linatungojea tu. Lakini hatuwezi kufanya hivyo reli zikiwa katika hali zilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapopewa kitu lazima ushukuru, naomba tena nishukuru kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kutusaidia wananchi wa Tabora kupata *X-ray* imeshafika Tabora. Lakini basi tunaomba watusaidia pia kupata vyombo vya *mortuary,* jengo tumeshaanza kulijenga na karibu tunalimaliza. Jamani tusaidieni na sisi wana Tabora tumalize hiyo *Mortuary* ili tuweze kuwahifadhi ndugu zetu wanapokuwa wametutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kengele inigongee maana nina nidhamu sana ya muda kwa haya machache niliyosema naomba kusema tena kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu asilimia mia . Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii muhimu ili niweze kuongea moja kwa moja na Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kwenye uchaguzi mdogo hasa wale waliotoka kwenye Chama cha Mapinduzi, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yeye pamoja na wasaidizi wake wote, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, pamoja na Watendaji wote waliohusika katika kurekebisha na kuleta hotuba hii nzuri katika ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu alipotembelea Mkoa wa Mwanza alifanya kazi mbalimbali za maendeleo na baadaye alitoa ahadi ya shilingi 500,000/= katika Shule ya Sekondari ya Busongo. Napenda nimhakikishie kwamba ahadi hiyo tumeshaipokea na kuifanyia kazi ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Unapompongeza Waziri Mkuu si peke yake, Waziri Mkuu ana timu na timu hiyo ni mali ya Chama cha Mapinduzi nao ni askali wa miavuli. Nawapongeza sana kwa kazi ambayo mnaweza kumsaidia Waziri Mkuu na baadaye kufanya kazi yake kwa raha mstarehe. Hongereni sana Mawaziri na Manaibu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nigusia katika ukurasa wa 44 katika Hotuba ya Waziri Mkuu suala linalohusu maji. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yako umezungumzia suala la maji, lakini niseme kwamba miji inayokuwa kando kando ya Ziwa kama Misungwi, Bukoba pamoja na Musoma ina matatizo makubwa ya maji kuliko sehemu nyingine yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji kwa mji wa Misungwi ni kubwa sana. Bunge lako tukufu kwa mara ya kwanza nilizungumzia maji, nikapewa ahadi, mwaka 2002 nimezungumzia maji, ahadi ikabaki iko pale pale. Nianze kuwapongeza kwa sehemu kidogo Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa juhudi ambazo wameweza kuzifanya. Wamejitahidi wamezungumza na *ADB* ikashindikana, wamezungumza na *European Union* hawakuweza kufanikiwa lakini bado juhudi zimeendelea wameongea na Wafaransa kwa bahati nzuri wameonyesha nia ya kutupa mradi wa maji katika Mji wa Misungwi, Bukoba pamoja na Musoma. Nawapongeza sana kwa hatua hizo za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Waziri Mkuu aangalie kwa macho mawili *Central Tender Board* ina matatizo makubwa sana. Wafaransa wameshakubali kutoa msaada huo lakini *Central Tender Board* hawajakaa miezi nane mpake leo hii. Kuna tatizo gani huko? *CTB* ina matatizo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimeongea na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Ruth Msafiri, analalamikia matatizo ya maji katika Mji wa Bukoba, Mheshimiwa Wilson Masilingi, analalamikia maji katika mji wa Bukoba hata Dr. Diodorus Kamala, amezungumzia suala la Maji bado Mheshimiwa Wankanga Marwa, amezungumzia masuala ya maji katika Mji wa Musoma. Tatizo bado *Central Tender Board* hawajakaa. Je, hiyo bahati tuikose? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri alishughulikie hilo na katika majumuisho yako ukipata nafasi ningefurahi utueleze kwamba ni lini watakaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa unyenyekevu mkubwa kabisa Wananchi wa Misungwi kama tatizo ni pesa wako tayari kuchangia kikao hicho cha *Central Tender Board* wakae ili tuweze kukamilisha hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la TAMISEMI. Wizara hii huenda ni pana mno, ina majukumu mengi, kazi yake kwa kweli sasa hivi hasa vijijini haionekani. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu una nafasi kubwa ya kuweza kumweleza mwenye Wizara kwa maana ya Rais wetu tuna matatizo makubwa sana. Nimezungumzia barabara ya kutoka Manawa, Mbalika, kupita Kasololo, Nduha bado haijatengenezwa. Nimemwomba Naibu Waziri, atembelee huko aweze kuona hajapata nafasi ya kufika eneo hilo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali nisaidie katika eneo hilo ili iweze kupitika. Wananchi wa Mbarika wana matatizo makubwa mno. Naomba hilo ulitatue ni sehemu ya kero naomba ulitatue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie ushirika. Katika ukurasa wa 23 Waziri Mkuu amezungumzia suala la ushirika, ameelezea vizuri na nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ushirika na Masoko kwa kazi nzuri anayoweza kufanya katika suala la kufufua ushirika. Amejitahidi sana na katika hatua za awali pesa za kununulia mazao kwa Vyama vya Ushirika zimeshapatikana.

Nampongeza sana kwa hilo anaendelea vizuri. Sasa hivi kuna imani kwa Vyama vya Ushirika karibu asilimia 80. Bado kuna masuala madogo madogo ambayo tunafikiri kutokana na hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, umeeleza kwamba wataleta sheria hapa katika kipindi hiki, isomwe kwa mara ya kwanza na baadaye iweze kuletwa katika ukumbi huu na baadaye tuweze kuipitisha sheria hiyo ili tuweze kufanikisha shughuli zetu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaloomba kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba kuna matatizo makubwa sana katika Wizara hii hasa kwa upande wa bodi za mazao. Bodi za mazao kukaa upande wa kilimo ni tatizo.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwezekana bodi zote zitolewe zipelekwe kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko. Sioni kuna sababu ipi ya msingi ya kubaki Wizara ya Kilimo. Waziri wa kilimo ana kazi nzito kama mambo ya *research* mimi sina matatizo. Ukiriguru ibaki kwenye upande wa Wizara ya Kilimo sina matatizo, Uyole Mbeya nayo ibaki kilimo sina matatizo nayo, lakini bodi zote za mazao zirudishwe Wizara ya Ushirika na Masoko wauze kwa urahisi. *(Makofi)*

Sasa hivi msimu wa pamba kwa mfano utafunguliwa tarehe 30, watu wa Ushirika na Masoko hawana habari mpaka wakaazime maneno kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula. Wizara ya Kilimo na Chakula ina shughuli nyingi mno. Mheshimiwa Waziri Mkuu wapunguzie mzigo hawa watu wa Wizara ya Kilimo na Chakula, bodi zote zirudi Wizara ya Ushirika na Masoko tuwahoji vizuri ili waweze kufanikisha shughuli zao kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihamie kwe-nye Wizara ya Ujenzi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi John Pombe Magufuli, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Katika Wilaya ya Misungwi tulikuwa na barabara moja mbaya mno. Barabara ya kutoka Mwanangwa, Misasi, Salawi mpaka Mwagirigiri sasa hivi ni nusu lami, nawapongeza sana. Isipokuwa kulikuwa kumebaki na kipande kama robo hivi nina imani mtaikamilisha. Tatizo kubwa lililobaki ni Daraja la Mto Mwame. Niliwahi kulizungumza hapa matatizo ni makubwa sana, daraja hilo limewahi kuleta ajali na wananchi wetu wakapoteza maisha yao. Sasa hilo katika hotuba yako nadhani unaweza ukaligusia ili liweze kutatuliwa. *(Makofi)*

Lakini bado barabara ya Furo Nyambiti, Mheshimiwa Richard Ndassa, alizungumzia hiyo, lakini mmetengeneza nusu imebaki nusu. Sasa nakuomba katika Bajeti hii uweze kulifikiria ili iweze kukamilika.

Nigusie suala la mawasiliano. Sasa imefika mahala sisi wananchi wa Kwimba na Misungwi, tumechoshwa na ahadi zisizo na mwisho za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Tutakoroga simu mpaka lini?

**WABUNGE FULANI:** Mpaka liamba.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Sasa tumechoka tunahitaji simu na sisi za wa wakati. Tunawauliza wanaambaa ambaa tu wanasema suala lako tunalishughulikia, mnalishughulikia mpaka lini? Tunahitaji mawasiliano. Kumpata Mkuu wa Mkoa ni shida, ukikoroga ikishindikana mpaka ubande mahali, utafute ukoroge ufanye nini, haiwezekani hiyo tunataka simu za kileo, tumesubiri tumechoka. Hilo nakuachia ulitatue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kupambana na wahalifu kwa juhudi mnazozifanya hongereni sana. Lakini katika kidogo mtakachokuwa mmepata katika Bajeti hii, muangalie sana Idara ya Zimamoto, imesahaulika kabisa. Juzi tu tumepata ajali katika jengo letu la Ushirika. Msaada tulioupata kwenye hiyo idara ya Zimamoto labda kupewa namba ya simu ili tumpigie yule *Night Support* wakati Wizara yenyewe imo humo humo ndani na hicho kitengo cha Zimamoto kipo hapo wangeteketea wote. Wizara ya Viwanda na Biashara nayo iko pale. Hivi hii Idara hamuishughulikii? Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu uko hapa liangalie hilo. *(Makofi)*

Mwisho naomba niongelee juu ya nyumba za askari. Hivi hawa askari mbona hamuwakumbuki? Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu uko hapa hata kwa kuanzia hapa Dodoma mmeshindwa? Kuna Misonge ya mabati, watumishi wanakaa humo, unaridhishwa na Misonge hiyo? Wafanyakazi kwa saa 24 akipata hata dakika mbili ya kwenda kupumzika, akapumzike wapi? Nadhani katika Bajeti ijayo kwa sababu Waziri yupo basi naomba ujumbe huu umfikie moja kwa moja yeye mwenyewe, Mheshimiwa Waziri wakumbuke sana askari hata kwa kuanzia Makao Makuu ya nchi yetu askari wake wawe na maisha bora, siyo bora maisha. Hilo nakuomba sana Waziri liangalie lisije likawa ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo hakuna marefu yasiyo na mwisho, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaruhusu pesa alizoomba Waziri Mkuu, apewe kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii ya pekee kabisa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Lakini kabla ya hapo nitumie nafasi hii vile vile kuwapongeza sana na kuwakabirisha Waheshimiwa Wabunge, wote waliopata ridhaa ya wananchi kujiunga na sisi katika Bunge hili tukufu nasema karibuni sana.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni hotuba nzuri ambayo imejaa matumaini. Mimi nimeipokea kama alama ya ukombozi wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuzungumzia suala zima la elimu nchini. Ninapoingeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ilizozionyesha kwa kuboresha elimu ya msingi nchini. Haijawahi kutokea toka tupate Uhuru mamilioni ya fedha kufika vijijini kwa ajili ya kuimarisha elimu ya msingi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iendelee na mkakati wa kuboresha zaidi mazingira ya elimu ya msingi. Lakini pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha elimu ya msingi bado kuna matatizo ambayo nadhani tukirekebisha elimu ya msingi nchini itaboreka zaidi. Kuna matatizo makubwa ya madai ya walimu wetu wa shule za msingi. Walimu wa shule za msingi wanadai haki zao hawalipwi, ikiwa ni pamoja na mapunjo ya mishahara yao, uhamisho, marekebisho ya Ikama na ajira mpya ambazo zilitokea hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matatizo makubwa kwani walimu wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Sasa inapotokea hata haki zao za msingi wanashindwa kuzipata kwa kweli hatuwatendei haki. Tunazungumzia utawala bora unaozingatia sheria na haki za binadamu, sasa mtu unapochelewesha malipo yake unakiuka haki za binadamu. Hili ninaishauri Serikali iliangalie walimu wetu waweze kupata haki zao kama inavyostahili na baadaye waweze kuipenda kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kielelezo kabisa mimi nina kielelezo cha madai ya walimu wa jimbo langu la Bukombe wanadai jumla ya shilingi milioni 176. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo linapelekea kuwavunja mioyo walimu wetu. Serikali ninaomba iangalie lile liwezekanalo kulipa madai ya walimu si walimu wa Bukombe tu bali walimu wote wanaoidai Serikali. Serikali ichukue hatua za kulipa madai yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine la fedha za *captation* ambazo zinapelekwa kwenye shule zetu za msingi nazo haziendi kulingana na uwiano wa wanafunzi walivyo. Kwa hiyo, Serikali hili nalo iliangalie kwa sababu inachangia sana kudorora kwa elimu. Mahitaji yanaposhindwa kukidhi haja kunakuwa na utata katika utoaji wa elimu katika shule zetu za msingi. Naomba nizungumzia suala la elimu ya sekondari. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu hili amelitolea taarifa na ameonyesha jinsi gani Serikali imejiandaa kupambana nalo. Kwa kweli Elimu ya Sekondari katika nchi yetu ilikuwa nyuma mno. Ilifika mahali hata vijana wetu wanaofanya vizuri kwenye Elimu ya Msingi wanashindwa kujua waende wapi kwa sababu Elimu ya Sekondari tulikuwa bado hatujaiandalia mazingira ya kupokea wanaofaulu kutoka kwenye Shule za Msingi. Sasa naomba mazingira ya Elimu ya Sekondari yaboreshwe, Sekondari zetu zipewe kipaumbele. Mikakati iliyotumika kuboresha Elimu ya Msingi, basi itumike kuboresha Sekondari zetu nchini ili ziwe na uwezo wa kupokea vijana wetu ambao wanafaulu kuingia Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la madini. Sekta ya Madini ni sekta muhimu sana katika Pato la Taifa. Lakini sekta hii bado sera zake hazijawa wazi. Asilimia zinazotolewa kwa ajili ya sekta hii hazilingani na uharibifu unaojitokeza katika maeneo husika. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili upya ili iweze kuongeza angalau asilimia sita kwa ajili ya uharibifu ambao unatokea. Lakini vile vile Sera ya Madini haijawa wazi kwa wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wamekuwa wakivumbua dhahabu, lakini bahati mbaya sana hawapewi hata haki ya kumiliki maeneo ambayo wameyavumbua na matokeo yake ni kufukuzwa, wanamilikishwa wachimbaji wengine na hasa wa kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi wa wazi kabisa kwenye eneo moja linaloitwa Kigosi, kuna Kampuni moja imejitokeza ya *Tancan*. Wachimbaji wadogo waligundua dhahabu eneo hilo wakaanza kuvuna, lakini sasa kuna mwekezaji wa nje amekuja amemilikishwa eneo hilo na wao hawana haki tena katika eneo hilo na anachodai sasa, yeye anasema anafanya utafiti. Sasa sijui ni utafiti wa namna gani wakati wachimbaji wadogo tayari walikuwa wameanza kuvuna. Hili nalo Serikali iliangalie kwa sababu linachangia kwa kiwango kikubwa sana kuipotezea Serikali yetu mapato. *(Makofi)*

Naomba nizungumzie Sekta ya Nishati. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa juhudi inayoendelea kuzionyesha kwa kupeleka umeme mpaka Vijijini. Umeme ni maendeleo. Sehemu zote ambako umeme umepita utakuta maendeleo ya kweli yamepatikana, kwa sababu palipo na umeme hata wawekezaji wanaweka viwanda na vijana wetu wanapata ajira, lakini hata mazao ya wakulima yanasindikwa na hivyo yanakuwa na bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ajabu lakini ni kweli kwamba tuko kwenye karne ya 21 ya sayansi na teknolojia miaka 42 baada ya Uhuru, baadhi ya Wilaya hapa nchini bado hazijapata huduma hii muhimu sana. Baadhi ya Makao Makuu ya Wilaya hapa nchini hazina huduma ya umeme na hata wafanyakazi wake wamedumaa kiakili. Kazi inayopaswa kufanywa pengine siku moja, basi wao wanafanya wiki nzima. Wanahangaika na Ma-*PS* wao kufukuzana na mafaili, wenzao wanafanya kazi kwa kutumia *computer*. Kwa hiyo, hili suala linarudisha nyuma sana maendeleo ya nchi na hasa kwenye Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Sipingi maeneo ya Vijijini kupelekewa huduma ya umeme lakini kwa kweli Makao Makuu ya Wilaya ni muhimu sana kwa sababu Makao Makuu ya Wilaya ndiko kuliko na takwimu zote za nchi, takwimu zote za maendeleo na takwimu zote za huduma za jamii. Haiingii akilini kwamba Mkuu wa Wilaya anapopata dharura pengine saa moja usiku aende ofisini kwa kutumia kibatari na unapeleka umeme Kijijini unamkuta Balozi wa nyumba kumi yeye anatumia umeme. Kwa hiyo, ni jambo la ajabu sana.

Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya zote ambazo bado hazijapatiwa umeme ikiwemo Wilaya ya Bukombe. Wilaya ya Bukombe tuna bahati kubwa sana. Wilaya ya Bukombe ina uwezo wa kuzalisha mazao ambayo yanahudumia Mkoa wote wa Shinyanga mpaka imevutia hata wawekezaji wamewekeza viwanda vya kuchambua pamba. Lakini wawekezaji wameshindwa kuviendesha viwanda hivi kwa sababu ya gharama kubwa ya kuendesha viwanda kwa kutumia jenereta. Sasa naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka umeme katika Wilaya ya Bukombe. Serikali kwa maelezo yake inasema, uchumi umekua kwa asilimia sita, sasa wananchi wa Bukombe watanufaika vipi na kukua kwa uchumi huu? Kwa sababu nimejaribu kuangalia katika Bajeti hii, upande wa mawasiliano Bukombe hatuna hata simu. Mwaka 2002 Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba katika mwaka huu wa fedha Wilaya ya Bukombe itapatiwa huduma ya simu, lakini nimeangalia kwenye mpango wa maendeleo, Wilaya ya Bukombe haijapewa hata huduma ya simu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwaeleze wananchi wa Bukombe katika Bajeti hii ambayo tunaisifia, wananchi wa Bukombe wamenufaika na nini? Kama ni kodi ya maendeleo ni wananchi wote hata wale ambao wamepelekewa umeme Vijijini wamepunguziwa kodi ya maendeleo. Sasa wananchi wa Bukombe wamenufaika na nini katika Bajeti hii ambayo kwa kweli ni ya aina yake?

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaomba Serikali iungane na wananchi wa Bukombe ambao kwa muda mrefu hawakuwa na Hospitali ya Wilaya na hivi sasa wamejitahidi wameanzisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Wamejenga wodi nane za akina mama wajawazito, watoto pamoja na akina baba. Lakini sasa wameanzisha ujenzi wa jengo la utawala pamoja na Maabara. Naiomba Serikali iungane nao kuhakikisha kwamba jengo la utawala lililoanzishwa basi limekamilika ili wananchi wa Bukombe waweze kupata huduma ya afya kama Watanzania wengine. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, kwa sababu malalamiko ya wananchi wa Bukombe nimeyawasilisha na Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajali mno malalamiko ya wananchi, nina imani kwamba malalamiko haya itayafanyia kazi. Nasema naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kazi iliyopangwa kufanyika siku ya leo imekamilika, lakini kabla sijaahirisha Bunge tangazo hili nitakalolitoa si sehemu ya shughuli za Bunge, linatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge wajue tu ili mwenye nafasi aweze kwenda kushiriki. Nalo ni kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kesho tarehe 24 Juni, 2003 wanafanya kumbukumbu ya wale wahanga waliopata ajali ya treni tarehe kama ya kesho mwaka 2002, wanafanya kumbukumbu katika makaburi yao, mara baada ya kuahirisha kipindi cha asubuhi cha Bunge saa saba. Kwa hiyo, atakayepata nafasi ya kushiriki anaarifiwa hivyo.

Baada ya hapo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi .

*(Saa 01.38 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne*
*Tarehe 24 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*